

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 14 Februari, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Sita, Kikao cha Kumi tarehe 14 Februari, 2022. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2021.

**MHE. DENNIS S. LONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2021.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mawasilisho.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 106

**Mpango wa Kujenga Wodi ya Kinamama Wilaya ya Mbozi**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi mpya ya akinamama Wilayani Mbozi itakayokuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya akinamama wengi kujifungua?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali Mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe itakayogharimu jumla ya shilingi bilioni 12.26 mpaka kukamilika kwake. Hadi kufikia Disemba 2021 shilingi bilioni 9.8 imetolewa, ambapo jengo la *OPD* limekamilika na ujenzi wa wodi ya mama na mtoto unaendelea na unatarajiwa kukamilika Disemba, 2022.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Mbozi ambayo kwa sasa inatumika kama Hospitali Teule ya Mkoa wa Songwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa bado changamoto ni kubwa sana katika hospitali ya Wilaya ya Mbozi, na fedha ambazo tayari zimepelekwa hazijatosha kumaliza changamoto katika wodi ya wazazi. Nilikuwa nataka kufahamu, kwa nini sasa Serikali isifikirie kutuungezea fedha katika mwaka ujao wa fedha ili kuweza kumaliza changamoto zilizopo katika wodi ya wazazi likiwemo suala la upanuzi pamoja na ukarabati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu la pili, wanawake wa Mkoa wa Songwe katika Wilaya za Mbozi, Ileje, Songwe pamoja na Momba tuko vizuri sana katika suala la kuijaza dunia. Kitakwimu, katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi wastani wa watoto 450 huzaliwa kwa mwezi. Kutokana na changamoto hiyo Hospitali hii ya Wilaya ya Mbozi iko katika Kata ya Vwawa, na kata hiyo mpaka sasa hivi ninapoongea hakuna kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu, kwa nini sasa Serikali isifikirie kutujengea kituo cha afya katika Kata ya Vwawa ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue mchango wa Mheshimiwa Mbunge kwa wanawake wa Mkoa wa Songwe; amekuwa akifanya kazi. Ndiyo maana kama unavyoona, katika swalii lake la kwanza ambalo ameliuliza hapa, anasema Serikali ifikirie kuongeza fedha kwa ajili ya kusaidia ile wodi ya akina mama na watoto ya Hospitali ya Mbozi ambako yeye mwenyewe safari iliyopita kabla ya Bunge hili alikuwa hapo na ameahidi kulikarabati jengo hilo. Kwa hiyo nimponeze kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho ninaweza nikakisema ni kwamba Serikali imepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge ambapo katika swalii letu la msingi tumejibu kuwa katika mwaka unaofuata tutaweka milioni 50, lakini pia tutazingatia kwa kuangalia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuhusu kujenga kituo cha afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Kata ya Vwawa, na hili tumelipokea. Kwa sababu moja ya malengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, ombi lake nalo tumelipokea ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wanawake wa Mkoa wa Songwe na kazi nzuri ambayo wanaifanya ili kuhakikisha tunakisaidia Chama chetu Cha Mapinduzi pamoja na kuwasaidia wananchi ambao wana imani na Serikali yao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, nimekuona.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watu wenye ulemavu wanahitaji *privacy* zaidi na miundombinu rafiki wakati wa kujifungu. Je, Serikali inaonaje ikatenga vyumba maalum ambavyo vitatumika na wanawake hawa wenye ulemavu wakati wa kujifungua pale wanapoitokeza? Ahsante.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha watu wenyewe mahitaji maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza kabisa naye nimpongeze kwa kuwa anafanya kazi nzuri ya kufuatilia watu wenyewe mahitaji maalum nchi nzima. Hili alilolileta hapa kama swali. Ameeleza vizuri, kwamba watu wenyewe mahitaji maalum wanahitaji *privacy*, na je, Serikali tunalionaje hili kama moja ya mahitaji yetu ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyezekiti, niseme kwamba tumepokea mawazo na mapendekezo yake, na tutalipeleka katika timu yetu ya wataalam ili kuhakikisha kwamba walau katika baadhi ya hospitali na maeneo yote ambayo huduma ya afya inahitaji tuweze kutenga hivi vyumba maalum ili kuwasaidia wenzetu wenyewe mahitaji maalum. Kwa hiyo, tumelipokea na tutalifanyia kazi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na maswali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile hayuko tumeambiwa Kiongozi wa Shughuli za Bunge leo atakuwa ni Mheshimiwa George Huruma Mkuchika. Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo kwenye majukumu maalum, na barua nimeandikiwa, iko hapa mezani kwa ajili ya taarifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkuchika atakuwa ndiye kiongozi badala ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Tunaendelea na maswali, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini sasa aulize swali lake.

### **Ujenzi wa Madaraja ya Gunyoda**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je ni lini serikali itajenga madaraja ya Gunyoda na Baray ikizingatiwa kuwa madaraja haya ni muhimu sana katika kuunganisha Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Halmashauri ya wilaya ya Mbulu na Karatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Korongo la Gunyoda lenye urefu wa mita 70.4 na kina cha mita tano lipo barabara ya Waama-Masieda katika ya kata ya Gunyoda, Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na umuhimu wa daraja la Gunyoda ambalo linaunganisha Halmashauri za Wilaya ya Mbulu, Karatu na Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Serikali kuitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imetetenga bajeti katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu ili kufahamu gharama halisi zinazohitajika katika ujenzi wa daraja hilo. Baada ya kukamilika kwa upembuzi na usanifu wa barabara hiyo, Serikali itatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya barabara ya Waama – Masieda yenye urefu wa kilomita 19.98 lenye korongo la Gunyoda

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya kilometa 17.25 za barabara zilifanyiwa matengenezo kwa shilingi milioni 70.25. Kwa upande wa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya kilometa 14.2 zitatengenezwa kwa shilingi milioni 34.22 na Mkandarasi ameanza kazi za matengenezo na zitakamilika mwezi Mei, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara katika Jimbo la Mbulu kulingana na upatikanaji wa fedha, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu za jamii na kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangulize masikitiko makubwa ya majibu ya Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri alijejibu swali hili alijibu swali hili hili katika Bunge liliopita. Leo nilipoona swali hili limerudishwa kwa makosa kutoka swali lile la kwanza nililopenda kuuliza nikaacha kwa sababu nimetumiwa jana jioni. Lakini majibu yaliyotolewa ni tofauti kabisa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoystoa kule mwanzo kwenye Bunge liliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi niiombe tu Serikali kwamba, tunachouila hapa ni ujenzi wa Daraja la Bunyoda ambalo Serikali imepigwiwa kelele kwa miaka tisa. Na Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa majibu mazuri sana kwenye Bunge liliopita, kwamba usanifu wa daraja hili ni bilioni moja na milioni mia mbili. Leo jibu liliokuja ni kwenda kufanya usanifu upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kama Mheshimiwa Waziri atarejea kwenye majibu yake arejee, lakini kwa Bunge hili linalokuja daraja hili lisipowekwa kwenye bajeti, nadhani nitakuwa naunga mkono bajeti ambayo haina tija kwa wananchi wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ninaomba majibu ya kina ya daraja hili kujengwa kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu ndani ya Bunge hili, akisema

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

katika mwaka wa bajeti wa 2022/2023 daraja hili litatengewa fedha bilioni moja na milioni mia mbili ambapo usanifu wake uko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa maswali mawili si ni tayari?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yalikuwa maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Basi uliza kwa ufupi tafadhali.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, eneo la Mbulu Mji lina kata 10 vijijini na kata saba mjini. Eneo lote la vijijini lina makorongo makubwa. Ni lini wataalam wa TARURA na TAMISEMI watakwenda katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ili waweze kujua namna ya kuweza kutatua tatizo la makorongo linalokabili maeneo ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu katika maeneo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, baadhi ya maelezo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyatoa tuliyatoa katika Bunge lako Tukufu, na nilishatoa maelekezo katika ngazi za chini. Kwa hiyo kitu ambacho walikuwa wameshatueleza ni kwamba walikuwa bado hawajafanya usanifu, isipokuwa walitupatia zile gharama za awali, kwamba wanakadiri daraja lile litagharimu bilioni moja nukta mbili. Kwa hiyo sisi ambacho tunahitaji ni *exactly figure* ili tuweze kuliweka katika bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nipokee maoni na maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Mbunge, na niahidi kwamba nitalifanya kazi, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu haitakuwa tayari kulidanganya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo hilo hatutalipokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto nyongine za wananchi wa Jimbo la Mbulu kumaliza matatizo ya makorongo kwa kujenga madaraja pamoja na kurekebisha barabara, Mheshimiwa Mbunge na hili tumelipokea, tutaendelea kufanya usanifu pamoja na tathmini na kama ambavyo kiti chako kilieleza siku zilizopita uliopita, tathmini ya awali tumeshaifanya, bado tunakwenda kufanya tathmini ya kina ili kujua ukubwa wa matatizo katika maeneo yote nchini ikiwemo Jimbo la Mbulu, na sisi tutachukua hatua ya kuyakamillsha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mheshimiwa Kakosi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liliopo katika Halmashauri au Jimbo la Mbulu halitofautiani na tatizo liliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ambapo Daraja la Godegode halipitiki kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nipate kauli ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa daraja hili ambalo limekuwa ni kiungo katika kata za jirani lakini wananchi wamekuwa wakipata shida sana katika kupata usaifiri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja ambalo Mheshimiwa Mbunge amelieleza liko katika barabara ambayo inahudumiwa na *TANROADS*. Lakini kwa kuwa Serikali ni moja na sisi Ofisi ya Rais-TAMISEMI tunafanya kwa ukaribu sana na watu wa *TANROADS* tumelipokea hilo, na kwa sababu kama ni tathmini ya pamoja tunaifanya wote kwa pamoja, hususan katika zile barabara ambazo zina mwingiliano; kwa hiyo nilipokee na hili, nalo tuahidi tu kwamba tutalifanyia kazi ili kuhakikisha kuwa wananchi wa maeneo hayo wanapatiwa huduma. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nishukuru sana Serikali kwa kuleta fedha za *TARURA* zinazojenga Barabara ya kutoka Kambanga kwenda Ifinsi na kutoka Majalila kwenda Ifinsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani zote hizo barabara ile haitakuwa na umuhimu wa aina yoyote kama hakutakuwa na bajeti ya Daraja la Mto Mnyamasi eneo la Ifinsi.

Je, ni lini Serikali itajenga daraja hilo ili iweze kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Bugu ambao hawana mawasiliano kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naye ameomba daraja, na kiukweli madaraja mengi ndiyo hayo ambayo sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tuliahidi kwamba tunayafanyia tathmini ili kuhakikisha kwamba tunarahisisha usafiri katika maeneo mbalimbali nchini. Na ahadi hiyo tullitoa ndani ya Bunge kwa sababu maeneo mengi nchi hii yanazumbuliwa zaidi na madaraja, kwa sababu, moja, ya kuharibika, lakini pili, maeneo mengine yana madaraja ambayo wakati wa misimu ya mvua yanakuwa hayafikiki kabisa kwa sababu ni mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunatakiwa tukajenge madaraja ya kudumu ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapata huduma hiyo ya usafiri na usafirishajli wa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo ambalo amelieleza Mheshimiwa Kakoso lipo katika mipango yetu, na asubiri tu kwamba baada ya mwaka huu wa fedha, naamini yale yako ndani ya bajeti tutayatekeleza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar, nimekuona.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu alipofanya ziara jimboni kwangu tuliweza kwenda eneo moja ambako mto umekatika, mawasiliano hayakuwepo na akaahidi kutoa fedha, na bahati nzuri fedha imeshatolewa, lakini mkandarasi aliye pale ni jeuri na hafanyi kazi kama inavyotakiwa, na fedha tayari anayo.

Je, Waziri yuko tayari kutusaidia kumsukuma huyo mkandarasi aifanye hiyo kazi mara moja ili kuepusha shida

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

ya upitaji ya pale kwa sababu sasa hivi mvua zinaendelea kunyesha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilifika jimboni kwa Mheshimiwa Hussein na nilishuhudia hayo madaraja mabovu siyo moja tu mengine yameshaanza na kutekelezeka na baadha ya madaraja ambayo nilikuta katika jimbo lake ni madaraja ya miti, ambayo wananchi walikuwa wanalipishwa fedha. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tuliagiza fedha hizo ziende, sasa changamoto ambayo imetokea hapa ni mkandarasi kushindwa kufanya kazi kwa wakati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge moja nimelipokea, lakin pili kutumia Bunge lako Tukufu namuagiza huyu Mkandarasi afanye kazi kwa wakati kinyume na hapo tutavunja mkataba na kupeleka mkandarasi mwingine ili akamalizie hiyo kazi. Ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Na. 108

**Ahadi ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami – Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kilomita sita ya barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wa Makambako?

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizoahidiwa zinasimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini kwa maana ya TARURA. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kujenga kilomita sita za barabara kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Mji wa Makambako ambapo Wakala wa Barabara TANROADS alikasimiwa kutekeleza ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya kilomita 3.5 zimejengwa kwa kiwango cha lami ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.97 zilitumika katika ujenzi huo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha ujenzi wa kilomita sita kwa kiwango cha lami kwa kadri fedha zitakavyopatikana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Deus Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na niishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri ambayo imeifanya na hasa kwa barabara hizi kilomita sita na kilometa 3.5 kama alivyosema kwenye jibu la msingi zimejengwa. Kabla sijakwenda kwenda kwenye swali, nimshukuru Waziri wa TAMISEMI, Ndugu yetu Bashungwa alipopita kwenye kazi zake katika Mkoa wetu wa Njombe alikuta tuna maafa pale katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, akatoa fedha zake mfukoni kuwasaidia wahanga wale, namshukuru sana sana na wananchi wanakushukuru sana. (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, kwa kuwa kazi ni nzuri na kwa kuwa kilometa zilizobaki ni kilometa 2.5. Ni lini wataanza kuzijenga ili wananchi wa Makambako wawe na imani kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini katika kilomita hizo zilizobaki zitamaliziwa kujengwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo kwa maswali mafupi ya Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa moja ya jitihada kubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge anaifanya ni kuhakikisha hii ahadi ya Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kilomita sita inakamilika na kilomita zilizobaki ni 2.5 ambazo sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuitia *TARURA* tunapaswa kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishazungumza na Mheshimiwa Mbunge, tulishazungumza na *TARURA* Mkoa wa Njombe kuwaambia kwamba barabara hizi ziwekwe katika mpango wa kila mwaka wa fedha ili hizi kilometa 2.5 tuzimalize kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025. Kwa hiyo, matarajio yetu kabla ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2025 barabara hizi kilometa 2.5 zitakuwa zimeshakamika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimewaona Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa Kimei na Mheshimiwa Ester.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo. Nauliza kuwa, je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ya kujenga barabara ya kuanzia Gairo hadi Kata za Chagongwe na Nongwe kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWNEYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Christine kwa swali fupi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameainisha hapa ahadi ambayo imeahidiwa katika Awamu ya Nne ya Serikali na anataka Awamu ya Sita tuikamilishe kwa wakati. Jibu moja kubwa la msingi ambalo Wabunge wote wanapaswa kufahamu ni kwamba Ahadi zote za Viongozi, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumezianisha na zote zinathamani halisi ya fedha ambayo tumeziwekea kila ahadi, kama ni barabara, maji, Kituo cha Afya zote zipo katika vitabu vyetu na utekelezaji wake ni kwamba tumekuwa tukitenga fedha katika kila mwaka wa fedha. Kwa hiyo, hata hili la Awamu ya Nne na lenyewe lipo katika utekelezaji huo. Kwa hiyo, ninachowenza kukisema ni kwamba, litatekelezwa kulingana na fedha tunavyokuwa tunazipata kila wakati ili kuhakikisha tunamaliza ahadi zote za viongozi zilizopo. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Kimei na baadaye Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa nimeshatoa machozi ya kutosha mbele ya viongozi wetu wakuu kuhusiana na uhitaji wa lami kwenye barabara zetu tatu fupi pale Vunjo ambazo ni Barabara ya Uchira-Kisomachi-Kolalie, Barabara ya Pofo-Mandaka-Kilema na Barabara ya Himo Sokoni-Lotima. Nataka nimwombe Waziri kama ataridhia kuambatana nami kwenda kutembelea barabara hizi ili

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

aweze kuona uhalisia wa hadhi ya barabara hizi na kero ambazo wananchi wanapata? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante. Naomba kujibu kwa kifupi swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nipo tayari kuambatana na Mbunge kwenda kuziona hizo barabara ili tuhakikishe kwamba tunawapatia ufumbuzi wa kudumu. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru. Kama unavyojua Mji wa Bunda unakua kwa kasi na Serikali ya Awamu ya Nne iliji-commit kujenga kilomita 10 katika mitaa ya Mji wa Bunda na hasa ukizingatia sasa kuna barabara moja tu ya lami kutoka pale Mjini kwenda Bomani. Nataka nijue ni lini Serikali itakamilisha ahadi hii ya kilomita 10 ili Mji wa Bunda ufanane na Miji mingine kwa lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kama nilivyojibu awali kwamba ahadi zote viongozi zipo na tunachokifanya sasa hivi zote zimeshatengewa fedha yaani kwa maana thamani halisi. Kwa hiyo, tunavyopata fedha ndipo ambavyo tunatekeleza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nimwahidi najua Mji wa Bunda na bahati nzuri na mimi mwenyewe

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

nimefika, kwa hiyo ninachokiahidi ni kwamba zile barabara zitajengwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha hizo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbanga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 109

### **Kujenga Daraja la Kuunganisha Vijiji vya Kingoli – Litumbandyosi na Machimavyalafu Mto Ruhuhu**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja linalouanganisha Vijiji vya Kingoli – Litumbandyosi Wilaya ya Mbanga na Machimavyalafu Wilaya ya Ludewa katika Mto Ruhuhu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Liuka Kapinga Benaya, Mbunge wa Jimbo la Mbanga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la kuunganisha Vijiji vya Kingoli – Litumbandiyosi ni moja kati ya madaraja makubwa ambayo yamepewa kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kingoli hadi mto Ruhuhu yenye urefu wa kilometra 13.0 kwa sasa haipitiki kutokana na kukosekana kwa madaraja madogo ya kudumu katika Mito ya Linyanya na Nyamilola pamoja na daraja

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kubwa la Mto Ruhuhu. Hata hivyo, *TARURA* Wilaya ya Mbinga, ilitenga fedha katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2021/2022 ili kujenga madaraja mawili madogo ya Linyanya na Nyamilola na sasa hivi mkandarasi yuko anaendelea na kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhitaji mkubwa wa madaraja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na kwa kuzingatia umuhimu wa daraja linalounganisha Mkoa wa Ruvuma na Njombe kupitia vijiji vya Kingoli - Litumbandiyosi, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini itatenga shilingi milioni 25 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kufanya usanifu wa daraja linalounganisha Mikoa ya Ruvuma na Njombe lisilopungua urefu wa mita 40 ili kujua gharama halisi na ujenzi wake utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yenye nia ya dhati kabisa kuondoa adha kubwa ambayo wananchi wa wilaya hizi mbili, mikoa hii miwili ya Ruvuma na Njombe, kwa sababu mto huu una mamba wengi lakini ni mto mkubwa sana. Kwa hiyo, ni hatari kubwa sana kwa wananchi pale, kwa hiyo kwa majibu nashukuru sana. Ombi tu kwamba waharakishe ili daraja hili liweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ombi hili, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Barabara ya Unyoni kuelekea Maguhu inapitika kwa shida sana lakini ipo barabara kutoka hapo Maguhu Mapera kuelekea Kambarage, barabara hii iko hatarini kutoweka. Kuna korongo kubwa sana kutokana na mvua hizi zinazoendelea kunyeha.

Sasa je, Serikali ipo tayari kutoa fedha za dharura ili kuokoa ile barabara iweze kutumika kama inavyotumika siku zote? (*Makofifi*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu dogo la pili, jiografia ya Wilaya ya Mbinga hususan Jimbo la Mbinga Vijijini ni milima na mabonde hali ya kwamba inahitaji madaraja mengi lakini na barabara zinapitika kwa shida sana. Nahitaji *commitment* ya Serikali, je, iko tayari kuongeza fedha tofauti na ile hali ya kawaida katika Jimbo la Mbinga Vijijini? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mafupi ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Liuka Kapinga Benaya, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, bahati nzuri nilifika jimboni kwake, niliona kazi nzuri anayoifanya na jinsi wananchi wanavyomkulali kwa kuwa anafuatilia kwa ukaribu zaidi matatizo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba swali la kwanza alilouliza ni kwamba je, tupo tayari kutoa fedha za dharula ili kusaidi hili korongo kubwa linapita katika hizi barabara ambazo ameziainisha. Niseme tu katika Bunge lako Tukufu baada ya agizo la Mheshimiwa Spika tumeshafanya tathmini ya awali ya kugundua maeneo yote ambayo ni korofi nchi nzima. Kwa hiyo, ambacho tutakwenda kuangalia tu katika eneo lako la Mbinga kama maeneo hayo yametengwa. Kama halipo maana yake tutamuagiza meneja wa TARURA katika halmashauri yako afanye tathmini ili tuone namna ambavyo tunaweza tukasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusu kuongeza fedha, tumewaagiza Mameneja wote wa TARURA Mikoa pamoja na katika Halmashauri. Katika mwaka huu wa fedha, watakavyoleta zile bajeti zao waleti bajeti kulingana na uhalisia wa maeneo husika kwa hiyo, hilo ndiyo agizo. Kwa hiyo, naamini kwamba maeneo haya ambayo

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha yatakuwepo katika bajeti hizo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimewaona Mheshimiwa Injinia Ezra na Mheshimiwa Yahya.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Tatizo la madaraja katika Jimbo la Mbinga Vijiji ni sawa na tatizo la baadhi ya vijiji katika jimbo la Biharamulo. Kwa mfano; Kijiji cha Nemba kwenye Kata ya Nemba kuna Kijiji cha Kisenga kwenda Nyamazina, kuna makorongo makubwa sana watu hawawezi kupita na ni sehemu yenyewe mazao mengi Lusahunga, Midaho kwenda njia panda, Nyakahura kuna Kalukwete kwenda Msali B na Nyevyondo kwenda Ngara. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa madaraja ili wananchi hao waweze kuunganishwa na hatimaye waweze kupata huduma wanazostahili? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde kwa namna anavyojibu kwa ufasaha sana. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ambavyo *TARURA* inategemewa na Waheshimiwa Wabunge katika kutoa huduma kwenye majimbo yetu. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, juzi tuliita wakandarasi wote nchini ambao wanahudumu kuititia *TARURA*, tuliita Mameneja wa Wilaya ya Mikoa ili kuweza kujipanga vyema kufanya kazi kwa weledi katika kuhudumia barabara za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Waheshimiwa Wabunge tuwahakikishie tunajenga *TARURA* mpya. Tumejifunza upande wa *TANROADS* kwa mfano kwenye masuala ya manunuza, *TANROADS*huwa wanaanza mipango yao kuanzia Aprili kwa *assumption* kwamba haijawahi kutoka

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Wizara ikapata bajeti pungufu kwa mwaka fedha unaofuata pungufu ya asilimia 60 ya bajeti iliyopita. Kutohana na hilo *TANROADS* huwa wanafanya mipango ya manunuzi kuanzia Aprili ili inapoanza Julai 1 ya mwaka wa fedha wakandarasi wanakuwa wapo tayari kwenda site kuanza kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, utaratibu huo tunauleta ndani ya *TARURA* na tuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kuitia tozo kwa lita shilingi mia moja tayari *TARURA* kuna zaidi ya bilioni 322 kwa ajili ya kutoa huduma kwenye barabara kwenye wilaya zetu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha *TARURA* kuweza kupata Mifuko zaidi ya miwili ambayo tulikuwa nayo, Mfuko wa Tozo tumeona umeanza kutuletea fedha na Waheshimiwa Wabunge tutajipanga vizuri kuhakikisha huduma bora ya barabara za wananchi wetu vijijini na kwenye wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia kwenye mwaka wa fedha tutakaoleta Bajeti Bungeni hapa, Waheshimiwa Wabunge wataona mabadiliko na tumejipanga vizuri kuhakikisha tunafanya upembizi yakinifu mapema badala ya kusubiri kupata fedha ndiyo *TARURA* ikafanye usanifu, sasa hivi tutakuwa tunafanya mapema, tunakuwa tuna *database*, fedha inapopatikana tunakwenda kwenye utendaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye swalii la Mheshimiwa Ndugu yangu Liuka Benaya, Mbunge wa Mbanga Vijiini, ametaja barabara ambayo inaunganisha mikoa miwili. Dhamira ya *TARURA* ni kuvipa vipaumbele barabara kama hizo ni kwa sababu ni barabara za kimkakati. Kwa hiyo, tutabainisha hilo kwenye jimbo lake pamoja na majimbo yote ili kuhakikisha tunapotekeleza fedha inavyokwenda basi hiyo barabara inaleta *impactza* kiuchumi kwa wanachi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa majibu hayo ambayo naona yameleta

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

matumaini kwa Wabunge na naamini wananchi wetu watakuwa wamefarijika. Tumalizie na Mheshimiwa Yahya swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri na Waziri wake kwa majibu mazuri ya Serikali. Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwenye Jimbo langu la Nanyumbu, sasa hivi kuna kadhia kubwa ya korongo kubwa ambalo limesababisha wananchi wa Kijiji cha Chiube wawe kisiwani. Jambo ambalo limesababisha mama mmoja kujifungua kwa sababu ya kushindwa kufika hospitalini kutokana na korongo hilo.

Swali, je, Waziri atakuwa tayari kufuatana nami kwenda kuona kadhia kubwa iliyopo ambayo wananchi wa Kijiji kile cha Chiube wanashindwa kufika hospitalini kutokana na lile korongo ili tutafuta majawabu sahihi ya wananchi wale? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hiyo changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza hapa, alinieleza hata kabla hajaauliza hili swali la nyongeza na akawa ananiomba kwamba twende wote pamoja. Kwa hiyo, nafikiri amelileta hapa ili nimthibitishie kupitia Bunge. Nipo tayari kuongozana naye ili tukashuhudie hili eneo na tuweze kupata majawabu ya haraka kuhakikisha tunawasaidia wananchi wa eneo la Chiube. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri, Mheshimiwa David Silinde kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Afya; na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Na. 110

**Sababu za Kuifuta *TFDA***

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali iliifuta iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*)?

(b) Je, Serikali haioni kwa kuifuta *TFDA* itashindwa kudhibiti ubora wa vyakula ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) ilifutwa kwa kufuatia kuitishwa kwa Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka, 2019 iliyohamishia majukumu ya udhibiti wa chakula na vipodozi kutoka *TFDA* kwenda Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango (*TBS*). Lengo la kuhamisha majukumu haya ilikuwa ni kuondoa mwingiliiano wa majukumu, kati ya *TFDA* na *TBS* na kuweka mazingira wezeshi ya uendeshaji wa biashara nchini.

(b) Serikali imeendelea kudhibiti ubora wa chakula kuitia Taasisi ya Viwango Nchini (*TBS*). Aidha, wataalam wa chakula waliokuwa *TFDA* pamoja na vifaa vya maabara vya uchunguzi wa ubora wa chakula vilivyokuwa vinatumika *TFDA* vilihamishiwa *TBS* ikiwa ni pamoja na shughuli zote zinazohusiana na udhibiti wa ubora wa chakula. Hivyo, kufutwa kwa *TFDA* hakuwezi kuathiri usimamizi wa ubora wa chakula nchini. Ahsnate. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kutohana na kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukizwa yanayosababishwa na ulaji wa vyakula, kwa mfano *cancer* na viriba tumbo: Je, Serikali haioni kwamba *TBS* imeshindwa kudhibiti ubora wa vyakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa *TBS* inadhibiti ubora wa vitu vingi ikiwemo petroli, magari, matairi, *chemicals* na vitu vingine: Je, Serikali haioni kwa unyeti wa chakula ikaweza kutenganishwa na vitu hivi vingine? Ahsnate. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Neema Mgaya kwa sababu tu ushauri wake hauishii kwenye kutushauri kupitia maswali, lakini amekuwa ni mdau mzuri sana wa Wizara ya Afya katika kutoa ushauri hasa kwenye kuboresha afya za Watanzania. Swali lake la kwanza anadhani sisi hatuoni kwamba kutohana na matatizo ya *cancer* pamoja na viriba tumbo, inawezekana ikawa ni vigumu kusimamia eneo hilo kama haya mambo yataendelea kubaki *TBS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza moja, hili ni suala la kisheria. Liliuja Bungeni na ikaonekana sababu za kuweza kuhamisha hizi shughuli ziweze kupelekwa *TBS* badala ya kubaki Wizara ya Afya. Sasa, wazo lake ni zuri kwa sababu kweli kama ambavyo hata wiki iliyopita na inaonekana masuala ya *canceryamekuwa* yakisumbua watu, lakini kuna umuhimu wa masuala ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kujadiliana na Wizara ya Afya na tuko tayari kupokea maelezo na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kujadiliana na Wizara ya Viwanda, ambayo ni Wizara husika. Tukiona kuna umuhimu wa kuhamisha, basi tutarudi Bungeni kwa ajili ya kufanya hilo ambalo amelisema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba anadhani vile vile kule *TBS* wanafanya mambo mengi mengine hayahusiani kabisa na afya. Hata hivyo, nimwambie tu, hata petroli yenye *ina-impact* vile vile kwenye afya. Kwa hiyo, usipoangalia vizuri unaweza ukahamisha kila kitu ukalera afya. Kwa sababu, petroli ukienda kwa maana ya mazingira na mambo mengine bado yanarudi pale pale kumuumiza binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachowea kusema, wazo lake ni zuri, lakini ni suala la kisheria na Bunge lilikaa likapitisha, tutaendelea kukusanya maoni ya wadau, tutashirikiana na Wizara ambayo inahusika na masuala hayo. Kukionekana kuna uhitaji wa kurudi Bungeni kubadilisha sheria na mambo hayo yaje Wizara ya Afya, tuko tayari kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli *input* ya Mheshimiwa Mbunge ni muhimu kwa sababu tuna changamoto kubwa sana sasa hivi kwenye masuala mazima ya afya. Mimi nalichukua kama wazo, tunakwenda kuanza kufanya kazi. Nafikiri na mimi kuna umuhimu wa kuanza kutafakari kama anavyofikiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Florent Kyombo na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nakiri kwamba nimekuwa mtumishi wa *TFDA* kwa miaka kumi. Niseme, kuhamisha bidhaa za chakula na vipodozi kumekinzana na dhana nzima duniani ya udhibiti wa bidhaa hizo. Ukiangalia nchi zote duniani; uende Marekani bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, zote zinadhibitiwa pamoja. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani pote ndivyo ilivyo, lakini *TFDA* imekuwa ni kioo katika *East Africa*. Wamefundisha Rwanda, wamefundisha hadi Tanzania Visiwani leo tuna *ZFDA*. Kwa hiyo, kuhamisha kwenda kwenye *Bureau of Standards* ni jambo ambalo kidunia wanatushangaa. Je, ni lini sasa Serikali italeta sheria hapa ibadilishwe ili hizi bidhaa zidhibitiwe kulingana na matakwa ya kikanda na kimataifa? Nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Kwanza amesema ni *practice* ya kidunia na pia amesema kwamba *TFDA* ni mfano kwa *East Africa*. Nataka kumwambia, ni ya kwanza kwa Afrika nzima. Ndilo sasa hivi inaongoza kwa Afrika nzima kwa zile *standards* za kidunia. Kwa hiyo, kwa Afrika ni ya mfano, hata nchi zilizoendelea kuliko sisi tumewapita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mimi kama ambavyo nimejibu swali la msingi, naona kuna *element* hapo, lakini kwa sababu walioamua kubadilisha ilikuwa ni suala la kisheria na Bunge likaleta hapa Sheria Na. 8 ya Fedha ilivyobadilishwa ndiyo uamuvi ukafanyika, kwa hiyo, kabla ya kusema tutafanya nini, naomba mtupe muda wa kufanya uchambuzi wa kina kwa kushirikiana na Wizara husika ili tulete maamuzi hapa tusije tukaingilia mambo ambayo yanaweza yasitekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaelewa *concern* yenu Wabunge, tunaelewa *concern* ya swali la msingi. Tutaendelea kulichungulia vizuri na kushirikiana na wadau husika ili tuweze kuona tuendeje. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka niulize swali moja la nyongeza.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Majukumu ya *TFDA* ikiwa ni pamoja na Baraza la Wafamasia ni udhibiti wa dawa. Sasa hivi kumekuwa na tatizo kubwa sana la uuzaaji wa dawa holela ikiwa ni pamoja na hizi dawa zinaitwa P2. Nini mkakati wa Serikali wa kudhibiti uuzaaji holela wa dawa katika maduka bila kuzingatia misingi na matumizi ya dawa hizo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza kwamba kuna uuzaaji wa dawa kwa namna holela. Kikubwa wala hilo halihitaji kusema tunajipangaje. Hilo liko wazi, zipo hizo taasisi, yupo Mfamasia wa Serikali, ipo *Pharmacy Council*, wapo *TMDA* ambao ndiyo wanahusika kufanya hiyo kazi. *Straight forward* ni kwamba hatutaki kuliona hilo. Waanje kusimamia mlongozo na sheria na taratibu za kusimamia masuala mazima ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi ni agizo tu linatoka hapa kwamba inatakiwa hili analolisema Mbunge lisiweze kuonekana tena likitokea kama lipo. Tutakwenda kulifuatilia kama lipo, wanaofanya hivyo watawajibika na vile vile tutaenda kusimamia sheria kama ambavyo ilishapitishwa na Bunge. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Afya. Mheshimiwa Mwita Kimbaki Michael, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Tunza Malapo.

Na. 111

### **Tafiti za Dawa Asilia Nchini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuharakisha utoaji wa matokeo ya tafiti za ndani za tiba asilia za kutibu maradhi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mbalimbali kama inavyofanya kwenye tafiti za nje ya nchi kwa kuziundia Tume ya Jopo la Wachunguzi mapema?

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo.

**MWENYEKITI:** Yupo wapi mwenyewe? Haya mwenyewe ameshafika aulize swali lake.

*(Hapa mwenye swali la msingi hakusikika akiuliza swali lake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwitaa Kembaki Michael, Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa taarifa za utafiti mbalimbali zinazohusiana na dawa za asili zilizofanywa kuititia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (*MUHAS*) zinazolenga kuonyesha ufanisi na usalama wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili mpaka Septemba 2021, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi ya *NIMR*, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hospitali ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Rufaa ya Kanda *KCMC*, zilitokeleza utafiti wa ufuatiliaji wa ufanisi wa dawa saba za asili zilizosajiliwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa lengo la kupambana na maambukizi ya UVIKO-19. Matokeo ya utafiti huu yalitolewa na kutangazwa kwa umma kuititia vyombo vya habari mbalimbali. Ahsante. (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wakati maswali yanaulizwa tuwe makini sana. Kama Mbunge mwenzio, jirani yako au wa Mkoa wako hayupo, uwahi kuuliza. Sasa akitokea mtu mwingine yupo *sharp*, msipige kelele. Mheshimiwa Tunza Malapo. (*Makof*)

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa tunatambua...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo haki, yupo mwenyewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu tafadhali.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenyewe yupo aulize. Amka Kembaki amka!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naomba taratibu. kama mwenyewe yupo, ataruhusiwa, kama hayupo aliyemwulizia mwanzo kwa niaba ndio atauliza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Yupo!

**MWENYEKITI:** Yupo wapi?

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Nipo hapa.

**MWENYEKITI:** Haya mwenyewe aulize maswali ya nyongeza.

**MBUNGE FULANI:** Tuliza kiherehere, mwenye swalı lake yupo.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru na nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yametolewa na Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 45 ya Watanzania wanatumia tiba asili. Tunashuhudia waganga wa tiba asili wakiwapa watumiaji kwa vifungashio ambavyo siyo salama. Vilevile tunaona wanatumia vikombe kupima dawa na mengine ambayo sijayataja. Ningependa kujua, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba dawa wananchi wanazotumia ni salama na vilevile zinasajiliwa kwa ajili ya matumizi sahihi ya wananchi? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Mwitia Kembaki.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nijibu swalı la Mheshimiwa Kembaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichojaribu kusema ni kwamba asilimia 45 ya Watanzania wanatumia hizi dawa za asili ambayo ni kweli. Pia anajaribu kuonesha kwamba wakati mwingine zinafungwa kwenye vifungashio ambavyo siyo salama. Anataka kujua tunafanyaje ili kuhakikisha sasa hizi dawa zinaweza kuwafikia Watanzania zikiwa salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuna taasisi yetu ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo kazi yake moja kwa moja ni kwa ajili ya kupima usalama wa dawa hizo; lakini kuwapa maelekezo ni namna gani wanaweza wakazipaki na kufikisha kwa wananchi zikiwa salama.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri ukweli kwamba kwa kipindi hiki cha *corona* kumekuwa na dawa mbalimbali na mambo mengi ambayo yanaleta shida. Hata hivyo, Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kama nilivyosema nyuma hapa, alishatoa shilingi bilioni 1.2; na leo nimetoka ofisini, imeenda tena shilingi bilioni 1.2, kwa maana ya shilingi bilioni 2.4 kwenye eneo hili la tiba asili kwa ajili ya kwenda kujenga uwezo kwa hawa watu wetu wazalishaji wa tiba ya asili, lakini kujengea taasisi zetu uwezo wa kuangalia hizo tiba asili zinazotolewa.

Je, zina hivyo vitu ambavyo vinaweza kutibu ugonjwa wenyewe unaosemekana? Pia itaenda kununua mashine za kupima na mambo mengine ya kusaidia utafiti na kupima usalama wa dawa hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imojiwekeza kwenye hilo. Majibu mengine kutokana na hii shilingi bilioni 1.2 ambayo imetoka leo, nayo tutawaletea majibu yake kwa sababu tunaenda kuangalia dawa nyingine 56 ambazo zilikuwa zinatumika wakati huu wa *corona*. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Humphrey Polepole, nimekuona.

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nchi za Uingereza, *Denmark, Sweden* na *Norway* zimeamua kuachana kabisa na masharti kichefuchefu dhidi ya ugonjwa wa Corona; na kuamua kuishi na ugonjwa wa Corona kama magonjwa mengine. Nini kauli ya Serikali kuhusu mwelekeo huu mpya Kimataifa? Ahsante. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali, ninachokiona ni kwamba *Sweden* na nchi zilizotajwa zimeamua kusimama kwenye msimamo wa Tanzania toka mwanzo. Kauli ya Tanzania ni moja tu kwamba

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sisi kama Tanzania tutaendelea kuhakikisha tunakuwa makini katika kufuata zile taratibu zote ambazo *WHO* wamezielekeza. Pia tutaendelea kufuata zile taratibu ambazo ni *local*, zinazotokana na watu wetu na nchi yetu ambazo tulishazifuata toka mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo tutaendelea kulinda mipaka yetu na kuwapima watu wanaoingia na wanaotoka kuhakikisha watu wetu ndani ni salama. Pia tuwahakikishie usalama wenzetu waliopo huko duniani wakija kwetu, nasi tukienda kwao ili tuweze kuitengeneza dunia salama kwa kufanya kazi kwa pamoja. Kwa sababu tukiwa wote salama, wote tutakuwa salama; mmoja asipokuwa salama, wote hatutakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini niseme, dunia siku moja itafika mahali ikubali mwelekeo wa Tanzania toka mwanzo ulikuwa ni sahihi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swalii fupi la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Madawa ya asilia ni kweli kama Watanzania tulikuwa tunayatumia siku za nyuma mpaka sasa. Ila kwa sasa kumekuwa na matangazo mengi sana kwenye vyombo vya habari, wakielezea kwamba wanatibu magonjwa sugu ya figo na magonjwa mengineyo ambayo ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina kauli gani ya kukataza matangazo hayo kwa kuwa hayana tafiti sahihi kwa wananchi na wamepoteza fedha nyingi sana kwa kununua dawa hizo na zisitibu chocote? Tunaomba kauli ya Serikali kwa watu kama hao. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo fupi.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nampongeza kwa swali lake zuri, kweli kwamba kumekuwa na matangazo hayo. Ila ukisikia Serikali na Taasisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na *TMDA* tena inapunguziwa kazi; na hata Wizara ya Afya kwa kutumia wadau wengine, kwa kweli lengo ni moja kusaidia hawa watu ambao ni wabunifu wetu wanaohangaika huku na huku kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali hawakatishwi tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhakikisha tunawadhibiti ili wasiweze kufanya kitu ambacho kinaweza kikapelekea madhara kwa watu; na ndiyo maana leo kwenye Wizara ya Afya kuna Kurugenzi ya Tiba Asili. Moja ya kazi yake, pamoja na *ku-facilitate* waweze kuzalisha hiki wanachokifiki, lakini ni kuwa-*control* kuhakikisha wanachokifanya mwisho wa siku hakiwi holela. Tutakwenda kuongeza nguvu hapo kama Mheshimiwa Mbunge alivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge ukienda Wilaya ya Meru, najua kuna watu wasiokuwa na uelewa walivuruga. Kuna Hospitali ilikuwa inaitwa *MOMELA* ilikuwa unapimwa vipimo vingine vyote vya kidaktari; unapimwa *Ultra-Sound*, unapimwa damu kama kawaida, lakini ukifika duka la dawa, unapata dawa za tiba za asili. Tunataka tufike hapo, kwamba ifike mahali tuna dawa ambazo tunajua zinatibu ugonjwa, tuna dawa za kisasa na tiba asili. Vilevile uweze kufuata taratibu zote za kuhakikisha usalama. Huko ndiko tunakoelekeea.

Mhesiiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachukua wazo lako na tunaongeza nguvu kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Mollel. Sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 112

**Tanzania kufungua Ubalozi mdogo Lubumbashi**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, lini Serikali inafungua Ubalozi Mdogo katika Jiji la Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hilli, baada ya Mheshimiwa Rais kuniamini kuendelea na nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini. Nami namwahidi kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imefungua Konseli Kuu katika Jiji la Lubumbashi, Jimbo la Haut Katanga, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Ofisi za Konseli Kuu hiyo kwa sasa zipo katika Kiwanja namba 1174 Avenue Ruwe, Quartier, Makutano, Jijini Lubumbashi. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu Kuwa Konseli Mkuu tayari amewasili Lubumbashi tarehe 7 Februari, 2022. Aidha watumishi wengine wanaendelea kuripoti katika Kituo hicho kwa awamu kulingana na mahitaji na taratibu za kidiplomasia, ahsante sana. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kuipongeza Sarikali kwamba imefuata usauri wa wabunge na ushari wa kamati na pia kama Mbunge ni jambo ambalo nimekuwa nikilisema toka mwaka 2016 na hatimae Ubalozi mdogo umefunguliwa katika Jiji la Lubumbashi, kwa hivyo itarahisisha sana utendaji wa kazi na biashara kati ya nchi yetu na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninaswali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa kwa upande wa Ziwa Tanganyika upande ule wa Kalema tayari Serikali yetu imeshaanza ujenzi wa bandari na inaendelea vizuri, lakini upande wa pili ambao kuna kama mwalo wa moba ambao sio bandari hasa haujawa katika mazingira ambao yanaweza ku-facilitate meli na hivyo sisi kufanya biashara.

Je, Serikali iko tayari kukutana na Serikali ya Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo kuititia tume ya pamoja na hivyo kushirikiana na kuangalia uwezekano wa kuona namna gani watashirikiana katika jambo zima la kujenga miundombinu, ili biashara kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo iweze kushamiri? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masharibi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHAFRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha barabara sehemu ya pili ya *DRC*, na kwa hali hiyo tayari saa hizi mazungumzo yameshaanza kati ya *DRC* na Tanzania na mazungumzo hayo yataendelezwa pia katika

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mkutano wa Pamoja wa Ushirikiano (*JPC*) ambao unatarajiwa kufanyika mwezi Mei na maandalizi wa mkutano huo unategemewa kuanza mwezi wa Aprili. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini uliza swali lako.

Na. 113

### **Kujenga Vituo vya Polisi Nkasi**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya Polisi katika maeneo ya mpakani wilaya ya Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mpakani mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Wilaya ya Nkasi kuna vituo vitano vya Polisi vya daraja C, ambavyo ni kituo cha Wampembe, kituo cha Namansi, Kipili, Kilando na Kabwe. Vituo hivi vinatoa huduma kwa wananchi kwa saa 24. Pia kuna tarajija kujengwa kituo kingine cha Polisi cha Daraja C katika eneo la Mpasa. Vituo vyote hivyo vinakidhi mahitaji ya kutoa huduma katika eneo la mpakani kando ya ziwa Tanganyika katika Wilaya ya Nkasi. Aidha, Serikali imepanga kuimarisha huduma kwenye vituo hivyo kwa kuvipatia usafiri stahiki hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. Nakushukuru.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, nimesikiliza majibu ya Serikali.

Mheshimiwa mwenyekiti, swali langu la msingi lilijikita mpakani tukiamini kwamba Wilaya ya Nkasi inapakana na nchi ya Congo na nchi ya Burundi, Kituo cha Polisi ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu anazungumzia Daraja C, Daraja C hilo ambalo unalizungumza katika kata 10 za mwambao unazungumzia kata tano, na hao askari kila kituo ni askari watano, hakuna pikipiki, hakuna gari, hakuna usafiri wa majini wala wa nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo hayo yamekuwa yanavamiwa mara kwa mara Serikali haioni haja kwa kuwa shida yetu sio majengo ya kituo cha polisi, tunataka vituo vya Polisi vyenye hadhi ya kupambana ikitokea uvamizi kwenye maeneo ya mpaka. Hamuoni haja sasa ya kujenga vituo hivyo kwenye maeneo ya mpakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika kata 10 za mwambao ambazo ndio zimekuwa zinatumiwa na hao maadui. Kata tano zina vituo; kata tano hazina.

Je, tunaomba kujua Serikali ina mpango gani wa haraka kwa kuwasaidia ulinzi wa wale watu kwa sababu sio ulinzi wa Nkasi ni ulinzi wa nchi nzima, ni lini mtajenga vituo hivyo vya polisi kwenye kata ya Korongwe, Nkinga na kata ya Kala ambayo wanavamiwa kila wakati? (*Makof!*)

**MWENYEKITI**, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa vituo vya Polisi hasa maeneo yaliyo katika mipaka, na sio uwepo tu wa Jeshi la Polisi lakini kuititia Wizara ya mambo ya ndani Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo hata vyombo vyengine, ili lengo na madhumuni mipaka yetu iendelee kubakia kuwepo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa nimwambie tu kwamba katika mipaka mingi ambayo nimeizunguka wakati ule hasa nilipokuwa nipo katika Wizara ya Mambo ya Nchi, ambao naamini na Waziri huyu ambae sasa hivi ndio Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwepo kule aliizunguka mipaka mingi. Maeneo mengi vituo vya Polisi vipo, lakini vituo hivi vipo *distance* kidogo na maeneo ya mipaka. baada ya kuona kwamba kwenye ile mipaka yenye Polisi na vyombo vyengine wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimawambi tu Mheshimiwa asiwe na wasiwasi, Serikali itaendelea kujenga vituo vya Polisi, ili lengo na madhumuni wananchi waweze kuishi kwa amani na uatalivu ikiwa mipakani, ikiwa ndani ya miji, ikiwa pembezoni, ikiwa popote lengo na madhumuni watanzania waishi kwa amani na utulivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inapeleka vitendea kazi ili lengo na madhumuni zile huduma za doria na mambo mengine yapatikane katika maeneo ya wananchi, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, nimemuona Mheshimiwa Fakharia Shomari, Mheshimiwa Agnes Hokororo na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, kwa kuwa kituo cha Polisi cha Ng'ambo ambacho kipo Wilaya ya Mjini Unguja kina tataizo kama vituo kituo cha Polisi kilichozungumzwa. Na tatizo letu hasa ni uzio. Kwa sababu kituo hicho kipo katikati ya barabara pande zote, pia kimezungukwa na mitaa hatari ya magari yanaweza yakaingia ndani yakagonga kituo, au wanyama

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanaofugwa mtaani wakaingia ndani na kituo hicho kipo tokea wakati wa ukolono, hakijaongezwa uzio, ulikuwa uzio wa senyenge umezungushwa na majani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuzungumza kwenye baraza hili tukufu kwamba wakati wowote utawekwa uzio toka bajeti tulioimaliza na tunaenda kwenye bajeti mpya hali hiyo hajatengamaa. Je, uzio huo utawekwa lini ili watu wa pale wapate amani? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya uzio huo wa kituo cha Polisi Mjini jiji la Zanzibar.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru, naomba sasa kujibu swala la nyongeza la Mheshimiwa bi Fakharia Mbunge wa viti maalum kutoka Mkoa wa Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hichi ni moja ya mionganoni mwa vituo vyा Polisi ambavyo nimevifanyia ziara, na moja ya mionganoni mwa vitu ambavyo tayari vimeshafanyika ni tathmini kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa kituo kile, kalini wakati huo tunafanya tathmini tunaangali namna kwa sababu kile kituo ukikitazama unakuta kwamba kila pembe kimezungukwa na barabara. Kwa hiyo, *the way* utakavyojenga uzio kuna hatari ukaja ukajikuta kwamba unaila ile barabara. Sasa kula chote lakini usiile barabara kwasababu unaweza ukatengeneza mazingira mengine ambayo yanaweza kusababisha ajali za barabarani ambazo hazina sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba tathmini imeshafanyika na sasa tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile, Mheshimiwa wewe kwa niaba ya wananchi muwe na subra kidogo mtusubirie na sisi tumo mbioni kuhakikisha kwamba uzio unajengwa katika kituo kile. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Agnes Hokororo.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya za Mkoa wa Mtwara takriban zote ziko mpakani. Je, Serikali iampango gani wa kujenga kituo cha Polisi katika Wilaya Masasi katika kata za mpakani kabisa za Mnadhira, Mchauru, Sindano na Chikoropola ambapo kwa sasa kunaonekana kuna vuguvugu za vurugu katii ya wakulima na wafugaji? (*makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Agnes Hokororo Mbunge wa Viti maalum kutoka Mtwara kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha ile bajeti yetu ya 2021/2022 moja ya mionganini mwa mambo ambayo tunakwenda kuyafanya katika bajeti ile ni kujenga vituo vingi vyaa Polisi na hasa yale maeneo ambayo yanautauta kiulinzi, maeneo ya mipakani na maeneo mengi ambayo tunahisi yana sababu za zaidi asilimia moja kuwepo kwa vituo vyaa Polisi kwa ajili ya kulinda Maisha ya wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa kwamba awe na subra Serikali itahakikisha kwamba inajenga vituo vyaa Polisi maeneo mengi lakini hasa katika maeneo ambayo wameyataja ili liengi na madhumuni wananchi waweze kuishi katika Maisha ya ulinzi na usalama zaidi, Nashukuru.

**MWEYEKITI:** Nimekutaja Mheshimiwa Rashid Shangazi na mwisho nitampa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Lushoto ina tarafa 8 lakini tuna vituo 5 tu vyaa Polisi, lakini katika Kata ya Lukozi na Lunguza ambazo

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ni miji midogo na hii Lunguza ipo karibu kabisa na mpaka wa nchi jirani ya Kenya, wananchi wale wametenda maeneo na wanataka kulikabizi Jeshi la Polisi ili kwa kushirikiana nao tuweze kujenga vituo vya Polisi. Je, Waziri yuko tayari kumuagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga aje akabaini yale amaeneo na shughuli za ujenzi zianze? (*Makofii*)

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashidi Shangazi Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mionganini mwa azma kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaishi kwa amani na utulivu katika maeneo yao hasa baada ya kupata ushirikiano kutoka kwa Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama, na zaidi pale wananchi wanapoamua kwamba wao wenyeewe wameshajitolea wako tayari kujenga kituo cha Polisi, sisi kama Serikali kama Wizara kama Jeshi la Polisi tupo tayari kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nichukue fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nimuagize *RPC* Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na OCDs wake na baadhi ya mastafu wake, wahakikishe kwamba wanakwenda kutoa ushirikiano kwa wananchi ili lengo namadhumuni kituo hiki cha Polisi kijengwe ili wananchi waweeze kupata huduma ya ulinzi na usalama. Nakushukuru.

**MWEYEKITI:** Ahsante nilikuwa nimemalizia na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Wananchi wa mtaa wa Mavurunza Kata ya Kimara na mtaa Kibo kata ua Ubungo, tumechangishana tumejenga vituo 2 vya Polisi lakini hatujamalizia kwa sababu nguvu zimeisha. Je, Serikali

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inaweza ikaahidi kuingiza katika bajeti ijayo ili vituo hivi vikamilike? Ahsante sana.

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo Mbunge wa Jimbo la Ubungo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena azma ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wanajengewa vituo vyta Polisi ili lengo na madhumuni waweze kupata pahala pa kupeleka matatizo yao, lakini pia waweze kulindwa wao na mali zao. Nimwambie tu kwamba tupo tayari kuhakikisha kwamba tunaingiza fungu maalum kwa ajili ya ujenzi wa hicho kituo ili lengo na madhumuni wananchi wa Ubungo na maeneo ya Jirani waweze kunufauika na kituo hicho. Nakushukuru sana.

**MWEYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa nina vimemo 10 vimebaki vyta maswali kwenye Wizara yako, naomba wabunge tafadhalii mumwendee Waziri mkamuombe awape majibu ya maswali hayo, naamini vingi vilikuwa kwenye vituo sijui Mheshimiwa Naibu Waziri mmekwama wapi kwenye vituo vyta Polisi, nafikiri labda muangalie kwa vizuruzi zaidi.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Technolojia, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa viti Maalum aulize swalii lake.

Na. 115

### **Ujenzi wa Chuo cha VETA – Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Meatu?

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWEYEKITI:** Majibu ya swali hili Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Njika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kujenga Vyuo vya VETA katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini. Kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya 25 na Mikoa 4 ukiwemo Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Meatu na maeneo mengine, wananchi wa Meatu wanashauriwa kutumia Vyuo vya VETA na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo jirani kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, napenda kushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu yenye matumaini. Lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Je, ni lini Serikali sasa itajenga chuo cha VETA katika Wilaya ya Meatu na Wilaya ya Busega? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, naomba sasa kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Minza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kwamba ujenzi wa vyuo hivi unalingana sawa au unaendana sawa na upatikanaji wa bajeti na upatikanaji wa fedha. Lakini naomba nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu, hatuishii tu kwenye ujenzi wa vyuo hivi tunakwenda mbali zaidi kwa sababu tukishajenga ni lazima tuweze kuangania namna gani ya upatikanaji wa vifaa lakini vile vile upatikanaji wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imejikita katika umaliziaji wa vyuo hivi 25 na baadae sasa tutakwenda kwenye mkakati wa kuweka bajeti kwa ajili ya kufikia Wilaya hili ya Meatu, Busega na Wilaya nyingine nchini zillizobaki kwa sababu Wilaya bado ziko nyingi, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, vyuo hivi vya VETA ni muhimu sana kwa sababu husaidia katika kukuza ujuzi lakin pia vinaubua ubunifu, na kwa kufanya hivi husaidia vijana aidha kujiajiri au kupata ajira kwa haraka zaidi, asilimia kubwa ya Wilaya za Mkoa wa Mara hazina vyuo vya VETA. Ningependa kujua ni lini Serikali itajenga vyuo vya VETA walau kwa Wilaya ya Tarime, Rorrya na Bunda? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swalii hili la nyongeza.

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika Mkoa wa Mara anaozungumza Mheshimiwa Mbunge kwenye maeneo hayo katika Wilaya hizo alizozitaja bado hatujaweza kuzifikia, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

awamu ijayo maeneo ambayo yatapewa kipaumbele ni yale ambayo hatujayafikia hivi sasa kwa karibu.

Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi katika mgawo unaokuja tutahakikisha kwamba maeneo haya aliyoyataja yanapewa kipaumbele na kuanza ujenzi mara moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Genzabuke nimewaona.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi na Serikali ya Kijiji ya Mwambiti iliyopo Jimbo la Meatu katika Halmashauri ya Meatu imeridhia kutoa eneo lake la ekari mia moja bila fidia kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha VETA; Je, Serikali ipo tayari kupokea hati hiyo ya kieneo ili kukabiliana na vijana wanaokosa fusa zinazotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Komanya kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa hatua hiyo nzuri walioichukua ya kutafuta eneo na tayari wameshaandaa mpaka Hati na Wizara tuko tayari kupokea hati hiyo. Kwa sababu wameshapiga hatua moja mbele kwa kupata eneo na tayari wameshatafuta Hati tunaamini katika mchakato unaokuja pindi Serikali itakapopata fedha ina maana atakuwepo kwenye mgawo wa awamu hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mafupi. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibondo ni kati ya Wilaya kongwe nchini, Wilaya hiyo haina Chuo cha VETA. Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Kibondo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa swali fupi la nyongeza la Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Kibondo bado hatujaweza kuifikia kwenye Vyuo vyetu vya VETA, ingawa tuna Chuo kikubwa kilichojengwa Kasulu ambapo ni karibu kabisa na wenzetu wa Kibondo. Kwa sasa tunawashauri wananchi wetu wa Kibondo waweze kupata huduma hii katika chuo chetu kikubwa ambacho tumejenga katika Wilaya ya Kasulu wakati Serikali inaendelea na mchakato wake wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi katika eneo hili la Kibondo. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi niliruka la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aliulize.

Na. 114

**Utatuzi wa mgogoro wa bomoa bomoa katika  
eneo la Kimara - Kibamba**

**MHE ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutatua mgogoro wa bomoabomoa wa nyumba za wananchi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

zilizokuwa pembezoni mwa Barabara ya Morogoro kutoka Kimara hadi Kibamba ulioanza mwaka 2017?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2017/2018, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*), Mkoa wa Dar es Salaam iliondoshwa nyumba na mali za watu zilizokuwa zimejengwa kinyume cha sheria ndani ya eneo la hifadhi ya Barabara ya Morogoro kuanzia Kimara hadi Kibamba ikiwa ni maandalizi ya kupanua barabara hiyo toka njia mbili hadi njia nane ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 pamoja na Kanuni zake za mwaka 1955 na marekebisho yake Na. 13 ya mwaka 2009, imeanishwa kwamba upana wa hifadhi ya barabara hiyo kuanzia Kimara *Stop Over* hadi Kibaha (*TAMCO*) ni mita 121 kutoka katikati ya barabara kila upande. Hivyo, nyumba na mali zote zilizokuwa ndani ya eneo hili walikuwa wako ndani ya eneo la hifadhi ya barabara kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwaondoa wananchi waliokuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ili kupisha utekelezaji wa mradi huu lilifanyika kwa kufuata Sheria ya Barabara na hadi sasa Serikali haina mgogoro wowote na wananchi walioondolewa ili kupisha upanuzi wa barabara hiyo.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kutatokea mgogoro kati ya wananchi wa eneo la Kimara hadi Kibamba kuhusiana na bomoa bomoa ya nyumba zilizojengwa ndani ya hifadhi ya barabara ya Morogoro kinyume na sheria, mgogoro huo utatatuliwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini ukweli mwenye dhamana ya kutafsiri sheria ni Mahakama na kumekuwepo na kesi ya ardhi chini ya Jaji Bongoyo ya mwaka 2005 ikahukumiwa mwaka 2013. Kesi ya Prochesta Lyimo na wenzake 72 dhidi ya AG na Wizara ya Ujenzi. Katika dhamana hiyo wadai walihalishwa kwamba eneo ni la kwao na kama Serikali inalihitaji inatakiwa illipe fidia. Swali langu la kwanza, je, ni lini Serikali itatekeleza hukumu hii ya Mahakama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, Sheria ya Barabara ya mwaka 1932, Kanuni ya Mwaka 1955 na marekebisho Na. 13 mwaka 2009 inakinzana sana na Sheria nyingine za Mipangomiji na Sheria ya Vijiji ya mwaka 1999 ambayo ilifuta mikataba mingine na sheria nyingine zote zilizotangulia kwa kuweza kuwamilikisha watu ardhi ikiwa ilienda sambamba na zoezi la Operesheni Vijiji ya Mwaka 1974 na 1975 iliyoleta watu pembezoni mwa barabara kubwa na kuwapa miundombinu ya maji na elimu na kadhalika. Je, ni ipi kauli ya Serikali katika mchangamano huu au mchanganyiko wa sheria hizi ya barabara ya mwaka 1932 na hizi nyingine za ardhi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kiamba kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, kwanza nimshukuru na kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akilifuatilia suala hili kila wakati ili kuhakikisha tu wananchi wake hawa wanapata hicho ambacho anawapigania. Naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria iliyopo. Moja ya wajibu wa Serikali ni kulinda wananchi pamoja na mali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi aliyoisema ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo kwa Wakili Mkuu wa Serikali ambae yupo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatua waliyochukua wananchi hawa kupeleka suala hili kwenye vyombo vya kisheria, naomba nimhakikishie kwamba sheria itakapotamka mara ya mwisho nadhani haki itatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu sheria kukinzana naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tunatumia Sheria yetu ya Barabara, lakini suala la kukinzana kwa sheria nadhani Serikali imelichukua na itaenda kuangalia sheria mbalimbali zinavyokinzana ili ziweze kusomeka na kueleweka kwa pamoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Saashisha, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro wa muda mrefu sana kati ya wananchi wa Kata ya *KIA* kwa maana ya vijiji saba na Kata ya Rundugai na kule Arumeru dhidi ya Uwanja wa Ndege wa *KIA*. Mgogoro huu Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba ataumaliza, lakini humu ndani nimekuwa nikiahidiwa na Serikali kila mara kwamba tutaenda kuumaliza. Hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Diwani wa Kata ya *KIA*

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

muda si mrefu amenipigia simu akiniambia kwamba wameanza kuweka alama ya X nyumba za watu bila kushirikisha wananchi na viongozi wa wananchi. Naomba majibu ya Serikali yaliyo thabiti, je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huu? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na mgogoro kati ya wananchi na Serikali kwenye uwanja wa KIA. Mbunge amekuwa akiliifuatilia mara kwa mara, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ameshaunda timu ambayo imekwenda kufanya tathmini na kufanya utafiti na mara watakapoleta taarifa tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Mbunge atapewa hiyo taarifa na tuna uhakika baadaye tutakwenda kwenye eneo la tukio lenyewe na yeye pamoja na wananchi ili suala hili liweze kufika mwisho. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Bonnah Kamoli utamalizia.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Nanganga, Nangoo, Ndanda, Mwenda, Chikundi, Chigugu, Chikukwe, Chikunja pamoja na Lukuledi ambazo zinapitisha na barabara kuu inayokwenda Nachingwea kutokea Masasi au barabara kuu inayotoka Mingoyo kulekeea Mbamba Bay na Songea. Kwa muda mrefu sasa zaidi ya miaka Kumi hadi Ishirini nyumba za watu pamoja na mali zao zimewekewa alama

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

za X. Ziko alama za X za kijani lakini pia zipo alama za X nyekundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wameshindwa kufanya shughuli zao zozote kwa sababu hawaelewi tafsiri ya alama hizi. Nataka kauli ya Serikali itueleweshe ni nini maana ya kuweka alama (X) nyekundu au alama (X) ya kijani kwenye maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi ya swali hilo fupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alama hizi zinaonesha kwamba wananchi wamejenga kwenye hifadhi ya barabara ama barabara itapita kwenye maeneo hayo. Wapo ambao barabara imewafuata kijani na wale ambao watatakiwa kufidiwa walikuwepo barabara wamewekewa alama ya (X) lakini ni kwamba hawa wote wataondolewa kwa utaratibu na kwa mujibu wa sheria. Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah swali la mwisho kwa Wizara hii.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Kata ya Kipawa ambao walipisha *Airport terminal three* tangu mwaka 1997 na sehemu hiyo mpaka sasa hivi shughuli za maendeleo zimesimama. Je, ni lini Serikali itawalipa hawa wananchi fidia? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Ia Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi alioswasema wa Kipawa *Airport* ambao walipisha ujenzi wa uwanja wa ndege, suala hili nimwombe Mheshimiwa Mbunge aweze kutuletea maelezo sahihi kwa sababu ambao walilipwa na hawa ambao hawakulipwa ili tuweze kujua ni wapi ambao hasa anawasimamia ili tuweze kuwa na majibu sahihi kwa upande wa Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah, nafikiri umemsikia Mheshimiwa Waziri, basi utatoa ushirikiano ili muweze kujua wale ambao bado.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda siyo Rafiki hatutakuwa na maswali ya nyongeza isipokuwa swali la muuliza swali. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Bonaphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu sasa aulize swali lake.

Na. 116

### **Hitaji la Mbegu Bora za Alizeti**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa utoaji wa mbegu bora za alizeti ili kuongeza uzalishaji wenye tija kwa Wakulima katika Wilaya ya Kishapu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni mionganini mwa Halmashauri zenyefursa ya uzalishaji wa zao la alizeti nchini. Kutokana na umuhimu wa nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula, Serikali kwa kushirikiana na sekte binafsi inatekeleza Kampeni ya Kitaifa yenye lengo la kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kwa kuimarisha utafiti, kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeongeza bajeti ya Taasisi yetu ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) kutoka Shilingi bilioni 7.5 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Shilingi bilioni 11.6 kwa mwaka 2021/2022 na bajeti ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*) kutoka Shilingi bilioni 5.42 kutoka 2020/2021 hadi kufikia Shilingi bilioni 10.8 kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mikakati hiyo upatikanaji wa mbegu bora za alizeti umeongezeka kutoka tani 587 mwaka 2021 hadi tani 2,124 mwezi Januari, 2022. Kati ya hizo *ASA* imesambaza tani 1,600 kwa bei ya ruzuku ya Shilingi 3,500 kwa kilo, ambapo tani 48 za mbegu bora za alizeti zimesambazwa katika Mkoa wa Shinyanga na usambazaji wa mbegu unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na mahitaji. Aidha, katika msimu wa 2022/2023 Serikali inalenga kuzalisha na kusambaza tani 5,000 za mbegu bora za alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako tukufu, naomba kutoa wito kwa viongozi katika Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kuwa mbegu zinazosambazwa kwa wakulima zinatumika kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kutokana na suala la zao muhimu la alizeti katika nchi yetu.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tani ambazo zimetajwa hapa tani 48 zilizosambazwa katika Mkao wa Shinyanga na tani hizi za mbegu hazijaainishwa katika Wilaya ya Kishapu ni kiasi gani cha tani za mbegu ambazo zimesambazwa katika Wilaya ya Kishapu peke yake. Pengine katika maswali yangu ya nyongeza ni kwamba ASA ambaye ni Wakala aliye kuwa anashughulikia usambazaji wa mbegu katika Mkao wa Shinyanga Wilaya ya Kishapu peke yake ni Wilaya ambayo ilibidi wakulima wapate huduma kutoka Kishapu kwenda Manispaa ya Mjini Shinyanga Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza; je, Serikali haioni haja ya kusogea huduma hii ili ASA aweze kusambaza ama kutoa huduma katika Wilaya *per se?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; lipo eneo katika Wilaya yetu ya Kishapu ambalo linamillkiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ambayo ni zaidi ya ekari mia tatu. Je, Serikali ipo tayari kuja kuliona eneo hilo na ikiwezekana kuanzisha kilimo maalum cha zao la pamba kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu hizi za kisasa ili tuongeze tija na upatikanaji wa karibu zaidi kwa wananchi wa Kishapu kwa ajili la suala zima la mbegu za alizeti?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa eneo la ekari 300 Serikali tupo tayari kushirikiana na Halmashauri husika ili tuweze kuona ni namna gani hilo eneo linaweza kutumika na kwa maslahi ya wananchi wa Kishapu, hivyo, milango ya Wizara ya Kilimo iko wazi karibu wewe na Mkurugenzi wako tuweze kujadiliana ni namna gani tunaweza kulitumia hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusogea huduma za ASA katika Halmashauri ya Kishapu. Ninataka tu nimuombe

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mbunge na niwaombe Wabunge wote, siyo rahisi kuweka ofisi ya ASA katika kila Wilaya kwa wakati mmoja, gharama za uendeshaji zitakuwa kubwa na hazina *economic value*. Kama Halmashauri husika ina mahitaji *specific* ya mbegu, tupo tayari watuletee mahitaji yao, tuy-*aggregate* pamoja na tuwapelee katika ngazi ya Halmashauri ama Mkoa halafu wao wenyewe waweze kusambaza katika maeneo yao na wakulima wao kama tulivyofanya katika Mkoa wa Singida na Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawa-*encourage* Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu, mahitaji ya mbegu za alizeti za Halmashauri yake wayalete kimaandishi ili sisi tuwapelekee katika ofisi zao za Halmashauri badala ya kufungua ofisi katika eneo hilo linalohusika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunamalizia na Wizara hiyo ya Kilimo na sasa ni swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 117

### **Kupanda kwa bei ya mbolea nchini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha bei ya mbolea inashuka hadi kufikia kiwango cha Wakulima kumudu kuinunua ili kuiepusha nchi yetu kukumbwa na janga la njaa.?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

### **WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye eneo (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakiri kwamba bei ya mbolea katika Soko la Dunia na hapa nchini imepanda kwa msimu wa mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2020/2021. Kupanda huko kwa bei hakutokani na Serikali au wafanyabiashara wa ndani kupandisha bei, bali kumetokana na kupanda kwenye Soko la Dunia na wakulima wote duniani wameathirika na upandaji huo uliotokana na athari za UVIKO. Mfano, hadi kufikia mwezi Januari, 2022 bei ya *Urea* ni Dola za Kimarekani 700 kwa tani ikilinganishwa na Dola za 350 kwa msimu wa 21, sawa na ongezeko la asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za kupanda kwa bei za mbolea nchini, Serikali inachukua hatua za muda mfupi na muda mrefu. Hatua za muda mfupi zilizochukuliwa mpaka sasa ni pamoja na kununua mazao ya nafaka kwa bei ya juu kuliko bei ya soko ambapo mahindi yalinunuliwa kwa bei ya shilingi 500 badala ya 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhakikisha kwamba bandari zetu zinatoa kipaumbele cha kushusha mbolea ili kupunguza tozo za bandarini, ununuzi wa mbolea kwa mfumo wa (*BPS*) katika baadhi ya mazao mfano Tumbaku. Matumizi ya reli kusafirisha mbolea katika maeneo ambapo reli inapita. Matumizi ya mbolea mbadala kama *NPS* na *NPS-Zinc* na kuruhusu ushindani kwenye uagizaji wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mrefu zilizochukuliwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya mbolea. Kutokana na uhamasishaji huo, Kampuni ya *ltracom Fertilizers* kutoka Burundi inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha mbolea Mkoani Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea na tani 300,000 za chokaa kwa mwaka. Wawekezaji wengi zaidi wanaendelea kujitokeza kutoka nchi mbalimbali kama vile Misri na Saudi Arabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekutana na uongozi wa kiwanda cha mbolea cha Minjingu kujadili namna kiwanda hicho kinavyotakiwa kuzalisha mbolea

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kulingana na mahitaji ya udongo na kuongeza uzalishaji wa mbolea kutoka tani 30,000 hadi kufika 100,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua umuhimu wa mbolea katika uzalishaji wa mazao ya chakula ili kuihakikishia nchi Usalama wa Chakula. Kutokana na tathmini iliyofanyika ambayo iliangalia changamoto hii pamoja na utabiri wa mvua, ulioonesha hatutapa mvua nyingi kwa miaka miwili iliyopita, bado maoteo ya uzalishaji yanaonesha nchi itaweza kujitosheleza katika chakula. Mpaka sasa maeneo mengi ya nchi yanaendelea kupata mvua nzuri. Matumizi ya mbolea yapo kwenye asilimia 50 ya kawaida ya mazao ya shambani. Kwa hali hiyo, Wizara ya Kilimo inapenda kuwashakikishia wananchi kwamba, nchi haitakumbwa na janga la njaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MAONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sasa naomba niulize swali la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, mpaka sasa hivi Serikali bado hajawa na majibu sahihi kwa wakati sahihi yanayohusiana na suala la mbolea, ambayo kimsimgi imepanda bei katika maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania, hususan Mkoa wa Ruvuma: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku kwenye mbolea ili wananchi wawezesha kupata mbolea kwa bei nafuu?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mkoa wa Ruvuma ndiyo benki ya chakula nchini Tanzania; na bila shaka yoyote Mkoa wa Ruvuma umeongoza takribani miaka minne mfululizo kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha uzalishaji wa mbolea katika nyanda za juu Kusini, hususan Mkoa wa Ruvuma ikiwa ni pamoja na kuweka benki ya kilimo katika Mkoa wa Ruvuma? (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu ya maswali hayo mawili.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna njia ya mkato kwenye sekta ya kilimo zaidi ya *ku-design modal* ya kutoa ruzuku. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, ilikuwa ni vigumu kwa mwaka huu kutengeneza mfumo wa ruzuku kwenye bei ya mbolea kwa sababu, historia inaonesha mifumo ya awali iliharibu na mifumo ile ilisababisha fedha nyingi za umma kupotea na wakulima hawaku-*benefit* na mfumo wa ruzuku uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako Tukufu, maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, Wizara ya Kilimo tutengeneze *mechanism* ambayo itatuletea mfumo sahihi wa ruzuku kwa pembejeo. Tutaleta mfumo wa *stabilization fund* na katika bajeti ya mwaka kesho mtaiona na tutaiwekea mkakati ili ruzuku iweze kwenda moja kwa moja kuwafaidisha wakulima. Hiyo ndiyo njia pekee itakayoweza kuwalinda wakulima wetu wadogo na huo ndiyo mwelekeo wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tungetoa ruzuku leo, tusingekuwa na *framework* ambayo ingeweza kumfaidisha mkulima, bali kwenda kupoteza fedha za umma na hiyo isingekuwa haki kwa nchi. Kwa hiyo, kuanzia mwaka ujao wa fedha 2022/2023 tunaleta mfumo wa *Stabilization Fund* itakayotumika kwenye pembejeo na pale ambapo mazao ya wakulima yanaanguka kwa sababu zilizo nje ya uwezo wetu, ili kuwalinda wakulima wetu wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga kiwanda; uwekezaji wa kiwanda unaangalia *variables*nyingi sana, siyo tu kwa sababu eneo fulani linazalisha mazao mengi, upatikanaji wa rasilimali kwa maana ya *raw materials* na zipo

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

sababu nyingine. Siwezi kutoa ahadi ndani ya Bunge lako kwamba Serikali itaenda kujenga kiwanda katika Mkao wa Ruvuma, lakini kama atatokea mwekezaji anataka kujenga kiwanda Mkao wa Ruvuma, sisi kama Serikali tutamsaidia na kum-support ili aweze kujenga. Tunachokifanya, tunamsaidia mwekezaji wa *intracom* aliye hapa Dodoma ili aweze kuzalisha mbolea kutokana na ikolojia ya nchi yetu na yasitokee makosa yaliyotokea huko nyuma kwenye kiwanda cha Minjingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo tunayafanya na tunawapa *support*. Kwa hiyo, kuna kiwanda hiki cha hapa Dodoma; na vilevile tumewasaidia Minjingu kwa ajili ya kupata fedha waweze ku-expand kiwanda chao cha Minjingu ili kiweze kufikia zaidi ya tani 100,000 tuweze kukidhi mahitaji ya nchi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, kwa majibu hayo. Wizara yetu ya mwisho kwa siku ya leo ni Mifugo na Uvuvi na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela.

Na. 118

### **Kujenga Mialo Katika Forodha za Nankanga na Ilanga – Ziwa Rukwa**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mialo katika Forodha za Nankanga na Ilanga zilizopo ndani ya Ziwa Rukwa ili kurahisisha shughuli za Uvuvi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

### **NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkakati wa Serikali ni kuhakikisha inajenga na kuboresha mialo katika maeneo mbalimbali nchini yanayojishughulisha na shughuli za uvuvi ikiwemo maeneo yanayozunguka Ziwa Rukwa kama vile forodha za Nankanga na Forodha ya Ilanga. Aidha, utekelezaji wa mkakati huu unategemea upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mafupi namna hiyo. Mheshimiwa Deus Clement, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza. Pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kujenga mialo kwenye Forodha ya Nankanga na Ilanga, Iakini kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu ndani ya Ziwa Rukwa kati ya Hifadhi ya *Uwanda Game Reserve* na ile Rukwa Lukwati.

Je, Serikali mna mpango gani wa kuweka alama za kudumu zitakazowafanya wavuvi wafanye shughuli zao za uvuvi bila kubughudhiwa na askari wa wanyamapori wa *Uwanda Game Reserve* pamoja na wale wa Rukwa Lukwati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili: Ziwa Rukwa ni moja kati ya maziwa ambayo yana mamba wengi hapa Tanzania na imesababisha wavuvi wengi kupoteza maisha. Nataka kujua, ili kuwalinda wavuvi wetu ndani ya Ziwa Rukwa, Serikali mmejipangaje kuleta vyombo vyao uokozi ndani ya Ziwa Rukwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Deus Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza anataka mpango wetu juu ya kuweka maboya. Hili tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ndiyo inasimamia hizi *game reserves* kwa ajili ya kuweza kuona namna tunavyoweza kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, halikadhalika, lile la mamba wanaokula wavuvi; kwa kuwa mamba pia ni rasilimali na inasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba nirejee tena katika jibu la mwanzo kwamba tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na tutafanya mukutano wa pamoja ili tuweze kutafuta suluhu ya jambo hili, ikiwemo kupata vifaa vitakavyowawezesha wavuvi hawa kuweza kuokolewa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali letu la mwisho kwa siku ya leo ni la Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 119

### **Kurejesha Shamba la Kupumzisha Mifugo la Kinyangili – Wilayani Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italirejesha Shamba la kupumzishia Mifugo la Kinyangiri kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, Mbunge wa Iramba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa maeneo haya katika biashara ya mifugo na mazao yake, hususan kipindi hiki ambapo soko la nyama limezidi kuongezeka nje ya nchi, Serikali inakusudia kuendelea kuboresha maeneo yake yote ya mifugo ikiwa ni pamoja na eneo la Kinyangili ili kusudi biashara ya mifugo na biashara ya nyama nchini iweze kushamiri kwa kuzingatia viwango vyote vinavyotakiwa katika Soko la Kitaifa na Kimataifa. Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Mttinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpaka sasa Halmashauri ya Mkalama ndio wanaotunza shamba hili; na kwa kuwa, hatuna ugomvi na Wizara na tunajali sana maslahi ya umma: Je, Wizara ipo tayari sasa kukaa meza moja na Halmashauri ya Mkalama ili tuweze kukaa na kujadili matumizi bora zaidi ya eneo hili kuliko kuendelea kuwa shambaporii kama ambavyo lilitivo sasa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Isack Francis Mttinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, milango ya Wizara iko wazi. Tunawakaribisha viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, wakiongozwa na Mheshimiwa Mbunge makini, wawewe kuja tukae mezani kuzungumza na kuona hatima

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

njema ya eneo lile na hususan katika kuboresha mifugo yetu na huduma nyingine. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Huu ndiyo mwisho wa maswali yetu kwa siku ya leo. Yafuatayo sasa ni matangazo.

Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge kuwa, wataalam wa afya kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa wapo kwenye viwanja vya Bunge, eneo la nyuma ya Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya Kliniki Maalum ya Uchunguzi wa Afya ya Moyo, Macho, Kinywa na Meno, Masikio, Pua na Koo, pamoja na huduma za ushauri wa afya. Huduma hii itatolewa kuanzia leo tarehe 14 hadi 18 Februari, 2022. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kupata huduma hizo.

Matangazo mengine ni wageni waliopo Bungeni mchana huu. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wa kwanza ni wageni 22 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Mbunge na Waziri wa Madini, ambao ni Makatibu wa CCM wa Kata 17 wakiongozwa na Ndugu Odilia Batimayo, katibu wa CCM Wilaya Bukombe kutoka Mkoani Geita. Karibuni sana wageni wetu na wa Mheshimiwa Waziri, katika Bunge letu. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni Ndugu Mikidadi Alli Mpinda - mtoto wake, Ndugu Salumu S. Mboggo - Mwanahabari na Ndugu Tukupilika T. Mbiga - Wifi yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu na wa Mheshimiwa Mwakagenda. (*Makof*)

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge, ambao ni wafanyakazi wa Azam TV; Ndugu Fatma Stambuli na Ndugu Betty Omala, kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana katika Bunge letu. (*Makof*)

Wageni wengine 15 ni wa Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge, ambao ni viongozi wa timu nne kutoka

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kata ya Magomeni, zilizoingia nusu fainali ya *Tarimba Sodo Cup* (Mpira wa Chandimu) wakiongozwa na Katibu wa Mbunge, Ndugu Salumu Madenge kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Jerry Slaa, Mbunge, ambao ni Wapaka Rangi za Kucha Maarufu, kutoka Jimboni Ukonga, Jijini Dar es Salaam; Ndugu Timotheo Mgara na Grayson Rayson. Karibuni sana vijana wetu. (*Makofii*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Cecil Mwambe, ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Masasi, wakiongozwa na Mheshimiwa Antony Chihako, Diwani wa Kata ya Msikisina na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kutoka Mkoa wa Mtwara. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Mtwara. (*Makofii*)

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, ambao ni wanafunzi kutoka Jimboni Mbagala, Ndugu Natasha Swalleh Mohamed, Ndugu Idrisa Jumanne Mwanuh, Ndugu Khaimin Ally Chamalys, wakiongozwa na mtoto wake Ndugu Kheri Chaurembo, kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Ndugu zetu kutoka Dar es Salaam. (*Makofii*)

Wageni wengine ni wageni 17 wa Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge, ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Igulula, Mkoani Tabora, wakiongozwa na Ndugu Alicia Mwami. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofii*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 144 na walimu 13 kutoka *Camel Pre-Primary School* ya Jijini Arusha, wakiongozwa na Mwalimu wao Othman Yusufu. Karibuni sana wanafunzi wetu kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni pamoja na walimu wenu. Natumaini mmejifunza vizuri. (*Makofii*)

Katibu, tuendelee.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria  
kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 na Taarifa ya  
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za  
Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021**

**MWENYEKITI:** Hoja za Kamati. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Karibu sana Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI  
YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa Kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba kwanza nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa na Bunge lako Tukufu kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi wa asilimia 100 wa kura zote alizopigiwa unaonesha ni kwa kiwango gani Wabunge wa Bunge hili wana imani kubwa naye katika kutekeleza majukumu ya kuwa Mkuu wa Mhimili wa Bunge.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, kwa kuchaguliwa kwa asilimia 98.33 kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sana Wajumbe wa Kamati kwa kuniamini, kuniunga mkono na kunichagua kwa kura zote kuwa kiongozi wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaahidi na kwa neema za Mwenyezi Mungu nitatekeleza jukumu hili kwa weledi na uaminifu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii kabla yangu Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Waziri wa Sanaa na Michezo na wewe mwenyewe Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na uliye kaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati hii tangu Aprili 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wajumbe wa kamati hii kwa uongozi bora, umoja, ushirikiano na mshikamano mkubwa. Umoja ushirikiano na mshikamano huu umeiwezesha kamati yetu kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Katiba na sheria imepewa majukumu ya kusimamia Wizara nne kama zifuatano: Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha Februari 2021 hadi Februari 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, imetekeleza shughuli zifuatazo:

(a) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(b) Kuchambua Miswada ya Sheria iliyofanyiwa marekebisho ya sheria mbalimbali;

(c) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara na Taasisi zake;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(d) Kupokea na kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 za Wizara na Taasisi zake kwa kipindi kinachoishia Disemba 2021;

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuainisha majukumu ya kamati na shughuli zilizotekelzwa na kamati kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022 naomba sasa nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo kamati iliyabaini wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yatakayotolewa katika taarifa hii ni yale ambayo kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipaumbele ili kuiwezesha kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye matokeo ya uchambuzi wa kamati na nianze na uchambuzi wa yanayotokana na taarifa za utendaji wa taasisi za Serikali:

(a) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mpango wa kupanua *program* ya kukuza ujuzi nchini kwa lengo la kuwafikia vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kamati kuhusu taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu mbele ya Kamati iliyowasilishwa mbele ya kamati tarehe 27 Oktoba 2021 ilibainisha kuwa mpango wa kupanua *program* ya kukuza ujuzi nchini kwa lengo la kuwafikia vijana wengi zaidi unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:

(i) Kuibuka kwa uhitaji mkubwa wa mafunzo ya kukuza ujuzi kutoka kwa vijana ambao hawakupata fursa ya kuendelea na elimu ya juu, kutokana na hali duni za familia zao hususan familia za vijijini.

(ii) Vijana wengi kushindwa kumudu għarama za kuhudhuria mafunzo kwa sababu ya umbali kutoka

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanakoishi vijijini, kuja kwenye Makao Makuu ya halmashauri kunapotolewa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua katika kutatua changamoto zinazoweza kuathiri utekelezaji wa mpango huu wa kuwafikia vijana wengi zaidi na kuwajengea ujuzi wa kujitambua na kupambana na soko la ajira kutoka ndani na nje ya nchi. Hivyo ni maoni ya kamati kuwa Serikali itazingatia utolewaji wa kasi na kiasi cha fedha kulingana na mahitaji ambayo Wizara imejipangia.

(b) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa sheria ya usajili wa vizazi na vifo kwa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ilibainisha baadhi ya mafanikio yanayopatikana katika utekelezaji wa sheria ya usajili wa vizazi na vifo hapa nchini pamoja na changamoto zilizobainika na jinsi ya kuzitatua. Kwa upande wa mafanikio taarifa hiyo ilibainisha yafuatayo:

(i) Sheria imewezesha kusogeza huduma karibu kwa wananchi ikiwemo kuongeza vituo vyta usajili wa watoto kuanzia chini ya miaka mitano hadi 18 kutoka vituo 139 ambazo ni ofisi za Wakuu wa Wilaya hadi vituo 8,817.

(ii) Wananchi wengi wameondokewa na usumbufu wa kutumia muda mwingu kufuatilia vyeti vyta kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo uchambuzi wa kamati uliweza kubaini changamoto zifuatazo:

(i) Kuwepo kwa changamoto ya usajili ya kizazi cha mtanzania kilichotokea nje ya nchi, ambapo imebainika kwamba bado sheria haitoi mamlaka kwa RITA kutekeleza jukumu hilo.

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(ii) Huduma hii ya usajili wa watoto bado inaendelea kutegemea ufadhili wa wadau wa nje ya nchi kwa kiasi kikubwa.

(c) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu mpango mkakati wa Ofisi ya Mashtaka wa kuanzisha ofisi zake kila wilaya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa haki jinai kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo umebaini kuwa tangu kuanzishwa kwake ofisi hiyo imetekeliza yafuatayo:

(i) Kuratibu uanzishaji wa ofisi ya Taifa ya mashtaka katika ngazi za mikoa na wilaya na;

(ii) Kuratibu uandaaji wa miongozo inayohusu upeletelezi na uendeshaji wa mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizobainika pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za upeletelezi na mashtaka kwa kuanzisha ofisi za mashtaka mikoa 29 na wilaya 14 kumekuwa na changamoto ambazo zimekuwa zikirudisha nyuma juhudzi za Serikali za kusogeza huduma za mashtaka ya jinai kwa wananchi zikiwemo ziufatazo:

(a) Upungufu wa rasilimali fedha;

(b) Kukosekana kwa majengo ya ofisi;

(c) Upungufu wa watumishi na;

(d) Uhaba wa magari na vitendea kazi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha uchambuzi wa kamati umebaini kuwa *program* ya kutenganisha mashtaka na upeletelezi inajumuisha uratibu wa taasisi kadhaa ikiwa ni pamoja na majukumu ya aina mbalimbali. Hata hivyo

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

utekelezaji wa majukumu mbalimbali yaliyochini ya *program* hii imekuwa ikitegemea zaidi fedha kutokana na bajeti ya matumizi mengine kwa maana ya *OC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utegemezi wa chanzo hiki umekuwa na matatizo ya kutotosheleza hata kwa kulipia mahitaji yale ya msingi ya uendeshaji wa ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Miswada ya Sheria, katika kipindi kinachotolewa taarifa kamati ilichambua na kujadili jumla ya miswada sita ambayo ilichambuliwa na kujadiliwa na kamati na hatimae kuitishwa na Bunge. Miswada iliyofanyiwa kazi ni kama ifuatavyo:-

- (a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2021;
- (b) Muswada wa Sheria ya Maendeleo ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2021;
- (c) Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2021;
- (d) Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2021;
- (e) Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2021;
- (f) Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6, na. 7 wa mwaka 2021;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Miswada hii ilikusudia kufanya marekebisho katika sheria 58 kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji ili sheria hizo ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika sekta zinazohusika.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa Wizara ambazo kamati inazisimamia kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2021. Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba 2021 katika vikao vilivyofanyika Februari 2022. Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa bajeti kwa mafungu 14 ya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati kama ifuatavyo:

(a) Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano Fungu Na. 26 na 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 26 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais iliidhinishiwa shilingi bilioni 8.71 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia Disemba 2021 ofisi hiyo ilikuwa imepokea shilingi bilioni 5.85 sawa na 53.3% ya fedha iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 31 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira iliidhinishiwa sh. Bilioni 7.14 kama fedha ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.88 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Disemba 2021 Fungu hilo ilipokea shilingi bilioni 3.45 sawa na 48.3% ya fedha ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 128.08 sawa na 3% tu ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ilitaarifiwa kwamba fedha zilizopokelewa zilitekeleza majukumu mbalimbali ya ofisi ya Makamu wa Rais ikiwemo uratibu wa masuala ya muungano pamoja na usimamizi wa hifadhi ya mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ofisi hii inajumuisha mafungu manne ambayo ni Fungu 25 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu, Fungu 27 Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Fungu 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ofisi hii pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 57.81 kwa ajili ya matumizi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya kawaida ambapo hadi kufikia Desemba 2021 shilingi bilioni 37.4 zilikuwa zimepokelewa sawa na 72.5% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya maendeleo ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 9.52 kati ya hizo shilingi bilioni 3.52 ni fedha za nje na shilingi *billion* 6 ni fedha za ndani. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na ifuatayo:

- (i) Mradi wa makazi ya Waziri Mkuu, Mlimwa Dodoma,
- (ii) Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali na
- (iii) Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa vyama vyasiasa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kwamba hadi kufikia Desemba 2021 ofisi hii ilikuwa imepokea shilingi milioni 453.67 tu kati ya fedha yote ya maendeleo iliyoidhinishwa ikiwa sawa na asilimia 4.76 kamati ilibaini pia kati ya fedha hizo hakuna fedha ya nje iliyopokelewa kufikia Disemba 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Ofisi ina mafungu mawili ambayo nii Fungu 65 Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu pamoja na fungu 15 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Hadi kufikia Desemba 2021 Fungu Na. 15 ilipokea shilingi bilioni 1.93 kati ya shilingi bilioni 3.87 ya fedha ya matumizi ya kawaida ikiwa sawa na 49.87%ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 65 iliidhinishiwa shilingi bilioni 13.67 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia Desemba 2021 shilingi bilioni 7.12 ilipokelewa ikiwa sawa na 52.08%. Kamati ilitarifiwa kwamba fedha iliyopokelewa na ofisi hii na taasisi zake ilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa pamoja na uratibu, huduma, usimamizi na tathmini ya masuala mbalimbali ya kisera.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande bajeti ya maendeleo Fungu Na. 65 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 11.81 ambapo katì ya hizo shilingi *billion* 10 ni fedha za ndani ili kutekeleza miradi ifuatayo: *Program* ya kukuza kazi za staha, *Program* za kukuza ujuzi nchini na *Program* za maendeleo ya vijana. Hadi kufikia Desemba 2021 Fungu 65 lilikuwa limepokea shilingi bilioni 6.20 sawa na 52.56% ya fedha iliyotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake Kamati imeridhishwa na naipongeza Serikali kwa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo hasa ukizingatia kuwa miradi hiyo inalenga nguvu kazi ya Taifa (vijana).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa na Bunge shilingi bilioni 178.77 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Desemba 2021 Wizara pamoja na taasisi zake zilipokea kiasi cha shilingi bilioni 9.83 ikiwa ni sawa na 51% ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa upande wa miradi ya maendeleo Bunge liliidhinishia Wizara hiyo pamoja na taasisi zake jumla ya shilingi bilioni 52.91 ambapo hadi kufikia Desemba 2021 Wizara pamoja na taasisi zake zote zilikuwa zimepokea kiasi cha shilingi bilioni 16.18 sawa na takriban 30.58% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tathmini ya kamati utekelezaji wa bajeti za Wizara ni wa kuridhisha kwa kuwa sehemu kubwa fedha iliyokuwa imeidhinishwa ilipokelewa kwa kadri ilivyotarajiwa. Hata hivyo kamati imebaini kuwepo na mwenendo usioridhisha kwa upande wa fedha iliyotengwa kwa miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia nusu mwaka mapokezi yalikuwa chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya kamati kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu sehemu ya kwanza inahusu utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa maafa wa mwaka 2014.

Kwa kuwa, imebainika kuwepo uelewa na ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika halmashauri zetu

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

nchini kuhusu mfumo wa usimamizi na udhibiti wa maafa katika ngazi za kata, tarafa na wilaya kwa mujibu wa sheria.

Na Kwa Kuwa, ombwe la uelewa na ushirikishwaji wa wananchi katika kudhibiti maafa yanayotokea kwenye maeneo yao unaathiri utekelezaji wa sheria ya maafa kwa kiwango kilichokusudiwa.

Hivyo basi, kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(i) Ione umuhimu wa kuandaa mfumo wa utoaji elimu ya udhibiti wa maafa kama sehemu ya masomo kuanzia elimu ya msingi kutokana na ongezeko kubwa la madhara ya mabadiliko ya tabia ya nchi;

(ii) Kuandaliwe mkakati endelevu wa udhibiti wa maafa na madhara yake katika visiwa vya Zanzibar kwa kuwa hili ni suala la Muungano na kwa hasa kwa kuzingatia jiografia ya Kisiwa hicho;

(iii) Ione umuhimu wa kuifanya marekebisho sheria hii ili Wabunge wawe sehemu ya wajumbe wa kamati za maafa katika ngazi ya wilaya na mkoa na;

(iv) Ione umuhimu wa kuwa na mfuko maalum wa usimamizi na udhibiti wa maafa nchini chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa lengo la kuwa na bajeti ya uratibu wa masuala ya maafa hasa yale ambayo yanaathari za kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, Mfuko wa maendeleo ya vijana kwa kuwa kamati imebaini uwepo mfuko wa maendeleo ya vijana kuwa ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya vijana nchini, kutokana na uratibu mzuri unaotekelzwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na kwa kuwa kuwepo kwa mahitaji makubwa ya vijana zaidi ya uwezo wa Mfuko kunaweza kusababisha fursa hiyo isiwafikie vijana wengi nchini;

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Hivyo basi Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

(i) Kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ili Mfuko huo uweze kuwafikia vijana wengi zaidi kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kudhihirisha uwezo mkubwa katika uratibu wa Mfuko huo;

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane kwa ukaribu zaidi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ndiyo wenyewe dhamana na halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila halmashauri inawajibika kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana pamoja na asilimia 4% za fedha za halmashauri, kwa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na marejesho yake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria; utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo kwa Ustawi wa Jamii:-

Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa, ufanisi katika utekelezaji wa sheria hii unategemea sana ushirikiano wa kiutendaji kati ya *RITA* na *NIDA*;

Na kwa kuwa ushirikiano wa taasisi hizo pamoja na nyingine za Serikali ni wa umuhimu kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na Vitambulisho vya Taifa kwa watu ambao hawatakiwi kwa mujibu wa Sheria;

Na kwa kuwa fursa za mwingiliano wa Watanzania na wananchi wa mataifa mengine unahitaji umakini katika kuhakisha haki ya Utaifa inazingatiwa kwa mujibu wa sheria za nchi zilizopo kwa sasa;

Hivyo basi Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo: -

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) Kuhakikisha kunakuwepo ushirikiano wa karibu baina ya mifumo *RITA* na *NIDA* ili kuondoa changamoto ya mtu asiyekuwa Mtanzania kukutwa ana cheti cha kuzaliwa kwa hoja kwamba, aliomba cheti hicho kwa sababu alikuwa na cheti cha *NIDA*;

(ii) Kuanzishwe mfumo rasmi kisheria na kiusimamizi wa kusimamia taarifa za vizazi na vifo kwa Watanzania walioko nje ya nchi hususan wale ambao bado hawajakana Utanzania wao;

(iii) Serikali ianze kujipanga kuanzisha mfumo wa kibajeti wa gharama za uratibu wa Programu ya usajili wa Matukio ya Binadamu pasipokuendelea kutegemea wadau wa nje ambao wanaweza kutoweke muda wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 na Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria za Mwaka 2018:-

Kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa idadi ndogo ya watoa huduma ya Msaada wa Kisheria nchini ikilinganishwa na idadi ya watanzania wanaohitaji msaada wa kisheria;

Na kwa kuwa watoa huduma ya msaada wa kisheria waliopo, hususan wasaidizi wa kisheria, wamebainika kutokuwa na bajeti za kutosha kuendesha shughuli zao;

Na kwa kuwa huduma ya msaada wa kisheria kutegemea sana bajeti za wahisani ambazo sio endelevu kutekeleza majukumu ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

Na kwa kuwa uwepo wa changamoto hizo unaathiri upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wengi ambao hawatambui hatua za kisheria za kuchukua wanapokabiliana na changamoto ya kisheria kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha katika masuala ya kisheria;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Hivyo basi Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza yafuatayo:-

(i) Ione umuhimu wa kuondoa au kupunguza ada ya usajili wa watoa huduma ambao tayari wameshasajiliwa kama AZAKI (*NGOs*) ili kuwapunguzia gharama za utoaji wa huduma hii kwa kuwa inatolewa bure kwa wananchi;

(ii) Ione umuhimu wa kuandaa mpango wa kibajeti wa kuanza kutumia bajeti ya Serikali na wadau wengine kufadhili shughuli za watoa huduma ya msaada wa kisheria kupitia Mfuko wa Msaada wa Kisheria, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, watoa huduma hao wanawafikia wananchi wengi zaidi hususan wananchi wa vijiji; na

(iii) Wizara kwa kushirikiana na wadau wake lendelee kutoa elimu kwa Umma kwa jamii kuhusu haki za makundi hususan wanawake na watoto katika umiliki wa mali kwa njia mbalimbali ikiwemo kurithi, pamoja na haki za makundi hayo katika jamii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Mkakati wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa kuanzisha ofisi zake kwa kila Wilaya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa haki jinai kwa wananchi:-

Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa, jitihada za kutungwa kwa sheria ya kusimamia mfumo wa uendeshaji wa mashtaka nchini haikwenda sambamba na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wake;

Na kwa kuwa utekelezaji wa mpango huo ulitegemea sana fedha za matumizi ya kawaida (*OC*), ambazo hazikuweza kukidhi mahitaji kwani baadhi ya kazi za mpango wa kutenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka zilikuwa zinaathiri shughuli za maendeleo kama vile kazi za ujenzi wa ofisi, ununuzi wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta, samani za ofisi na usimikaji wa mfumo wa kieletroniki;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Na kwa kuwa hali hiyo ya ufinyu wa bajeti imeshindwa kukidhi mahitaji kutokana na kasi ya uboreshwaji wa huduma za Mahakama nchini na hivyo kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa mpango huo;

Hivyo basi ili kuimarisha na kurahisisha usimamizi wa mifumo ya utoaji haki jinai nchini kwa wakati, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuongezwe Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa matumizi ya mengineyo (*OC*) na maendeleo kulingana na maoteo ya bajeti ya ofisi ambayo itakadiriwa na kuthibitishwa kama bajeti halisi kwa ustawi wa ofisi hii;

(ii) Kuwepo na Programu Maalumu ya Ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa na Wilaya kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo au kutumia rasilimali fedha zinazokusanya na ofisi kwa njia ya utaifishaji au ulipaji wa fidia; na

(iii) Motisha na mazingira ya kazi kwa watumishi viboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi katika mifumo ya utoaji haki nchini:-

Kwa kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati;

Na kwa kuwa usimamizi wa utoaji wa haki nchini unategemea sana ufanisi wa taasisi husika zenye dhamana hiyo;

Hivyo basi Kamati inaendelea kuzishauri taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria zinazohusika na usimamizi wa utoaji haki kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

(i) Mhimili wa Mahakama uendelee kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake uliojiwekea wa kuhakikisha kila hakimu

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

na jaji anashughulikia na kukamilisha idadi ya mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya wananchi kwa chombo hicho;

(ii) Serikali iendelee kuboresha Bajeti ya Fungu 55; na

(iii) Serikali ione umuhimu wa kuboresha mazingira ya rasilimali watu chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson na Naibu Spika pamoja na wewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mliota kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote. Kwa kutambua mchango wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, naomba niwatambue Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao wamepewa dhamana ya kuongoza Wizara mbalimbali zinazosimamiwa na Kamati yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Profesa Joyce Ndlichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Patrobas Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Khamis Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa. Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hizi pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano ambao wametupa kama Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati pale alipohitajika kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha hoja za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkoo wa Sheria wa Serikali (*CPD*) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada mbalimbali. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa washauri wa masuala ya sheria Bungeni kwa namna bora walivyoshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza majukumu katika kipindi hiki cha taarifa. Orodha ya baadhi ya wadau hao ipo katika ukurasa wa 68 wa taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyoordheshwa katika taarifa hii, ukurasa wa 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mwihambi (*ndc*), kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelawa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli ilizozitekeleza kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofii)*

### **TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2021 HADI FEBRUARI, 2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa Chini ya Kanuni ya 136(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **1.0 MAELEZO YA JUMLA**

###### **1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani leo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa Kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii adhimu kukupongeza kwa kuchaguliwa na Bunge letu tukufu kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi wa asilimia mia

moja (100%) ni kielelezo kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana imani kubwa. Aidha, nimpongeze **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb)**, kwa kuchaguliwa kwa asilimia tisini na nane nukta tatu tatu (98.33%).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini, kuniunga mkono na kunichagua kwa asilimia mia moja (100%) kuwa kiongozi wao. Aidha, kwa kutambua nafasi yao katika utendaji wa Kamati hii, ninawashukuru sana **Mhe. Mohammed Ommary Mchengerwa (Mb)** – Waziri wa Michezo na Utamaduni, pamoja na **Mhe. Najma Murtza Giga (Mb)** – Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Mwenyekiti wa Bunge ambao wameongoza Kamati hii kwa vipindi tofauti katika mwaka huu. Bila wao, taarifa hii isingekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekeliza na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo: -

- a) Sehemu ya Kwanza inatoa Maeleo ya Jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekeliza;
- b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- c) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- d) Sehemu ya Nne ni hitimisho la taarifa.

## 1.2 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Katiba na Sheria ni mionganini mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo imeundwa chini ya Kifungu cha 5 (b) kikisomwa pamoja na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kamati imepewa jukumu la kusimamia Wizara nne (4) zifuatazo: -

- a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)
- b) Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu
- c) Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu); na
- d) Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa Kamati nydingine za kisekta, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria imekabidhiwa majukumu yafuatayo: -

- a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### **1.3 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Katiba na Sheria hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge kwa mujibu wa **Ibara ya 96 (1)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ili kutimiza masharti ya **Ibara ya 63 (2)** ya Katiba ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

136 (3) na (5) kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2020/2021 na 2021/2022 kama ifuatavyo:-

- i) Vikao vya uchambuzi wa Bajeti za Serikali kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge.
- ii) Vikao vya kushughulikia Miswada ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iii) Kupokea maoni ya Wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iv) Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoishia kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake, kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotengwa na kupokelewa na taasisi husika;
- v) Vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa Fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- vi) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge,

### **1.4 Shughuli zilizoteklezwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeliza shughuli zifuatazo: -

#### **1.4.1 Kutembelea na kukagua utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayozitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilitembelea na kukagua Miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

#### **1.4.2 Kuchambua Miswada ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati hii ilishughulikia Jumla ya Miswada ya Sheria Sita (6) iliyofanya marekebisho katika Jumla ya Sheria Hamsini na Nane (58) zinazohusu Sekta mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 1) wa Mwaka 2021 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) ACT, No. 1 of 2021]**

**Mheshimiwa Spika** Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Tatu ambazo ni: -

- i) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1,
- ii) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216: na
- iii) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Marekebisho hayo ni kutambua rasmi Matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya Sheria na lugha ya Mahakama.

b) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2021 [The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No.2 of 2021]**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Kumi na Mbili (12) kwa lengo la kurahisisha utekelezaji madhubuti wa Sheria hizo na kuondoa upungufu uliojitezea wakati wa utekelezaji wake. Sheria hizo ni:-

- i) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act, Cap.341)
- ii) Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 (The Birth and Deaths Registration Act, Cap.108)
- iii) Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 (The Business Names (Registration) Act, Cap 213);
- iv) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 (The Civil Aviation Act, Cap. 80);
- v) Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 (The Companies Act, Cap. 212);
- vi) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 (The Environmental Management Act, Cap.191);
- vii) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (The Interpretation Act, Cap.1);
- viii) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (The Land Disputes Courts Act, Cap.216)
- ix) Sheria ya Mahakama za Hakimu, Sura ya 11(The Magistrates' Courts Act, Cap. 11)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- x) Sheria ya Uendeshaji Bunge, Sura ya 115 (The National Assembly (Administration) Act Cap. 115)
  - xi) Sheria ya Utalii, Sura ya 65 (The Tourism Act Cap.65); na
  - xii) Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326 (The Trade and Service Marks Act, Cap.326)
- c) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 (The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2021;**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu ulifanya marekebisho ya Sheria mbalimbali Kumi na Nne (14) ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba inayohusiana na Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Bomba litakalosafirisha Mafuta Ghafi kutoka Holma – Uganda hadi Chongoleani, Tanga – Tanzania na miradi mingine ya kimkakati. Sheria zilizofanyiwa Marekebisho ni:-

- i) Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta, Sura ya 306 (The Electronic and Postal Communications Act, (Cap. 306);
- ii) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 (The Environmental Management Act, (Cap. 191);
- iii) Sheria ya Ushindani wa Biashara, Sura ya 285 (The Fair Competition Act, (Cap. 285);
- iv) Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5 (The Government Proceedings Act (Cap. 5);
- v) Sheria ya Bima, Sura ya 394 (The Insurance Act, (Cap. 394);
- vi) Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 (The Local Government (District Authorities) Act, (Cap. 287);
- vii) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290(The Local Government Finances Act, (Cap. 290);

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- viii) Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288 (The Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288);
- ix) Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449 (The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449);
- x) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi, Sura ya 450 (The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450);
- xi) Sheria ya Petroli, Sura ya 392 (The Petroleum Act, (Cap. 392);
- xii) Sheria ya Reli, Sura ya 170 (The Railways Act, (Cap. 167);
- xiii) Sheria ya Barabara, Sura ya 167 (The Roads Act, (Cap. 167); na
- xiv) Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103 (Public Private Partnership Act, (Cap. 103).

d) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No.4 of 2021*).**

**Mhesimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria kumi na moja (11) zifuatazo: -

- i) Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta, Sura ya 306 [*The Electronic and Postal Communications Act, (CAP 306)*];
- ii) Sheria ya Stahili na Mafao ya Kustaafu ya Majaji, Sura ya 424 [*The Judges (Remuneration and Terminal Benefits Act, (CAP 424)*];
- iii) Sheria ya Idara ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70, [*The Medical Stores Department Act,) (Cap 70)*];
- iv) Sheria ya Madini, Sura 123 [*The mining Act, (Cap 123)*]

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- v) Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129 [*The National Council for Technical Education Act, (CAP 129)*];
- vi) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, (Sura 395) [*The National Health Insurance Fund Act, (Cap 395)*];
- vii) Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 [*The Non-citizens (Employment Regulation Act (Cap. 436)*];
- viii) Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya Viongozi wa Kisiasa, Sura ya 225 [*The Political Service Retirement Benefits Act, (Cap 225)*];
- ix) Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura ya 447 [*The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act, (Cap.447)*];
- x) Sheria ya Shirika la Posta Tanzania, Sura ya 303 [*The Tanzania Postal Corporation Act, (Cap 303)*];
- xi) Sheria ya Huduma za Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 422 [*The Universal Communications Service Access Act, (Cap.422)*];
- xii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82 [*The Vocational Education and Training Act, (Cap. 82)*] na
- xiii) Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 [*The Workers Compensation Act, (CAP 263)*].

**Mheshimiwa Spika, Madhumuni** ya marekebisho ya Sheria hizo ni kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria husika.

e) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No.5 of 2021*)**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika 'Sheria Tisa (9) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Orodha ya Sheria zilizofanyiwa Marekebisho katika Muswada huu ni hizi zifuatazo:-

- i) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432;
- ii) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyा, Sura ya 95;
- iii) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura ya 366;
- iv) Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura ya 180;
- v) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54;
- vi) Sheria ya Tasnia ya Nyama Sura ya 421;
- vii) Sheria ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza Sura ya 241;
- viii) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma; Sura ya 371; na
- ix) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260.

f) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) wa Mwaka 2021 (The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, No.7 of 2021);**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Orodha ya Sheria zilizofanyiwa Marekebisho katika Muswada huu ni hizi zifuatazo: -

- i) Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Sura ya 209
- ii) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- iii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20
- iv) Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200
- v) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430
- vi) Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49
- vii) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16
- viii) Sheria ya Upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 422; na
- ix) Sheria ya Veterinari, Sura ya 319.

### **1.4.3    Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kifungu cha 6 (2)(a) na(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(d) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili Jumla ya Taarifa (9) za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozismamia pamoja na Taasisi zake, ambapo, Taarifa Tano (5) ziliwasilishwa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taarifa Nne (4) kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama ifuatavyo:-

#### **a)        Taarifa Tano (5) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu:-**

- i) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2014
- ii) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi ya Mwaka 2003;
- iii) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Shughuli za Kiwanda cha Viatu na bidhaa za Ngozi kinachomilikiwa kwa ubia na Jeshi la Magereza na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF); Aidha, kwa kibali cha Spika, Kamati ilifanya ziara

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya kutembelea na kukagua kiwanda hicho Mkoani Kilimanjaro, kuanzia tarehe 22-24 Oktoba, 2021.

iv) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mpango wa kupanua Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa lengo la kuwafikia Vijana wengi zaidi; na

v) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni, Sura ya 436.

**b) Taarifa Nne (4) kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu:-**

i) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo kwa ustawi wa Jamii;

ii) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017; na Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria za Mwaka 2018;

iii) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Mpango Mkakati wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa kuanzisha Ofisi zake kwa kila Wilaya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa Haki Jinai kwa Wananchi; na

iv) Taarifa ya wizara ya katiba na sheria kuhusu ufanisi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na mchango wake katika sekta ya sheria nchini.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (c) cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**1.5 Uchambuzi wa Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kwa Kipindi cha Nusu Mwaka Kuanzia Julai hadi Disemba, 2021**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ikinsomwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, katika Vikao vya Mwezi Februari, 2022 kuelekea Mkutano wa Sita (6) wa Bunge la Kumi na Mbili, Kamati ilipokea na Kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha Nusu Mwaka, kuanzia Julai hadi Disemba, 2021, kwa kuzingatia fedha iliyoldhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Wizara nne (4) Pamoja na tasisi zake ziliwasilisha taarifa zake zikibainisha utekelzaji wa bajeti kwa kipindi hicho. Matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

### **SEHEMU YA PILI**

## **2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**2.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelzeza na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa Taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuiwezesha Kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyobainishwa na Kamati kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Yatokanayo na Taarifa za Utendaji wa Taasisi za Serikali

#### A. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2014

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 20 Oktoba, 2021 ilibainisha hatua mbalimbali zinazochukuliwa kuimarisha Usimamizi wa Maafa nchini. Baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo: -

- i) Kuimarisha uwezo wa Jamii na Kamati za Usimamizi wa Maafa
- ii) Kuimarisha uwezo wa vifaa vya utafutaji na uokoaji
- iii) Kufanya tathmini za hatari ya majanga
- iv) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa ambacho kitaanzishwa Jijini Dodoma; na
- v) Kuanzisha Jukwaa la Kidigitali la Usimamizi wa amafunzo na ukame.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kuchambua kwa kina kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa kwenye SEHEMU YA TATU ya taarifa hii.

#### B. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 21 Oktoba,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

2021, Kamati ilichambua na kubaini kuwa, OSHA imeweza kuitambulisha Tanzania katika nchi za SADC katika masuala ya Usalama na Afya Mahali pa kazi, ambapo Wakala umepata Dawati la Usalama na Afya Mahali pa kazi katika jumuiya hiyo.

Aidha, Wakala umezingatia maoni na Ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu la Kumi na Moja (11), kuhusu kuondoa tozo ambazo zilibainika kuwa kero kwa Wadau wa Wakala huu hususan Wawekezaji wa Sekta ya Viwanda na Makampuni. Hivyo, Kamati imebaini kuwa, jumla ya tozo na ada 11 zimeondolewa kupitia GN 719 ya tarehe 16 Novemba, 2018, GN 994 ya Tarehe 13 Novemba, 2020 na GN.496F ya tarehe 30 Juni, 2021. Pia, hatua hiyo imekwenda sambamba na Wakala kupunguza Urasimu katika kuwashudumia wadau kwa kuboresha Mifumo ya TEHAMA.

Vile vile, Kamati imeridhishwa na hatua ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu kukamilisha ujenzi wa Jengo Jipyaa la Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Wakala huo Jijini Dodoma, ambapo kwa Maoni ya Kamati baada ya kutembelea na kukagua Jengo hilo, Jengo hilo limezingatia mahitaji ya ukuaji wa shughuli za Wakala na limekidhi vigezo vya kuhudumia Makundi Mbalimbali ya Wadau ikiwemo Wadau wenye mahitaji Maalum. Maoni ya Kamati ni kuwa, Taasisi nyngine za Serikali zitaiga mfano huo mzuri wakati wa Ujenzi wa Ofisi zao hapa Jijini Dodoma.

**Mheshmiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, kulibainika pia baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi, ili kuendeleza mafanikio ya Wakala yaliyofikiwa pamoja na kuongeza ufanisi zaidi. Changamoto hizo ni:-

- i) OSHA imebainika kukabiliwa na changamoto ya Watumishi, ambapo ina takriban watumishi 70 tu badala ya watumishi wasiopungua 136 wanaohitajika kwa sasa;
- ii) Kuwepo kwa ongezeko la Vihatarishi vya Usalama na Afya mahali pa kazi linalochangiwa na mabadiliko ya teknolojia za kisasa; na

iii) Uelewa mdogo wa Masuala ya Usalama na Afya mionganini mwa wadau inaathiri utekelezaji wa Sheria kwa ufanisi zaidi;na

**Mheshimiwa Spika, baada** ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilioa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

**C. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Shughuli za Kiwanda cha Viatu na bidhaa za Ngozi kinachomilikiwa kwa ubia na Jeshi la Magereza na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu mbele ya Kamati, ya tarehe 22 Oktoba, 2021, ilibainisha kuwa, Mwezi Machi, 2017, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na uliokuwa Mfuko wa Pensheni wa PPF, ulianzisha Kampuni ya Ubia illyojulikana kwa jina la '*Karanga Leather Industries Co. Ltd*' ili kutekeleza mradi huu. Kwamba, baadaye Kampuni ilibadilisha jina na kuitwa "*Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd (KLICL)*", kama sehemu ya mkakati wa kujitangaza na kuweka mweleko mpya.

Aidha, taarifa hiyo ilibainisha kuwa, baada ya kuunganishwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini, Mfuko wa PSSSF ulirithi mali zilizokuwa zinamiliwi na Mfuko wa PPF, ikiwa ni pamoja na umiliki wa Kampuni hii. Hivyo, Mfuko wa PSSSF unamiliiki hisa za Kampuni kwa **asilimia 86** na Jeshi la Magereza kwa **asilimia 14**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Umiliki wa Jeshi la Magereza katika Kampuni unatokana na mchangwo eneo la kiwanda lenye hekari 25 lenye thamani ya **shilingi Bilioni 10.04**. Aidha, Mchangwo wa Mfuko wa PSSSF ni kugharamia ujenzi wa Majengo ya Kiwanda, ununuzi wa Mashine na Mitambo na gharama za awali za uendeshaji wa Kampuni, ambapo mpaka kukamilika kwa mradi zinatarajiwa kufikia **shilingi Bilioni 126.19**. Kati ya kiasi hicho **shilingi bilioni 59.96** ni mchangwo wa hisa katika Kampuni na **shilingi Bilioni 66.23** ni mkopo kwa kampuni ambao unatarajiwa kurejeshwa katika kipindi cha miaka 10.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea na kujadili taarifa hiyo, kwa kibali chako, mnamo tarehe 23 hadi 24 Oktoba, 2021, Kamati ilifanya ziara Mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kujiridhisha yaliyobainishwa kwenye taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu ufanisi wa Mradi huo, ambapo kutokana na ziara hiyo, Kamati ilibaini faida za mradi huo kwa Nchi kama ifuatavyo:-

- i) Mradi huo ni kitega uchumi mahsus i kwa ajili ya kulinda thamani ya uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa PSSSF na Jeshi la Magereza kwa ustawi wa fedha za Mfuko na Taifa kwa ujumla;
- ii) Mradi umelenga kuinua Uchumi wa Wafugaji nchini kwa kutoa soko la uhakika la ngozi ghafi kutoka kwa wafugaji hao kwenye Mikoa ya Jirani na Mikoa mingine hapa nchini;
- iii) Mafunzo Maalum ambayo yamekuwa yakitolewa na Mradi kwa Jamii ya Wafugaji kuhusu namna bora ya ufugaji na uchunaji unalenga kuongeza thamani ya ngozi inayozalishwa hapa nchini, hatua ambayo itaongeza uthamani wa bidhaa za Ngozi na hivyo kukidhi ushindaji wa Soko la ndani nan je ya nchi;
- iv) Mradi huo umelenga kutengeneza Ajira za moja kwa moja 3,000 na zaidi ya ajira 7,000 zisizo za moja kwa moja katika mnyororo wa thamani na huduma;
- v) Upo uwezekano Mkubwa wa Mradi huo kuongeza mapato ya Taifa kupitia kodi mbalimbali;
  
- vi) Mradi utakuwa na manufaa makubwa kwa Mkoaa wa Kilimanjaro pamoja na Mikoa jirani kwa kuboresha mfumo wa maisha na kuongeza kipato kwa Wakazi; na
- vii) Mradi unaweza kusaidia ukoaji wa fedha za kigeni kwa kupunguza uingizaji wa bidhaa za ngozi nchini na kuongeza mapato ya fedha za kigeni kwa kuuza bidhaa za ngozi nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati **kupokea** na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mradhi huo pamoja na kuutembelea mradi huo, ilioa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

**D. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mpango wa kupanua Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa lengo la kuwafikia Vijana wengi Zaidi**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusu taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu mbele ya Kamati, ya tarehe 25 Oktoba, 2021, ilibainisha kuwa, Mpango wa kupanua Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa lengo la kuwafikia Vijana wengi zaidi unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- i) Kuibuka kwa uhitaji mkubwa wa mafunzo ya kukuza ujuzi kutoka kwa vijana ambao hawakupata fursa ya kuendelea na elimu ya juu, kutokana na hali duni za familia zao hususan familia za vijiji;
- ii) Vijana wengi kushindwa kumudu gharama za kuhudhuria mafunzo, kwasababu ya umbali kutoka wanakoishi vijiji kuja kwenye makao makuu ya Halmashauri kunapotolewa mafunzo hayo; na
- iii) Vijana wengi wamekosa elimu ya kujitambua, uelewa juu ya stadi za maisha na ujasiriamali, ambapo imebainika vijana wengi hawaoni umuhimu wa kupata mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini changamoto hizo, Kamati illomba ufanuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutatua changamoto hizo, hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa, Programu hiyo ni muhimu katika kuwawezesha Vijana kupata ujuzi utakaowawezesha aidha kukidhi ushindani wa Soko la Ajira au kujajiri wenyewe na kuwaajiri Vijana wenzao.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifa Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu mbele ya Kamati, ya tarehe 25 Oktoba, 2021, ni kwamba, Serikali ya

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, imepanga kutumia shilingi Bilioni 550 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii kwa kipindi cha miaka mitano (5), ambapo Shilingi Bilioni 102 zimepangwa kutumika kila mwaka wa Fedha kwa kipindi cha mwaka 2021/22-2025/2026. Hivyo, kwa mpango huu wa kibajeti, Programu itaweza kutoa mafunzo kwa jumla ya Vijana 681,000 kwa kipindi hicho cha miaka mitano (5), ambapo jumla ya Vijana 136,000 watafikiwa kwa kila mwaka, ikilanganishwa na Vijana 20,000 wanaopatiwa mafunzo ya ujuzi kwa mwaka, kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo muhimu kwa kuwa imeonesha nia njema katika utatuzi wa changamoto zinazoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango huu wa kuwafikia Vijana wengi zaidi na kuwajengea Ujuzi wa kujitambua na kupambana na Soko la Ajira kutoka ndani na nje ya nchi. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itazingatia utolewaji wa kiasi hicho cha fedha kwa wakati, kwa kipindi cha miaka mitano kama ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Programu hiyo ya kuwajengea Ujuzi Vijana nchini, Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

### **E. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni, Sura ya 436**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 26 Oktoba, 2021, ilibainisha mafanikio na changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa Sheria hiyo, katika kuimarisha uratibu wa Ajira za Wageni, kuongeza fursa za Ajira kwa wazawa kupitia uwiano wa idadi ya Wafanyakazi wageni na wazawa pamoja na kurithisha ujuzi wa kazi kwa Wazawa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa hiyo, Kamati ilibaini baadhi ya changamoto katika mfumo wazamani wa kuratibu maombi ya vibali vya kazi kama ifuatavyo:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) Mfumo ultumia muda mrefu katika uchambuzi wa maombi
- ii) Mfumo ulisababisha ongezeko la gharama kwa mwombaji;
- iii) Mfumo ulichochea mahusiano yenyе viashiria vya rushwa baina ya Watendaji na Waombaji Vibali;
- iv) Kuwepo kwa mifumo tofauti ya kiserikali katika kushughulikia vibali vya Kazi na Ukaazi(Work Permit and Residence Permit) baina ya Uhamiaji na Ofisi ya Kamishna wa Kazi; na
- v) uwepo wa vishoka (middlemen) waliojihuisha na shughuli hii kinyume cha sheria.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, Kamati ilibaini baadhi ya mafanikio kutokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kutatua changamoto hizo. Baadhi ya mafanikio hayo ni: -

- i) Kuanzishwa kwa mfumo mpya wa kielektroniki wa kuratibu Ajira za Wageni kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali Na. 4 ya Mwaka 2021;
- ii) Kuongezeka kwa muda wa kufanya kazi nchini kwa raia wa kigeni kutoka miaka 5 hadi 8 hatua ambayo itaongeza fursa ya kuendelea kupata ujuzi kwa wazawa;
- iii) Kuongezeka kwa idadi ya Wageni nchini na hivyo kukuza uchumi wa nchi;
- iv) Uwiano wa Idadi ya Ajira ya Mgeni Mmoja kwa Wazawa 10 uliotokana na marekebisho ya Sheria utaongeza uwigo wa ajira kwa wazawa; na
- v) Mfumo mpya wa kielektroniki umechochea ongezeko la makusanyo ya maduhuli ya Serikali ambapo, kwa kipindi cha Julai hadi tarehe 30 Septemba, 2021 Jumla ya Shilingi Bilioni 17,017,874,775 zimekusanywa ikilinganishwa na shilingi Bilioni

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

3.89 zilizokusanywa kwa kipindi hicho hadi tarehe 30 Septemba, 2020 kupitia ada za vibali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, Kamati ilioa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa mfano mzuri katika kutekeleza ushauri na maoni ya Kamati, kwa ufanisi mkubwa. Utekelezaji huo umethibitishwa na Kamati siyo tu kwa kupitia taarifa za Serikali bali kwa Kamati kutembelea baadhi ya Programu, Miradi na Taasisi Kama Vile OSHA, WCF, NSSF na PSSSF, inayoratibiwa na Ofisi hii na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati.

### **F. Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo kwa ustawi wa Jamii**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ilibainisha baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo hapa nchini pamoja na changamoto zilizobainika na jinsi ya kuzitatua. Kwa upande wa mafanikio, taarifa hiyo ilibainisha yafuatayo:

- i) Sheria imewezesha kusogeza huduma karibu kwa Wananchi, ikiwemo kuongeza vituo vya Usajili wa Watoto kuanzia chini ya miaka 5 hadi 18, kutoka vituo 139 ambazo ni Ofisi za Wakuu wa Wilaya hadi Vituo 8,817 vikiwa na vituo vya kutolea huduma za afya 5,656 na Ofisi za Kata 3,161;
- ii) Wananchi wengi wameondokewa na usumbufu wa kutumia muda mwingi kufuatilia yeti vya kuzaliwa
- iii) Mafunzo mbalimbali yameendelea kutolewa katika kuwajengea uwezo Watumishi wa OR - TAMISEMI, pamoja na kupewa vitendea kazi ambavyo vimeongeza ufanisi zaidi;

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- iv) Mfumo wa matumizi ya TEHAMA kupitia Simu janja umerahisisha sana uratibu wa taarifa za mtoto na kuzituma kwa Wakala kwa ajili ya Usajili;
- v) Usajili umekuwa wa papo kwa papo na hivyo kupunguza hatua nyingi za usajili zilizokuwepo;
- vi) Kuondolewa kwa ada za usajili kwa watoto chini ya miaka 5 na hivyo kuhamasisha usajili wa Watoto wengi zaidi;
- vii) Elimu imeendelea kutolewa kwa jamii kuhsu umuhimu wa usajili na kuwa na cheti cha kuzaliwa;
- viii) Uhakika wa upatikanaji wa taarifa za mtoto pale zinapohitajika;
- ix) Kuwezesha mabadiliko ya jina la mtoto kuanzia miaka 2 hadi 18;
- x) Kuondoa ingizo kwenye rejestra pale inapobainika mtoto au mtu amesajiliwa ziadi ya mara mbili;
- xi) Kuanzishwa kwa utaraibu wa usajili wa Vifo viavyotokea nje ya nchi tofauti ilivyokuwa kabla ya marekebisho ya sheria hii ambapo kwasasa sheria imetoa mamlaka kwa RITA kusajili Vifo vyta ya Watanzania wanaofariki nje ya nchi;
- xii) Sheria imewezesha kuimarisha usiri wa taarifa za mtu kuhusu taarifa zake za vizazi au vifo ikiwa ni pamoja na taarifa za vyeti; na
- xiii) Uwepo wa huduma ya utoaji wa cheti cha kuzaliwa kwa Watoto walioasiwa ili wavitumie kupata huduma mbalimbali za kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, uchambuzi wa Kamati uliweza kubaini changamoto zifuatazo: -

- i) Kuwepo kwa changamoto ya usajili wa kizazi cha mtanzania kilichotokea nje ya nchi, ambapo imebainika

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

kwamba, bado Sheria haitoi mamlaka kwa RITA kutekeleza jukumu hilo;

- ii) Huduma hii ya usajili wa Watoto bado inaendelea kutegejemea ufadhili wa wadau wa nje kwa kaisi kikubwa: na
- iii) Watendaji wa RITA wameendelea kukaimu kwa muda mrefu zaidi ya masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, Kamati ilioa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

### **G. Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017: na Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria za Mwaka 2018**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ulibainisha kuwa, katika kutekeleza Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017 na Kanuni zake, yafuatayo yamefanyika kwa ufanisi mkubwa: -

#### **i) Utoaji wa elimu ya kisheria kwa wananchi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ni jukumu la Serikali kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi kwenye masuala mbalimbali kama vile ardhi, mirathi, ndoa, ajira na maeneo mengineyo, ambapo, hadi sasa, wizara kupitia watoa huduma ya msaada wa kisheria imefanikiwa kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi wapatao 1,627,690 ambapo wanaume ni 1,180,519, wanawake ni 348,631 na watoto ni 98,540.

#### **ii) Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwenye maeneo ya vizuizi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa hii ulibainisha kuwa, kupitia sheria hii, elimu ya kisheria imeweza kutolewa kwenye

maeneo ya vizuizi (Vituo vya Polisi na Magerezani). Aidha, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na wadau wanaotoa huduma ya msaada wa kisheria, walitua elimu ya kisheria kwenye maeneo ya vizuizi.

Pia, jumla ya watuhumiwa na wafungwa wapatao 11524 walipata huduma ya msaada wa kisheria ikijumuisha elimu kwa umma na ushauri wa kisheria, katika hao wanawake wapatao 872 walipata huduma ya msaada wa kisheria ambapo 196 walipata ushauri wa kisheria na 676 walipa elimu ya sheria. Vilevile, watuhumiwa na wafungwa wapatao 10,352 walipata msaada wa kisheria ambapo 2,115 kati ya hao walipata ushauri wa kisheria na 8,237 walipata elimu ya sheria, na watoto amba ni watuhumiwa wapatao 300 walipata huduma ya msaada wa kisheria ambapo 136 walipata ushauri na 164 walipata elimu ya kisheria.

### **iii) Kuunda Kamati za Uratibu wa Msaada wa Kisheria**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulibainisha kuwa, kwa kupitia Sheria ya Msaada wa Kisheria na Kanuni zake, Wizara ya Katiba na Sheria imefanikiwa kuunda Kamati za Uratibu za Msaada wa Kisheria (*Inter-Agency Legal Aid Co-ordination Committee*) katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara kwa lengo la kuleta ufanisi katika huduma kwa kushirikisha wadau wote muhimu. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, Mikoa ambayo kamati hizi za msaada wa kisheria imefanikiwa kuundwa katika Tanzania Bara ni pamoja na Mkoa wa Simiyu, Tanga, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Njombe, Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara na Lindi, huku Mikoa mingine ikiwa bado haijafikiwa kutokana na changamoto mbalimbali.

### **iv) Kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa msaada wa kisheria imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wataalamu wanaohusika na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwenye maeneo ya vizuizi na wale wanaolinda na kusimamia ulinzi na usalama

wa mtoto. Watalaamu waliopewa mafunzo ni hawa wafuatao: -

- 1) **Askari Polisi na Askari Magereza:** Wizara ilifanikiwa kuendesha mafunzo kwa askari polisi wapatao 112 na askari magereza wapatao 160. Lengo kuu la mafunzo hayo ilikuwa ni kuwajengea uwezo, ujuzi, maarifa juu ya masuala ya msaada wa kisheria katika maeneo ya vizuizi. Maafisa hawa wameteuliwa kuwa Maafisa wa Dawati la Msaada wa Kisheria la Jeshi la Polisi na Magereza. Aidha, Wizara pia iliwapatia mafunzo maafisa 15 wa Jeshi la Polisi na 17 wa Jeshi la Magereza juu ya mbinu wezeshi za kusaidia watoto na kutoa huduma bora za msaada wa kisheria kwa watoto waliokinzana na waliokutana na sheria.
- 2) **Wasajili Wasaidizi:** Hawa ni Maafisa Maendeleo ya Jamii wa mikoa, wilaya na halmashauri ambao walipatiwa mafunzo ya namna ya kusimamia na kuratibu masuala ya msaada wa kisheria kwenye mikoa, wilaya na halmashauri zote nchini. Mpaka sasa kuna Wasajili Wasaidizi wapatao 209 walioteuliwa kwa Tangazo la Serikali Na. 215 la Februari, 2018 ambao wapo katika Ofisi za Sekretarieti za Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini. Wasajili hawa walipatiwa pia mafunzo ya kuwajengea uwezo ili waweze kuwaratibu kwa ufanisi watoa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yao;
- 3) **Wasaidizi wa Kisheria:** Jumla ya wasaidizi wa kisheria wapatao 2798 wamepatiwa mafunzo ya msaada wa kisheria kupitia mtaala ulioandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau wa huduma ya msaada wa kisheria. Mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi wa wasaidizi wa kisheria katika kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii; na
- 4) **Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria:** Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria Walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili waweze kutoa huduma hiyo ya msaada wa kisheria kwa watoto waliokinzana na waliokutana na sheria katika maeneo yao.

v) **Kuanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria Mahakamani**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, Serikali imeanza mchakato wa kuanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria kwenye Mahakama za Mwanzo mpaka Mahakama Kuu. Lengo ni kuhakikisha Huduma ya Msaada wa Kisheria inapatikana mahakamani.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na wadau wa msaada wa kisheria wakiwemo Mahakama ya Tanzania wameanza mchakato huo kwa kuanzisha madawati hayo kwenye mahakama ya mfano kama ile Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Kituo Jumuishi cha utoaji Haki Kinondoni 8 na Mahakama Jumuishi katika Wilaya ya Temeke. Tayari wanasheria wapatao 15 wamepatiwa mafunzo elekezi na Mahakama kwa ajili ya kazi hiyo. Maafisa hawa watafanaya kazi katika Mahakama hizi sita. Pia Mahakama imeteua Maafisa ambao watafanya kazi pamoja na watoa huduma katika Madawati hayo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo za mafanikio, Kamati iliweza kubaini changamoto ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi zaidi katika usimamizi na utekeleaji wa Sheria hiyo. Baadhi ya Changamoto hizo ni:-

1) Kuwepo kwa uchache wa watoa huduma ya Msaada wa Kisheria nchini ikilinganishwa na idadi ya watanzania wanaohitaji msaada wa kisheria;

2) Watoa huduma ya Msaada wa Kisheria waliopo, hususan wasaidizi wa kisheria, kutokuwa na bajeti za kutosha kuendesha shughuli zao;

3) Huduma ya Msaada wa kisheria kutegemea sana bajeti za wahisani ambazo sio endelevu kutekeleza majukumu ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- 4) Vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwemo kutozingatiwa kwa haki za makundi maalumu hususani wanawake na watoto, kuendelea kuongezeka kutoka na mfumo dume wa mila na tamaduni za baadhi ya maeneo nchini na hivyo kuibuka kwa migogoro mbalimbali katika jamii ambayo hupelekea uvunjifu wa haki; na
- 5) Wananchi kutotambua hatua za kisheria za kuchukua wanapokabiliana na changamoto ya kisheria kutockana na kutokuwa na elimu ya kutosha katika masuala ya kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, Kamati ilitoa ushauri **kwa** Serikali kama ilivyoainishwa katika SEHEMU YA TATU ya taarifa hii.

### **H. Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Mpango Mkakati wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa kuanzisha Ofisi zake kwa kila Wilaya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa Haki Jinai kwa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilianzishwa kwa Hati Idhini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 2018 liliofanya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi huru na inayojitegemea. Uchambuzi wa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo, umebaini kuwa, tangu kuanzishwa kwake, Ofisi hiyo imetekeleza yafuatayo: -

#### **1) Mkakati Wa Kuanzisha Ofisi za Mashtaka za Mikoa na Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, mpango mkakati ulibainisha kuwa, ili kutekeleza jukumu la kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka ya Jinai sanjari na utekelezaji wa majukumu yote ya msingi na ya Kikatiba, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilitakiwa, kwa mujibu wa uanzishwaji wake iwe imefungua ofisi za mashtaka katika Mikoa na Wilaya zote zilizopo Tanzania Bara ndani ya kipindi cha miaka mitatu

tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018, ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

**2) Kuratibu uanzishaji wa Ofisi za Taifa ya Mashtaka katika ngazi za Mikoa na Wilaya**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia Oktoba, 2021 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefanikisha uanzishwaji wa Ofisi katika mikoa yote IShirini na Sita (26) iliyopo Tanzania Bara, vilevile imeongeza mikoa mingine mitatu ya kimashtaka katika mkoa wa Dar es salaam ambapo awali ilikuwa ni ofisi za mashtaka za wilaya. Mikoa hiyo ya kimashtaka ilioanzishwa ni Ilala, Temeke na Kinondoni.

Aidha, kwa upande wa Ofisi za Wilaya, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021, ofisi imefanikisha uanzishwaji wa ofisi katika wilaya kumi na nne (14) ambazo ni; Monduli, Nzega, Chato, Tarime, Illemela, Kigamboni, Kondo, Korogwe, Serengeti, Kahama, Mufindi, Karagwe, Kilombero na Ubungo. Hivyo mashtaka katika wilaya hizo yanaendeshwa na Mawakili wa Serikali.

Pia, pamoja na kukosekana kwa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, zoezi hili la kufungua Ofisi za mikoa na wilaya limeendelea kwa kuanzia majengo ya kupanga na kupeleka watumishi wakuanzia pamoja na vitendea kazi vya kuanzia.

**3) Kuratibu uandaaji wa miongozo inayohusu upelelezi na uendeshaji wa mashtaka.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, jukumu hili limikuwa likitekelezwa hatua kwa hatua ambapo miongozo mbalimbali imekuwa ikitolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka, ambayo ni pamoja na Mwongozo Kuhusu Utaratibu Mpya wa Ufunguaji wa Kesi za Jinai GN.296/2012, Mwongozo wa Kufungua na Kuendesha Mashtaka Wakati wa Wimbi la Ugonjwa wa UVIKO 19, Mwongozo Na.1 wa Uendeshaji Mashauri ya Wanyamapori na Misitu wa 2018, Waraka wa Mkurugenzi wa Mashtaka Na.1 wa mwaka 2021 kuhusu

ushughulikiaji na usimamizi wa masuala ya haki jinai na miongozo ya kutembelea magereza na ‘*Plea Bargain*’ iko mbioni kutolewa.

#### 4) Changamoto zilizobainika

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo za mafanikio, Kamati iliweza kubaini **changamoto** ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi zaidi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kamati imebaini kuwa, agizo la kutungwa kwa Sheria ya kusimamia mfumo wa uendeshaji wa mashtaka nchini halikuwa limeenda sambamba na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wake. Utekelezaji ulitegemea sana fedha za matumizi ya kawaida (OC), ambazo hazikuweza kukidhi mahitaji kwani baadhi ya kazi za mpango wa kutenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka zillikuwa na asili ya shughuli za maendeleo kama vile kazi za ujenzi wa ofisi, ununuzi wa vitendea kazi kama vile magari, Kompyuta, Samani za ofisi na usimikaji wa mfumo wa kieletroniki, hali ambayo bajeti ya Matumizi Mengineyo (OC) imeshindwa kukidhi mahitaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, kutokana na kasi ya uboreshwaji wa huduma za Mahakama nchini, mahitaji halisi ya fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka ni **Takribani Shillingi Bilioni 45**, na mtiririko (trend) wa bajeti inayotolewa kwa miaka minne (4) ni wastani wa **Shillingi Bilioni 8.2**.

Hivyo, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka kwa kuanzisha Ofisi za Mashtaka mikoa 29 na wilaya 14, kumekuwa na changamoto ambazo zimekuwa zikirudisha nyuma juhudzi za Serikali za kusogezza huduma za mashtaka ya jinai kwa wananchi kama ifuatavyo:

##### a) Upungufu Mkubwa wa Rasilimali fedha/Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, Ofisi imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali fedha katika

kutekeleza jukumu kubwa la kuendesha mashtaka na kuratibu upelelezi kwa vyombo vya upelelezi kama vile Polisi, Jeshi la Uhamiajji, TAKUKURU, TANAPA, Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa, ambavyo vipo Mikoa na Wilaya zote nchini. Kwa hiyo, kibajeti Ofisi imekuwa ikipewa Ukomo Mdogo wa Bajeti ikilinganishwa na aina na ukubwa wa majukumu ya Usimamizi na Uratibu iliyonayo, ambapo ukomo huo wa bajeti hauakisi hali halisi ya mahitaji ya Ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, Ofisi imekuwa ikipokea mgao wa Matumizi Mengineyo (OC) wastani wa shilingi 753,000,000 kwa mwezi, Kiasi hiki ni kidogo na hakiwezi kutosheleza kuwezesha utekelezaji kwa ufanisi majukumu mbalimbali yaliyopo **katika** ngazi zote za Ofisi ya Mashtaka ambazo ni Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi za Mashtaka za Mikoa 29, Ofisi za Mashtaka za Wilaya 14 na uratibu upelelezi na mashtaka katika wilaya 125 ambazo bado Ofisi za Mashtaka hazijafunguliwa.

Aidha, kukosekana kwa fedha za kutosha kumesababisha kushindwa kufungua Ofisi za Mashtaka kwa wilaya zilizosalia, vilevile kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu muhimu ikiwemo kufanya ukaguzi wa magereza, sehemu wanapozuiliwa wahalifu (Lockups) na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa ofisi za mikoa na wilaya, ili kupima utendaji kazi wa watumishi na kupatia ufumbuzi changamoto zinazojiteza huko. Wakati mwingine mawakili wamekuwa wakishindwa au kuahirisha ufanyakaji wa vikao mbalimbali vya Mahakama Kuu na hivyo kushindwa kuendana na kasi ya wadau wengine katika kuhakikisha kesi zinamalizika kwa wakati mahakamani.

Hivyo, ili kutoqwamisha vikao vya Mahakama, wakati mwingine Mawakili wa Serikali wanalazimika kufanya safari pasipo malipo ili waweze kwenda kuendesha vikao vya Mahakama Kuu.

**b) Kukosekana kwa Majengo ya Ofisi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, pamoja na ukweli kwamba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imekuwepo tangu

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Uhuru wa Nchi hii, Ofisi hiyo haijawahi kujenga ofisi zake katika ngazi zote kuanzia Makao Makuu, Mikoa na Wilaya. Katika mikoa na wilaya zote zilipoanzishwa ofisi za mashtaka zipo kwenye majengo ya kupanga ama kuazimwa isipokuwa kwa wilaya moja ya Serengeti ambapo jengo la Ofisi ya Mashtaka ya Wilaya limejengwa na wadau wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa majengo ya ofisi kunaleta athari zifuatazo: -

- i) Kupunguza uwezo wa Mkurugenzi wa Mashtaka wa kuboresha huduma za uendeshaji wa kesi, ununuzi wa vifaa, na mafunzo kwa watumishi jambo linalopunguza ufanisi kwa watumishi katika kutekeleza majukumu yao;
- ii) Kuwepo lwa ghamama kubwa kwa ajili ya kulipa pango ambapo fedha hizo zingetumika kwa ajili ya shughuli nyingine za kiofisi. OTM inatumia wastani wa shilingi billion 1.5 kwa ajili ya kulipa pango la ofisi zote kwa mwaka; na
- iii) Malengo ya kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa mashtaka na upeletelezi kwa kueneza dhana ya civilianization katika mikoa na wilaya yanaelekea kutokufikiwa kwa wakati.

### c) Upungufu wa watumishi

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, upanuzi wa majukumu ya Ofisi ya Mashtaka ulipaswa uende sambamba na ongezeko la mahitaji ya watumishi na vitendea kazi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, Ofisi imekuwa na idadi ndogo ya watumishi ambapo inakadiliwa kuwa na upungufu wa asilimia 89, idadi hii ndogo haiendani na uzito wa kazi ambapo katika baadhi ya maeneo kuna Mahakama zenye mahakimu wengi kuliko idadi ya Mawakili wa Serikali inayohitajika ili kuwezesha huduma katika mahakama hizo kutolewa kwa ufanisi na hivyo kulazimisha watumishi kufanya kazi kwa muda mrefu pasipo kupumzika.

**Mheshimiwa Spika**, mfano halisi ni kuwa, taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ilibainisha kuwa, idadi ya mawakili wa

Serikali waliopo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni 386, ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka, Naibu Mkurugenzi na wakuu wa divisheni za kisekta, ambapo mawakili hawa huendesha mashtaka katika Mahakama ya Rufani yenyeye jumla ya Majaji 24, Mahakama Kuu yenyeye jumla ya majaji 84, Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya, na kwa sasa Mahakama za mwanzo, baada ya kupitishwa sheria inayoruhusu mawakili kuendesha kesi katika mahakama za mwanzo, zenyeye jumla ya Mahakimu 1117.

Aidha, uchache wa Mawakili wa Serikali kumesababisha maeneo mengi nchini kuendelea kuwatumia maofisa kutoka vyombo vyatupu au Uchunguzi kufanya kazi za Waendesha Mashtaka na hivyo kuathiri dhana ya utenganishaji shughuli za upelelezi na mashtaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, pamoja na Juhudi za Ofisi kutafuta mawakili ambao wapo kwenye Utumishi wa Umma ili waweze kuhamia katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, mawakili wengi wanakataa kuijunga na Ofisi yetu kwa kigezo kuwa Ofisi inafanya kazi zenyeye mazingira hatarishi ambayo hayatoi motisha kwa watumishi kufanya kazi ukilinganisha na taasisi wanazofanya kazi.

**d) Uhaba wa magari na vitendea kazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, katika ofisi za mikoa na wilaya zinakabiliwa na uhaba wa vyombo vyatupu usafiri kwa ajili ya safari za kwenda mahakamani, kuratibu upelelezi na kufanya ukaguzi wa magereza na vituo vyatupu polisi. Sambamba na hili watendaji katika ofisi hizi wamekuwa wakikabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za kila siku za kiofisi.

**e) Kutokuwa na Mfumo wa Kieletroniki kwa ajili ya Uratibu wa Uendeshaji wa Mashtaka**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, kutokana na hali ya sasa kuna uhitaji mkubwa wa matumizi ya teknolojia kutokana na uhaba wa fedha, hivyo ofisi haijaanza kutumia

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mfumo wa Usimamizi wa Kesi kwa njia ya kieletroniki (Case Management Information System - CMIS).

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, kutokutumika kwa mfumo wa kieletroniki kunapunguza ufanisi utekelezaji wa majukumu ya ofisi hasa katika kipindi hiki ambacho wadau wetu wakubwa ambao ni Mahakama wanatumia mifumo ya kieletroniki katika usajili na usikilizaji wa kesi.

### **f) Kutohuwa na Motisha na mazingira hatarishi ya kazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, kutokuwepo motisha wa kipekee kwa **watumishi** kutokana na mazingira magumu ya utendaji kazi na hivyo kusababisha watumishi kuhama au kuacha kazi.

Aidha, Kamati imebaini kuwa, Watumishi waliopo chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamekuwa wakifanya kazi ngumu na ya hatari kwa kuendesha mashauri yenyе mvuto na yanayohusisha watu hatari na wenye fedha. Baadhi ya mashauri hayo ni ya uharamia, ugaidi, ujambazi, dawa za kulevyaa na ujisadi. Hali hiyo imewafanya kuwa katika mazingira hatarishi ilihali wakiishi katika makazi wanayoishi wahalifu au ndugu zao.

Pia, mbali na kuwa katika mazingira hatarishi, maslahi duni kwa Mawakili wa Serikali yamekuwa yakiwafanya Mawakili wengi wazuri na wenye uzoefu kuacha kazi na kukimbilia taasisi nyingine za Serikali au binafsi ambako wanapata maslahi mazuri. Kutokana na mawakili wengi wazoefu kuacha kazi, ofisi imeendelea kuwa na mawakili wapya ambao wanajifunza na wengi wao hawawezi kumudu changamoto za mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, hali hii inasababisha Serikali kuendelea kupoteza kesi hata zile ilizostahili kushinda.

**g) Kukosekana kwa mafunzo katika maeneo mapya ya sheria**

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka ya hivi karibuni maeneo mapya ya sheria yameibuka sambamba na maendeleo ya Sayansi na Technologia. Maeneo hayo ni kama vile wizi wa kutumia komputa (cybercrime), ugaidi, uharamia wa Baharini (piracy), utakatishaji wa fedha (money laundering), utaifishaji wa zana na mazalia ya jinai (recovery of proceeds and instrumentalities of crime) na mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, uendeshaji wa kesi za namna hiyo ni lazima mwendesha mashtaka apewe mafunzo stahiki kuwezesha kupata matokeo chanya. Hii ni kwa sababu mbinu zinazotumika katika kutenda makosa hayo ni za hali ya juu na zinataka mtu mwenye uelewa ili kuthibitisha mashtaka. Hata makosa yaliyo zoleleka, sasa watuhumiwa kwa kushirikiana na wenzao kutoka nje ya nchi wamebuni na wanatumia mbinu za hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ukweli huo, Kamati imejiridhisha pasipo shaka kuwa, Ofisi ya Mashtaka inashindwa kuwapatia mafunzo ya kutosha mawakili wake kutokana na ufinyu wa bajeti na kutokuwepo kwa kituo cha mafunzo kwa ajili ya waendesa mashtaka. Kwa kuwa wahalifu wanaendelea kubuni mbinu mpya za kutenda uhalifu na kwa kuwa kila wakati makosa mapya yanaibuka, maoni ya Kamati ni kuwa, ni vema watumishi wa Serikali wakajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo stahili ya nadharia na vitendo. Mafunzo kwa watumishi yatawawezesha kuendesha kesi kwa umahiri na hatimaye kufanikisha kutiwa hatiani kwa wahalifu.

**h) Kutokuwepo Kwa Bajeti Maalumu kwa ajili ya Programu ya Kutenganisha Kazi za Upelelezi na Mashtaka**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, programu ya kutenganisha mashtaka na upelelezi inajumuisha uratibu wa taasisi kadhaa ikiwa ni pamoja na majukumu ya aina mbalimbali. Hii ni programu kubwa ambayo utekelezaji wake unayo malengo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ambayo yote yanahitaji kuwa

na fedha za ziada kutokana na upanuzi wa huduma za ofisi katika meneo mapya ya kiutendaji kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, utekelezaji wa majukumu mbalimbali yaliyo chini ya programu hii umekuwa ukitegemea zaidi fedha kutokana na bajeti ya matumizi mengineyo (OC). Utetegemezi wa chanzo hiki imekuwa na matatizo na kutokutoshereza hata kwa kulipia mahitaji yale ya msingi ya uendeshaji wa ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika **SEHEMU YA TATU** ya taarifa hii.

## 2.2.2 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Jumla ya Miswada Sita (6), ambayo ilichambuliwa na kujadiliwa na Kamati na hatimaye kupidishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoainishwa katika sehemu ya kwanza ya taaarifa hii, kwa ujumla, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Miswada hii illikusudia kufanya marekebisho katika **Sheria Hamsini na Nane (58)** kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, ili Sheria hizo ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika Sekta zinazo husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilitekeleza wajibu wake wa kikanuni kwa uaminifu, weledi na ufanisi mkubwa katika kulisaidia Bunge kutunga Sheria jumuishi kupitia Miswada iliyohusika. Aidha, Kamati iliwashirikisha Wadau kutoka taasisi na maeneo mbalimbali nichini wakati wa kutekeleza jukumu la Uchambuzi wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakushukuru wewe binafsi na Uongozi wako kwa ujumla, kwa kuendelea kuthamini na

kutambua nafasi ya Kamati hii katika jukumu la kushughulikia Miswada ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, kama moja ya Majukumu yake ya msingi. Kwasababu hiyo, Kamati inajivunia kuwa sehemu ya Mabadiliko makubwa ya Kisheria nchini yanayoendelea kutekelezwa na Serikali katika Sekta mbalimbali nchini, kupitia Bunge lako Tukufu, kwa maendeleo ya Taifa letu.

### **2.2.3 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Wizara ambazo Kamati inazisimamia kwa Kipindi cha Julai hadi Disemba, 2021**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Kipindi cha Nusu Mwaka, kuanzia Julai hadi Disemba, 2021 katika vikao vilivyofanyika Februari, 2022. Sehemu hii inaelezea kwa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa bajeti kwa Mafungu 14 ya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati kama ifuatavyo: -

#### **a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) - FUNGU 26 na 31**

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 26 (Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais) liliidhinishiwa **shilingi biliioni 8.71** ikiwa ni fedha za matumizi ya Kawaida ambapo hadi kufikia Disemba, 2021 Ofisi hiyo ilikuwa imepokea **shilingi biliioni 5.85** sawa na **asilimia 53.3** ya fedha iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 31 (Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira) liliidhinishiwa **shilingi biliioni 7.14** kama fedha ya Matumizi ya Kawaida, na **shilingi biliioni 3.88** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba, 2021 Fungu hilo ilipokea **shilingi biliioni 3.45** sawa na asilimia 48.3 ya Fedha za Matumizi ya Kawaida, na shilingi **milioni 120.089** sawa na **asilimia tatu** tu ya fedha za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, fedha zilizopokelelewa zilitekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwemo uratibu wa Masuala ya Muungano Pamoja na Usimamizi wa Hifadhi ya Maizingira hapa nchini.

b) Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii inajumuisha mafungu manne (4) ambayo ni **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu, **Fungu 27** – Msajili wa Vyama vya siasa, **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi hii pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 57.81** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo hadi kufikia Disemba, 2021 **shilingi bilioni 37.40** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 72.5** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bajeti ya Maendeleo, Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 9.52**. Kati ya hizo, **shilingi bilioni 3.52** ni fedha za nje na **shilingi bilioni 6** ni fedha za ndani. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na ifuatayo: -

- **Mradi wa Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu Mlimwa, Dodoma:** ambapo kazi iliyofanyika ni pamoja na ukamilishaji wa miundombinu ya uzio unaozunguka makazi hayo.
- **Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha uchapaji Nyaraka za Serikali:** ambapo Kamati ilitaarifiwa kwamba, kazi iliyofanyika ni kukamilika kwa michoro ya kiwanda na kumpata Mshauri Mwelekezi. Aidha, Ofisi inatarajia kuanza ujenzi mwezi Februari, 2022.
- **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dodoma:** amabpoa Kamati ilitaarifiwa kwamba ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2022 baada ya kukamilika kwa micho na kupata mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia Disemba, 2021 Ofisi hii ilikuwa imepokea **shilingi milioni 453.67** tu kati ya fedha yote ya maendeleo iliyoidhinishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 4.76**. Kamati ilibaini pia, kati ya fedha hizo, hakuna fedha ya nje iliyopokelewa kufikia Disemba, 2021.

c) Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu)

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ina mafungu mawili ambayo ni **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu pamoja na **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Hadi kufikia Disemba, 2021 Fungu 15 ilipokea **shilingi bilioni 1.93** kati ya **shilingi bilioni 3.87** ya Fedha Matumizi ya Kawaida ikiwa ni sawa na **asilimia 49.87** ya fedha iliyoidhinishwa. Fungu 65 liliidhinishiwa **shilingi bilioni 13.67** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo hadi kufikia Didemba, 2021 **shilingi bilioni 7.12** ilipokelewa ikiwa ni sawa na **asilimia 52.08**. Kamati ilitaarifiwa kwamba Fedha iliypokelewa na Ofisi hii na taasisi zake ilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali za uratibu, huduma, usimamizi na tathmini ya masuala mbalimbali ya kisera.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Fungu 65 liliidhinishwa jumla ya **shilingi bilioni 11.81 mabapo kati ya hizo shilingi bilioni 10** ni fedha za ili wa miradi ifuatayo:-

- Programu ya kukuza kazi za staha
- Programu ya kukuza ujuzi nchini
- Programu ya maendeleo ya vijana

Hadi kufikia Disemba, 2021 Fungu 65 illiliwa limepokea **shilingi bilioni 6.20** sawa na **asilimia 52.56** ya fedha iliyoitengwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla wake, Kamati imeridhishwa inaipongeza Serikali kwa upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo hasa ukizingatia kuwa miradi hiyo inalenga nguvu kazi ya taifa yaani vijana.

d) **Wizara ya Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai hadi Disemba,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

2021, ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake zilizoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake, iliidhinishiwa na Bunge **Shilingi bilioni 178.77** ikiwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Desemba, 2021 Wizara pamoja na Taasisi zake zilipokea kiasi cha **Shilingi bilioni 90.83** ikiwa ni sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishiwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa upande wa Miradi ya maendeleo, Bunge iliidhinishia Wizara pamoja na taasisi zake jumla ya **Shilingi bilioni 52.91** ambapo hadi kufikia Disemba, 2021 Wizara Pamoja na taasisi zake ziliikuwa zimepokea kiasi cha **shilingi bilioni 16.18** sawa na takriban **asilimia 30.58** ya fedha iliyoidhinishiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa tathmini ya Kamati, utekelezaji wa bajeti za Wizara ni wa kuridhisha kwa kuwa sehemu kubwa fedha iliyokuwa imeidhinishiwa ilipokelewa kwa kadri ilivyotaraijiwa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo na mwenendo usiordhisha kwa upande wa fedha iliyotengwa kwa Miradi ya Maendeleo ambapo hadi kufikia nusu mwaka, mapokezi yalikuwa **chini ya asilimia hamsini**.

### 2.2.4 Semina na Mafunzo

**Mheshimiwa Spika**, katika Kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipatiwa Semina na mafunzo kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge, kwa ajili ya kuijengea Kamati uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria hususan masuala ya msingi katika hatua za Uchambuzi wa Miswada. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo: -

- a) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa Legislative Support Program (LSP II)
- b) TWAVEZA
- c) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

d) Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS)

Aidha, kwa kibali chako, Ofisi ya Waziri Mkuu walitoa mafunzo ya Semina mbalimbali kuhusu masuala mbalimbali ya kisera, kisheria, Muundo na Majukumu ya Ofisi hizo kwa kuzingatia majukumu mapya ya Uwekezaji yaliyoongezwa.

Vile vile, Wizara ya Katiba na Sheria kupitia taasisi zilizo chini yake ikiwemo Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na RITA walitoa mafunzo kuhusu masuala ya Kisera, kisheria na Kitaasisi kwa lengo la kuiwezesha Kamati kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kushauri ipasavyo ili kuongeza ufanisi zaidi kwa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe na Sekretarieti yake wamejengewa uwezo na uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisera na kisheria na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuishauri Serikali ipasavyo.

**2.2.5 Mazingira Wezeshi ya Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitembelea Miradi mbalimbali ya Vijana na Watu Wenye ulemavu katika Wilaya za Mkoa wa Singida kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa kwa jinsi ambavyo vijana pamoja na makundi yenye mahitaji maalum wananaufaika na utekelezaji wa Miradi hiyo kupitia vikundi mbalimbali nya uzalishaji.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

**3.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika sehemu hii Kamati imezingatia masuala mbalimbali ya kiuchambuzi ili kuweza kuishauri

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Serikali kwa ujumla wake, na kwa wizara mahsusili kuboresha utendaji wa wizara hizo na taasisi zilizo za chini yake. Maoni na mapendekezo haya yakikubaliwa na Bunge lako yatakuwa maazimio kamili ili Serikali iyafanyie kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

### **Ofisi ya Waziri Mkuu**

#### **3.2 Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2014**

**KWA KUWA**, imebainika kuwepo uelewa na ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika Halmashauri zetu nchini, kuhusu mfumo wa usimamizi na udhibiti wa Maafa katika ngazi za Kata, tarafa na Wilaya, kwa mujibu wa Sheria;

**NA KWA KUWA**, ombwe la uelewa na ushirikishwaji wa wananchi katika kudhibiti maafa yanayotokea kwenye maeneo yao unaathiri utekelezaji wa Sheria ya Maafa kwa kiwango kilichokusudiwa;

**HIVYO BASI**; Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- i) Ione umuhimu wa kuandaa mfumo wa utoaji elimu ya udhibiti wa Maafa kama sehemu ya masomo kuanzia Elimu ya Msingi kutokana na ongezeko kubwa la madhara ya mabadiliko ya tabia nchi;
- ii) Kuandaliwe mkakati endelevu wa udhibiti wa maafa na madhara yake katika visiwa vya Zanzibar kwa kuwa hili ni suala la Muungano na kwa hasa kwa kuzingatia Jiografia ya Kisiwa hicho;
- iii) Kamati za Usimamizi wa Maafa pamoja na Mamlaka za Halmashauri zetu zijengewe uwezo wa mara kwa mara kuhusu namna bora ya kudhibiti na kusimamia maafa kwenye maeneo yao kwa lengo la kupunguza sintofahamu pale panapotokea maafa kwenye maeneo yao;
- iv) Kuandaliwe mpango wa utoaji Elimu ya Mazingira na tabia nchi na kwa lengo la kuielimisha Jamii ili kila Mwananchi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

atambue wajibu wake katika udhibiti wa maafa kabla na baada ya kutokea;

v) lone umuhimu wa kuifanyia marekebisho Sheria hii ili Wabunge wawe sehemu ya Wajumbe wa Kamati za Maafa katika Ngazi ya Wilaya na Mikoa; na

vi) lone umuhimu wa kuwa na Mfuko Maalum wa Usimamizi, na udhibiti wa Maafa chini ya OWM, kwa lengo la kuwa na Bajeti ya Uratibu wa masuala ya maafa hasa yale ambayo yana athari Kitaifa.

### **3.3 Utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi ya Mwaka 2003 chini ya OSHA**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa, OSHA inakabiliwa na changamoto ya Watumishi, ambapo ina watumishi 70 tu badala ya watumishi 136 wanaohitajika kwa sasa, pamoja na kuwepo kwa uelewa mdogo wa Masuala ya Usalama na Afya mionganoni mwa wadau;

**NA KWA KUWA,** uwepo wa changamoto hizo unaathiri utekelezaji wa Sheria ya OSHA na Kanuni zake kwa ufanisi zaidi;

**HIVYO BASI,** Kamati inashauri kuwa:-

i) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ishirikiane na Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa lengo la kuhakikisha kuwa, tatizo la upungufu wa Watumishi linatatuliwa haraka ili kuongeza ufanisi wa Wakala huu kwa kupatiwa Vibali vyta kuwaajiri idadi ya Watumishi wanaohitajika na wenye sifa stahiki;

ii) OSHA iandae mpango Mkakati wa kushirikisha Sekta isiyo rasmi katika kutambua masuala ya Afya na Usalama mahali pa kazi, kwa kushirikiana na wadau wengine katika kuwajengea uwezo. Aidha, utekelezaji wa mpango mkakati huo ulenge kuleta tija endelevu itakayopelekea kuitambua

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Sekta hiyo chini ya Sheria ya OSHA, yene kubeba kundi kubwa la Vijana na Wanawake wengi nchini ambao wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika Maendeleo ya Uchumi wa nchi; na

iii) OSHA iandae mpango endelevu na iutengee bajeti ya usimamizi, ambao utalenga kuwahamasisha wadau wake kuhusu kujikinga na kukabiliana na Magonjwa ya mlipuko kama UVIKO-19 kwa lengo la kuimarisha na kulinda afya za Wafanyakazi nchini;

**3.4 Ufanisi wa Shughuli za Kiwanda cha Viatu na bidhaa za Ngozi kinachomilikiwa kwa ubia na Jeshi la Magereza na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, mradi huu unaweza kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa soko la bidhaa za ngozi zinazotokana na Mifugo yetu ya ndani na hivyo kuongeza kipato cha uhakika kwa Wafugaji wetu;

**NA KWA KUWA**, ili mradi huo ufikie ufanisi huo, kunahitajika uhakika wa bidhaa zenyetukidhi hadhi ya ubora kwa ajili ya kupanya ushindani wa soko kwa ndani na nje ya nchi;

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuratibu utekelezaji wa yafuatayo:-

i) Soko la wanunuzi wa bidhaa za Kiwanda lipanuliwe kwa ndani na nje ya chini, kwa kuwa na Mawakala (Agents) wa bidhaa kwenye kila Mkoa bila kusahau Zanzibar ambako imebainika ni wanunuzi wa bidhaa halisi za ngozi kwa kiwango kikubwa;

ii) Ushirikiano uliopo wa Wadau wa Sekta ndani ya Serikali uimarishwe zaidi na uwe enedelevu baina ya Menejimenti ya Kiwanda, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara pamoja na taasisi zingine za Serikali ili kurahisisha upatikanaji wa mali ghafi,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kupunguza ghamama za uwekezaji lakini pia urahisishwaji wa upatikanaji masoko mionganoni mwa taasisi za Serikali;

iii) Serikali ione umuhimu (bila kuathiri soko la ushindani) wa kuhakikisha ina kisaidia Kiwanda kuwa na mtandao wa Soko endelevu la kusambaza mahitaji ya bidhaa za ngozi kwenye taasisi za umma(Majeshini, Shule za Serikali na Vyuo vya Serikali), ikiwemo kuwahamasisha Watumishi wa Serikali ambao ndiyo wawekezaji wa mradi huu, wawe wateja wa kudumu wa bidhaa za kiwanda chao;

iv) Menejimenti ihakikishe, inaboresha muonekano wa bidhaa za Viatu na bidhaa zingine zinazotokana na kiwanda hicho, ikiwa ni pamoja na kutathmini bei ya soko ili kuwezesha bidhaa hizo kupenya ushindani wa Soko la bidhaa zingine kutoka ndani na nje ya nchi; na

v) Ofisi ya Waziri Mkuu iandae utaratibu ambao utahakikisha kila Bunge la Bajeti la kila Mwaka, Menejimenti ya Kiwanda inakuwa na Banda la ndani katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutangaza bidhaa za kiwanda kwa Wabunge ambao watasaidia kutangaza bidhaa hizo kwa Wananchi kwenye maeneo yao. Aidha, hatua hiyo itatoa fursa kwa Wabunge, Wafanyakazi wa Bunge na Wananchi kununua bidhaa za ngozi zinazotengenezwa na Kiwanda hiki kwa bei nafuu. Pia, hatua hiyo iende sambamba na matumizi ya Maonyesho ya Sabasaba na Nane ya kila mwaka kutangaza bidhaa za kiwanda hiki ili wananchi wengi wapate nafasi ya kujua na kununua bidhaa hizo.

### **3.5 Mpango wa kupanua Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa lengo la kuwafikia Vijana wengi zaidi**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini uwepo wa uhitaji mkubwa wa mafunzo ya kukuza ujuzi kutoka kwa vijana ambao hawakupata fursa ya kuendelea na elimu ya juu, kutohakana na hali duni za familia hususan familia za vijijini;

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

**NA KWA KUWA**, Vijana wengi kushindwa kumudu ghamara za kuhudhuria mafunzo, kwasababu ya umbali kutoka wanakoishi vijiji kuja kwenye makao makuu ya Halmashauri kunapoktolera mafunzo hayo;

**NA KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, Serikali imepanga kutumia shilingi Bilioni 550 kwa ajili ya utekelezaji wa program hii kwa kipindi cha miaka mitano (5), ambapo Shilingi Bilioni 102 zimepangwa kutumika kila mwaka wa Fedha, kwa kipindi cha mwaka 2021/22-2025/2026;

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuzingatia yafuatayo:-

- i) Vijana wenge ulemau wajumuishwe kwenye programu hii pamoja na kwenye mkakati wa ajira katika miradi mbalimbali nchini;
- ii) Serikali iandae mfumo rasmi na kuuvekea muongozo kuhusu namna bora ya kuwatambua na kuwaingiza wahitimu na Wanafunzi wa Vyuo vikuu katika programu hii, kwa lengo la kuondoa changamoto kwa vijana wengi kutofikiwa na Programu hii;
- iii) Serikali iandae mwongozo maalum wa kuwapata vijana wengi Vijiini ili wajengewe ujuzi kwa ajili ya usimamizi wa Miradi mbalimbali inayoanzishwa na Serikali Vijiini lakini inakosa usimamizi kwasababu vijiji hivyo havina vijana qwenye ujuzi wa usimamizi wa miradi hiyo;
- iv) Serikali ione umuhimu wa kuendelea kuongeza idadi ya Wasichana kwenye program hii kwa lengo la kuwajengea ujuzi wa kujkwamua kiuchumi;
- v) Serikali ihakikishe inajidhatiti zaidi kwa walau 50% ya mafunzo ya prohgramu hii yawe yanayohusu Kilimo, ili kuleta matokeo chanya kwa Vijana walio wengi wanaoishi vijiji;
- vi) Porgramu hii iambatane pia na mafunzo kwa vijana kuhusu menejimenti ya raslimali fedha kwa uchumi endelevu, pamoja na Elimu ya Uzalendo; na

vii) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, iandae Ziara ya Kikazi ya Kamati kwa ajili ya kutembelea Zanzibar kwenye Vyuo vyenye mafunzo kama haya pamoja na kutembea Ofisi ya SMZ yenye jukumu linalofanana na hili ili Kamati ijifunze na kushauri ipasavyo.

### **3.6 Utekelezaji wa Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni, Sura ya 436**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa, kuanzishwa kwa mfumo mpya wa kielektroniki wa kuratibu Ajira za Wageni kuititia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 ya Mwaka 2021 kumekuwa na mafanikio mengi ya haraka ikiwemo kuongezeka muda wa kufanya kazi nchini kwa raia wa kigeni kutoka miaka 5 hadi 8 ili kuongeza fursa ya kupata ujuzi kwa wazawa, kuongezeka kwa idadi ya Wageni nchini na hivyo kukuza uchumi wan chi; uwiano wa Idadi ya ajira ya Mgeni Mmoja kwa Wazawa 10 utaongeza uwigo wa ajira kwa wazawa; na kuwepo kwa ongezeko la makusanyo ya maduhuli ya Serikali kama ilivyobainishwa kwenye taarifa hii;

**NA KWA KUWA,** matokeo ya utekelezaji wa Sheria hiyo na marekebisho yake utapanua huduma za utekelezaji wa Sheria hiyo kwa lengo la kuongeza mzunguko wa ajira za ndani na nje ya nchi

**HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

i) OWM iimarishe mfumo wa uratibu wa utaratibu wa Watanzania kupata ajira za kawaida nje ya nchi kwa mazingira salama kwa kulinganisha na Nchi jirani zinavyo ratibu ajira kama hizo kwa raia wao hapa nchini

ii) OWM kwa kushirikiana na mamlaka zingine ndani na nje ya nchi iongeze uhakiki na udhibiti wa vyeti na Maadili (integrity) ya Wageni wanaoomba na kupata vibali vyaa kazi au ukaazi hapa nchini;na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

iii) Serikali iongeze jitihada za kupambana na kudhibiti Vishoka wanaoingilia ufanisi wa utekelezaji wa Sheria hii, kwa usalama wa nchi yetu pamoja na usalama wa Wageni wenye nia njema kwa nchi yetu.

### **3.7 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuwa ni kichocheo muhimu cha **maendeleo** ya Vijana nchini kutokana na uratibu mzuri unaotekelizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu;

**NA KWA KUWA**, kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Vijana zaidi ya uwezo wa Mfuko kunaweza kusababisha fursa hiyo isiwafikie Vijana wengi nchini,

**HIVYO BASI**, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

i) Kuona umuhimu wa kuongea Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ili Mfuko huo uweze kuwafikia Vijana wengi zaidi kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kudhihirisha uwezo mkubwa katika uratibu wa mfuko huo;

ii) Ongezeko hilo la Bajeti liiwezeshe Serikali kupanua uwigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kuanza kutoa Mikopo kwa makundi mbalimbali ya Vijana yaliyosajiliwa na yenye mipango ya miradi yenye lengo la kuongeza ajira, CBOs na Makampuni yaliyosajiliwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya Kati na Mikubwa ya kutoa ajira nyingi kwa Vijana, na

iii) Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane kwa ukaribu zaidi na Ofisi ya Rais –TAMISEMI ambao ndiyo wenye dhamana na Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila Halmashauri inawajibika kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana pamoja na **asilimia 4%** za Fedha za Halmashauri, kwa

kusimamia utekelezaji wa Miradhi hiyo na marejesho yake kwa wakati.

**Wizara ya Katiba na Sheria**

**3.8 Utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo kwa ustawi wa Jamii**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii unategemea sana na ushirikiano wa kiutendaji kati ya RITA na NIDA;

**NA KWA KUWA**, ushirikiano wa taasisi hizo pamoja na nyingine za Serikali ni wa umuhimu kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa utoaji wa Vyeti vya kuzaliwa na Vitambulisho vya Taifa kwa Watu ambao hawatakiwi kwa mujibu wa Sheria;

**NA KWA KUWA**, fursa za muingiliano wa Watanzania na Wananchi wa Mataifa mwingine unahitaji umakini katika kuhakisha haki ya utaifa inazingatiwa kwa mujibu wa Sheria za nchi zilizopo kwa sasa;

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

i) Kuhakikisha kunakuwepo ushirikiano wa karibu baina ya mifumo RITA na NIDA ili kuondoa changamoto ya Mtu asiyekuwa Mtanzania kukutwa ana cheti cha kuzaliwa kwa hoja kwamba, aliomba cheti hicho kwasababu alikuwa na cheti cha NIDA;

ii) Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Mamlaka za Ajira Serikalini itatue changamoto ya ukaimishaji wa Watendaji wa RITA kwa muda mrefu kwa kuwa kunaathiri ufanisi wa Taasisi hiyo;

iii) Kuanzishwe mfumo rasmi kisheria na kiusimamizi wa kusimamia taarifa za vizazi na vifo kwa Watanzania walioko

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

nje ya nchi hususan wale ambao bado hawajakana utanzania wao;

iv) RITA iongeze umakini katika utekelezaji wa majukumu yake ili kudhibiti mianya ambayo ikitumiwa vibaya inaweza kutahiri usalama wan chi kwa kiasi kikubwa; na

v) Serikali ianze kujipanga kuanzisha mfumo wa Kibajeti wa gharama za uratibu wa Programu ya usajili wa Matukio ya Binadamu pasipokuendelea kutegemea wadau wa nje ambao wanaweza kutoweka muda wowote.

### **3.9 Utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017; na Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria za Mwaka 2018**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA, Kamati** imebaini uwepo wa idadi ndogo ya watoa huduma ya Msaada wa Kisheria nchini ikililinganishwa na idadi ya watanzania wanaohitaji msaada wa kisheria;

**NA KWA KUWA,** watoa huduma ya Msaada wa Kisheria waliopo, hususan wasaidizi wa kisheria, wamebainika kutokuwa na bajeti za kutosha kuendesha shughuli zao;

**NA KWA KUWA,** Huduma ya Msaada wa kisheria kutegemea sana bajeti za wahisani ambazo sio endelevu kutekeleza majukumu ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

**NA KWA KUWA,** uwepo wa changamoto hizo unaathiri upatikanaji wa huduma ya Msaada wa kisheria kwa Wananchi wengi ambao hawatambui hatua za kisheria za kuchukua wanapokabiliana na changamoto ya kisheria kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha katika masuala ya kisheria;

**HIVYO BASI,** Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza yafuatayo: -

- i) Ione umuhimu wa kuondoa au kupunguza ada ya usajili wa watoa huduma ambao tayari wameshasajiliwa kama AZAKI za kiraia (NGOs) ili kuwapunguzia gharama za utoaji wa huduma hii kwa kuwa inatolewa bure kwa wananchi;
- ii) Ione umuhimu wa kuboresha au kuimarisha Wasajili wa Saidizi ngazi ya Halmashauri ili wawe na uelewa wa kisheria kwa ajili ya kuongeza ushurikiano zaidi baina ya Serikali na Wato Huduma hiyo;
- iii) Ione umuhimu wa kuandaa mpango wa kibajeti wa kuanza kutumia bajeti ya Serikali na Wadau wengine kufadhili shughuli za Watoa huduma ya Msaada wa kisheria Kupitia Mfuko wa Msaada wa Kisheria, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Watoa huduma hao wanawafikia wananchi wengi zaidi hususan wananchi wa vijijini; na
- iv) Wizara kwa kushirikiana na wadau wake iendelee kutoa elimu kwa umma kwa jamii kuhusu haki za makundi hususan wanawake na watoto katika umiliki wa mali kwa njia mbalimbali ikiwemo kurithi, pamoja na haki za makundi hayo katika jamii kwa ujumla wake.

**3.10 Mpango Mkakati wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa kuanzisha Ofisi zake kwa kila Wilaya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa Haki Jinai kwa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, jitihada za kutungwa kwa Sheria ya kusimamia mfumo wa uendeshaji wa mashtaka nchini haikwenda sambamba na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wake;

**NA KWA KUWA**, Utekelezaji wa mpango hio ulitegemea sana fedha za matumizi ya kawaida (OC), ambazo hazikuweza kukidhi mahitaji kwani baadhi ya kazi za mpango wa kutenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka zilikuwa na asili ya shughuli za maendeleo kama vile kazi za ujenzi wa ofisi, ununuzi wa vitendea kazi kama vile magari, Kompyuta, Samani za ofisi na usimikaji wa mfumo wa kieletroniki;

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

**NA KWA KUWA**, hali hiyo ya ufinyu wa bajeti imeshindwa kukidhi mahitaji. Kutohana na kasi ya uboreshwaji wa huduma za Mahakama nchini na hivyo kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa mpango huo;

**HIVYO BASI**, ili kuimarisha na kurahisisha usimamizi wa mifumo ya utoaji haki jinai nchini kwa wakati, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- i) Kuongezwe Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa matumizi ya Mengineyo (OC) na Maendeleo kulingana na maoteo ya Bajeti ya Ofisi ambayo itakadiriwa na kuthibitishwa kama bajeti halisi kwa ustawi wa Ofisi hii;
- ii) Kuwepo na Programu Maalumu ya Ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa na Wilaya kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo au kutumia rasilimali fedha zinazokusanywa na ofisi kwa njia ya utaifishaji au ulipaji wa fidia;
- iii) Kuwepo na program maalumu ya kuongeza rasilimali watu, ambapo Wizara ya Katiba na Sheria iombe kibali cha ajira kwa ajili ya kuajiri watumishi wa kada mbalimbali zenye upungufu mkubwa angalau watumishi 200 kwa kila mwaka kwa kuanzia. Aidha, watumishi waliopo katika ngazi za wilaya wenye sifa za kuwa Mawakili wa Serikali wapewe kipaumbele na kuajiriwa na Ofisi hii ya Mashtaka ili wahudumu katika kuendesha mashtaka katika wilaya husika;
- iv) Motisha na mazingira ya kazi kwa watumishi viboreshwe ambapo, Kamati inapendekeza kuwa, Serikali iweke mkakati maalum wa kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi wa ofisi ya mashtaka kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi na kupunguza idadi ya Mawakili wanaoacha kazi kwa sababu ya maslahi duni;
- v) Kuwepo na programu maalumu ya mafunzo kwa watumishi wa ofisi ya mashtaka Kutoa mafunzo zaidi ndani na nje ya nchi katika maeneo mapya ili kuhakikisha watendaji wanakuwa na weledi wa kuendesha kesi na kuwezesha

kuelekeza upelelezi kufanyika kwa kutumia mbinu mbali za kukabiliana na makosa katika maeneo mapya ya money laundering, ugaidi, uharamia, utaifishaji wa mali zinazohusiana na *uhalifu* (*Asset Forfeiture and Recovery*) na kesi za dawa za kulevyia. Gharama zinazohitajika zitatimika kutoka kwenye bajeti ya Ofisi kama ikiongezewa ukomo kutoka maoteo halisi ya bajeti iliyombwa;

- vi) Kuanzishwe kituo cha mafunzo na utafiti kwa ajili ya waendesa mashtaka (Prosecution Academy), ambapo, Kamati inapendekeza kuwa, Serikali ikubali na ichukue hatua ya kujenga chuo cha waendesa mashtaka (prosecution academy). Chuo hiki kitatumika kwa ajili ya kuwafundisha mawakili na waendesa mashtaka na wadau wa Haki-Jinai walio kazini masuala muhimu yanayohusiana na jinai; na
- vii) Kuanzishwe kwa Mfuko wa Mashtaka (Prosecution Fund), kwa kuzingatia mapendekezo ya ni Kamati kuwa, kwa kuwa shughuli za uendeshaji wa mashtaka ni za kioparesheni ambazo zinahitaji rasilimali fedha kwa wakati, ni vema kukawa na mfuko wa mashtaka (Prosecution Fund) ambaao utatumika kwa ajili ya shughuli zote zinazohusiana na mashtaka. Maoni ya Kamati ninkuwa, chanzo kimojawapo cha mfuko huo ni fedha zinazopatikana kutoekana na mazalia ya uhalifu pamoja wa wadau mbalimbali wa maendeleo. Na mfuko huu utatumika pia katika program Maalumu ya Kutenganisha Kazi za Upelelezi na Mashtaka.

### **3.11 Ufanisi katika Mifumo ya Utoaji Haki nchini;**

**KWA KUWA;** ni jukumu la Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya Sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati;

**NA KWA KUWA;** usimamizi wa utoaji wa haki nchini unategemea sana ufanisi wa Taasisi husika zenye dhamana hiyo;

**HIVYO BASI;** Kamati inaendeleza kuzishauri Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria zinazohusika na usimamizi wa utoaji haki, kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) Mahakama iendelee kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake iliyojiwekea wa kuhakikisha kila Hakimu na Jaji anashughulikia na kukamilisha idadi ya Mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya Wananchi kwa chombo hiki cha utoaji wa haki nchini;
- ii) Serikali iendelee kuboresha Bajeti ya Fungu 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 16 la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 19 la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Fungu 35 la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi; na
- iii) Serikali ione umuhimu wa kuboresha mazingira ya Rasilimali watu chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara na Vitengo vyote vya Sheria kwenye taasisi zote za Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kutokana na mabadiliko makubwa ya mfumo wa Kisheria yaliyotekeliza hivi karibuni kwa mujibu wa Sheria.

### **3.12 Usimamizi wa Misingi ya usawa wa Kijinsia**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, nchi yetu imejengwa katika misingi ya haki na usawa kwa **Watu** wote bila kujali jinsi;

**NA KWA KUWA**, ili tuendelee kudumisha misingi hiyo, ni wajibu wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kuendeleza jitihada za kuhakikisha misingi ya usawa wa Kijinsia inazingatiwa katika Mifumo yote ya utoaji haki nchini, katika migawanyo ya raslimali zilizopo, Elimu na katika migawanyo ya nafasi za madaraka katika taasisi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria;

**NA KWA KUWA**, uzingatiaji wa misingi hiyo ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha maendeleo endelvu yanawafikia Wananchi wote bila kujali tofauti za jinsia zao;

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali kwa kushirkiana na Wizara zote nchini, ihakikisha kuwa, Sheria za nchi zizingatia usawa wa kijinsia katika mifumo yote ya utaoji haki, migawanyo ya raslimali pamoja na Migawanyo ya Madaraka katika vyombo mbalimbali vya utekelezaji nchini;
- ii) Kuhakikisha kuwa, Mtoto wa kike na wa kiume waanaendelea kutambuliwa, kuthaminiwa na kuheshimiwa kwa hadhi sawa katika ngazi zote za Kijamii kuanzia ngazi ya Familia; na
- iii) Elimu ya Usawa wa Kijinsia iendelee kutolewa pasipo kubagua upande wowote wa kijinsia kwa lengo la kuhakikisha Jamii yetu inakuwa na uelewa sawa kwa maendeleo enedelevu ya Taifa letu.

**3.13 Ufanisi katika mwenendo wa Bajeti za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, kumekuwepo ongezeka la upatikanaji wa Fedha za ndani ukilinganisha na upatikanaji usioridhisha wa Fedha za Nje, katika mwenendo wa Bajeti ya Serikali,

**NA KWA KUWA**; hatua hii ya kutumia fedha za ndani kuendeshea mipango ya nchi inapunguza utegemezi wa kiuchumi na ni ya uhakika zaidi,

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri kuwa:-

- i) Serikali iendelee kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika;
- ii) Serikali kupitia vyombo husika, ibuni vyanzo vipya vya mapato vyenye uhakika na endelevu, na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

iii) Elimu ya kulipa Kodi iendelee kutolewa kwa Wananchi ili kila Mtanzania aone umuhimu wa kulipa kodi kwa Maendeleo endelevu ya Taifa letu.

### **3.14 Semina na mafunzo kwa Kamati**

#### **Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Programu ya utekelezaji wa Mradi wa LSP (II) chini ya UNDP, imekuwa msaada mkubwa sana katika kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hii kuhusu masuala mbalimbali katika uchambuzi wa Miswada ya Sheria,

**NA KWA KUWA**, Kamati hii ina jukumu la Kuchambua na kujadili Miswada mingi ya Sheria za Marekebisho ya Sheria mbalimbali ambazo zinagusa Sekta mbalimbali nchini,

**NA KWA KUWA**; bado mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge na Sekretarieti ili kupanua wigo wa uelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao;

**HIVYO BASI**; Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kuona umuhimu wa kuendelea kupanua utekelezaji wa Mradi wa LSP (II) katika Bunge la Kumi na Mbili kwa kuendelea kuwajengea Uwezo Wabunge Wapya na Sekretarieti kuhusu masuala ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, Mikataba na Itifaki za Kimataifa pamoja na Uchambuzi wa Bajeti za Serikali, kwa lengo la kuongeza weledi kwa Wajumbe na Sekretarieti yake.

Hi ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mradi huu wa LSP uwe endelevu kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo yenye tija kwa kuongeza ufanisi zaidi kwa Wabunge na Sekretarieti yake katika kusimamia utendaji wa Serikali na Taasisi zake.

### **3.15 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati**

#### **Mheshimiwa Spika;**

**KWA KUWA**, Bunge lina dhamana kubwa ya kusimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa **Tanzania** ya Mwaka 1977;

**NA KWA KUWA**, katika kutimiza jukumu hili Bunge hutumia Kamati zake ambazo hutoa ushauri, Mapendekezo na maelekezo mbalimbali kwa Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake;

**HIVYO BASI**; Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati na kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri na mapendekezo hayo kila inapotakiwa kufanya hivyo.

## **SEHEMU YA NNE**

### **4.0 HITIMISHO**

#### **4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote. Kwa kutambua mchango wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, naomba niwatambue Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao wamepewa dhamana ya kuongoza wizara mbalimbali zinazosimamiwa na Kamati kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Pindi Chana, Mb – WN OWM (Sera, Bunge na Uratibu)
2. Mhe. Prof. Joyce Ndlichako, Mb – WN OWM (KVAWU)
3. Mhe. Suleiman Jaffo, Mb – WN OMR (Muungano na Mazingira)
4. Mhe. George Simbachawene, Mb – WKS
5. Mhe. Ummy Nderiananga, Mb – NWN OWM (SBU)
6. Mhe. Patrobas Katambi, Mb – NWN OWM (KVAWU)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

7. Mhe. Khamis Khamis, Mb – NWN OMR – (Muungano)
8. Mhe. Geofrey Pinda, Mb – NW KS

**Mheshimiwa Spika**, vilevile nichukue fursa hii kuwashukuru Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya wizara hizi pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer M. Feleshi, (Mb), kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati pale alipohitajika kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha hoja za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya Kisheria. Aidha, Kamati inawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada mbalimbali. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Washauri wa Masuala ya Sheria Bungeni kwa namna bora walivyoshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye kamati ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao: -

1. Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) chini ya Mradi wake wa Legislative Support Program (UNDP – LSP II)
2. Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG)
3. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (Legal and Human Rights Centre) – LHRC
4. Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (Tanganyika Law society) -TLS
5. Tanzania Women Lawyers Association -TAWLA

6. Baraza la Kikristo Tanzania (CCT)
7. TWaweza
8. Tangible Initiative,
9. WILDAF; na
10. Tanzania Network of Legal Aid Providers - TANLAP

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb – Mjumbe
4. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb – Mjumbe
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb – Mjumbe
6. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb – Mjumbe
7. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb – Mjumbe
8. Mhe. Zainabu Athumanji Katimba, Mb – Mjumbe
9. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb – Mjumbe
10. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb – Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb – Mjumbe
12. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb – Mjumbe
13. Mhe. Omar Ali Omar, Mb – Mjumbe
14. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb – Mjumbe
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb – Mjumbe
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb – Mjumbe
18. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb – Mjumbe
20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb – Mjumbe
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb – Mjumbe

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

22. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, ndc kwa uratibu mzuri wa Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2      **Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizotekelizwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli ilizozitekeleza kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa Hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria**

14 Februari 2022

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono na watu wengi sana, ahsante sana kwa taarifa hiyo.

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa; karibu sana. (*Makofi*)

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa hii ya

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022 iingizwe katika Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina lengo la kuliwezesha Bunge katika ufuatilaji wa matokeo ya shughuli za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina sehemu kuu nne kama zilivyoainishwa katika ukurasa wa kwanza hadi wa pili wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambulisha lengo Kuu la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi. Aidha, Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ina jukumu la kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Raís, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelizwa na Kamati katika kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022 ni pamoja na mambo yaliyoainishwa katika ukurasa wa tatu hadi wa nne wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya taarifa inabainisha shughuli zilizotekelizwa na uchambuzi wa matokeo. Katika sehemu hii, Kamati imefafanua shughuli zilizotekelizwa na Kamati na kubainisha mafanikio na changamoto zilizotekelizwa wakati wa utekelezaji kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi; mwezi Machi, 2021, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge na kutembelea baadhi ya miradi iliyotekelizwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; mwezi Machi, 2021, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Shughuli hiyo ilitokana na utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 19 na tarehe 22 Aprili, 2021, Kamati iliwasilisha Bungeni maoni yaliyotokana na shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipokea na kuchambua jumla ya taarifa kumi na tatu kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taarifa sita kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali; mbali na ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa taarifa mbalimbali, Kamati ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika mazingira halisi ya programu na mipango mbalimbali ya Serikali. Kamati iliweza kuainishaa taarifa zilizokuwa zikitolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi ilivyo kwenye maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi wa matokeo hayo kwa kila sekta ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali za Mitaa nchini. Kamati inatambua kuwa Ibara ya 145 ya Katiba

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaanishiwa Serikali za Mitaa na madhumuni yake yametajwa katika Ibara ya 146 ya Katiba.

Kwa mujibu wa Ibara hiyo, Serikali za Mitaa zimeanzishwa ili kupeleka madaraka kwa wananchi. Aidha, vyombo vyta Serikali za Mitaa vimepewa haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umebainisha mafanikio na changamoto mbalimbali. Naomba nilijulishie Bunge lako Tukufu baadhi ya mafanikio na changamoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini umekuwa na manufaa makubwa katika kuboresha utoaji wa huduma ya elimu ya sekondari. Kwa utaratibu huo, mafaniko yaliyopatikana ni pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia ikiwemo kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoongeza mori wa wanafunzi kujifunza na Walimu kufundisha. Hata hivyo, nia hiyo njema ya Serikali kutekeleza mpango mzuri inakabiliwa na changamoto ya wakandarasi kushindwa kumaliza ujenzi kwa wakati. Changamoto hii inachelewesha azma ya Serikali ya kuboresha mazingira ya utoaji huduma ya elimu ya sekondari katika shule kongwe zilizolengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji na urejeshaji wa fedha za mikopo zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Kamati imebaini kuwa utaratibu wa halmashauri nchini kutumia asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa makundi maalum, umekuwa wa manufaa makubwa katika jitihada za kuboresha uchumi wa wananchi na maisha yao. Kamati inazipongeza Halmashauri zinazofanikisha azma hiyo muhimu.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imegundua kuwa Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Fedha za asilimia 10 una udhaifu. Kwa mfano, baadhi ya Halmashauri kutokuwa na kumbukumbu za kutosha kuhusu fedha zilizokopeshwa, zilizorejeshwa na idadi ya vikundi vilivyokopa. Changamoto nyingine ni upungufu katika Sheria na Kanuni zilizoanzisha Mfuko huu ambapo kuna baadhi ya makundi yamesahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka ulilenga kuwasafirisha watu wengi kwa wakati mmoja ili waweze kufika haraka wanapokwenda. Utekelezaji wa Mradi huo umechangia uboreshaji huduma ya usafiri Jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, zipo changamoto zilizobainika ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Miiongoni mwa changamoto hizo ni udhaifu katika Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa *DART* kama vile kukosekana kwa sheria inayosimamia usafiri wa umma mijini na kukosekana kwa mfumo thabitii wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya soko na gulio ni muhimu kwa wananchi ili kuwawezesha kuuza na kununua bidhaa. Aidha, Halmashauri hufanikisha makusanyo kutoka kwenye huduma hiyo na wananchi wanaouza na kununua mazao au bidhaa kupata mazingira bora ya uuzaaji na ununuuzi. Katika kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022, Halmashauri nyingi zimefanikiwa katika kuwezesha mazingira mazuri ya masoko na magilio. Hata hivyo, jambo hili limekabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa walangazi ambao wanajihusisha na kupangisha vizimba (mabanda) ya biashara kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inasababisha tatizo la wafanyabiashara kupangiwa bei kubwa tofauti na gharama halisi za upangishaji za soko hali ambayo husababisha wafanyabiashara kushindwa kupanga katika vizimba au mabanda hayo. Jambo hili linaathiri mapato ya Halmashauri na masoko pamoja na kuzagaa kwa wauzaji na wanunuazi ndani ya maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ipo changamoto ya masoko yaliyojengwa kwa ghorofa kutoendana na hali halisi ya uhitaji na hivyo kuikosesesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kutokana na uhitaji wa uendelezaji Soko la Kariakoo lilitotokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali. Miongoni mwa mafanikio ya shirika hilo ni kuendelea kudhibiti na kusimamia masoko ya Kariakoo. Pamoja na changamoto hizo, shirika hilo linakabiliwa na changamoto ya mfumo wa uendeshaji na usimamizi, hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kikamilifu ikiwemo kukarabati miundombinu ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine inatokana na upungufu katika Sheria Na. 36 ya Mwaka 1974 illyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo. Sheria hiyo inasimamia uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Shirika la Masoko Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Wakala wa Barabara Vijijiini na Mijini (*TARURA*) ulizunduliwa tarehe 02 Julai, 2017 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali GN Na. 211 ya tarehe 12 Mei, 2017, takribani miaka mitano sasa. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuwezesha matengenezo endelevu ya mtandao wa barabara mijini na vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 inaitaka Serikali kuendeleza shughuli za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili ifikie malengo yake ya kuwezesha wananchi kuendelea na uzalishaji kwa ajili ya kuongeza kipato chao. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeelekezwa kuimarisha Mfuko wa Barabara ikiwemo kuboresha Mfumo wa ukusanyaji mapato unaotumiwa na *TARURA* na *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa *TARURA* imekuwa na manufaa makubwa katika kubuni, kuendeleza, kukarabati na kutengeneza mMtandao wa barabara mijini na vijijiini.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mafanikio hayo ni pamoja na kuwezesha maendeleo katika ujenzi wa miundombinu na usimamizi wake mijini na vijiji. Maendeleo hayo yanaendana na kaulimbiu ya *TARURA* isemayo: Ninanukuu: "*TARURA tunakufungulia barabara kufika kusikofikika*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendelezaji wa barabara mijini na vijini, *TARURA* huzingatia hati ya uanzishwaji wake ya mwaka 2017 inayoipa jukumu la kutoza ada kwa maegesho ya magari katika hifadhi ya barabara na matumizi ya hifadhi ya barabara. *TARURA* pamoja na mambo mengine, mwaka 2020/2021 ilianzisha matumizi ya Mfumo wa *TerMIS* kwa ajili ya kukusanya ada ya maegesho katika hifadhi za barabara. Kwa kutumia Mfumo huo, *TARURA* inakusanya mapato kiasi cha shilingi bilioni 80 kwa mwaka. Kabla ya kuwepo kwa mfumo ilikuwa inakusanya kiasi cha shilingi billioni 38 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia. Kwa kutumia mfumo huo, *TARURA* inakusanya mapato kiasi cha shilingi milioni 80 kwa mwezi, kabla ya kuwepo kwa mfumo ilikuwa inakusanya kiasi cha shilingi milioni 38 kwa mwezi. Makusanyo hayo yameongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 42 sawa na asilimia 90.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza *TARURA* kwa kuongeza mapato kwa zaidi ya mara mbili ya makusanyo ya awali. Ni rai ya Kamati kwamba ongezeko hili litatumika vizuri katika kutekeleza ukarabati na ujenzi wa barabara mpya na hivyo kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, matumizi ya mfumo yanakabiliwa na changamoto inayotokana na matumizi ya mtandao wa Halotel ambao unatumia Teknolojia ya 3G. Kwa teknolojia hiyo, mfumo wa malipo unaotumika hufanya kazi taratibu na kuchangia ucheleweshaji wa kuchakata taarifa za Ankara. Changamoto hiyo husababisha ankara kutolipwa kwa wakati

na nyininge kutolipwa kabisa, jambo linalosababisha kupotea kwa baadhi ya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto nyininge ni ukarabati wa barabara kipindi cha masika bila kuzingatia majira katika maeneo husika. Mfumo wa manunuzi ya vifaa kufanyika mikoani badala ya Halmashauri na kuchelewa kwa taratibu za manunuzi hali inayoongeza gharama na kuathiri ufanikishaji wa matarajio ya wananchi kwa wakati na mikataba kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kimakati inayotekelawa na Halmashauri nchini inakusudia kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza mapato, kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchangia ustawi wa maisha ya wananchi. Kwa utaratibu huo, yapo mafanikio iliyopatikana tangu kuanza kwa miradi hiyo ikiwemo ukusanyaji mkubwa wa mapato. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa iliripotiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 1.25 kutoka ghala la mazao tangu mradi ulipoanza kutoa huduma mwaka 2020 katika msimu wa Korosho. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Tunduru iliripotiwa kukusanya kiasi cha shilingi milioni 91.5 kutoka mradi wa maegesho ya malori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, zipo changamaoto zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kufikia tija iliyokusudiwa kupatikana kutokana na miradi hiyo. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za kimkakati hautoi fursa sawa kwa Halmashauri zote na usimamizi hafifu katika ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa kwa Kamati haikuonyesha matumizi ya fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo, badala yake taarifa hiyo imejikita katika matumizi ya fedha zilizotolewa na Serikali Kuu tu, kama vile fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19, ambao ulizinduliwa na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Rais tarehe 10 Oktoba, 2021, na fedha za programu nyingine kama zilivyoonekana katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka TAMISEMI kuziagiza Halmashauri zote nchini kuwasilisha taarifa ya matumizi ya fedha zilizokuwa zimetengwa kwenye bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2021/2022. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia msingi katika kutoa huduma zinazowezesha maisha bora ya wananchi. Azma ya Serikali kufanikisha dhima ya Utumishi wa Umma inategemea uzingatiaji wa misingi ya utawala bora, utawala wa sheria na madaraka kwa wananchi. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayo dhima ya kuhakikisha kuwa, utaratibu wa kufanya uamuzi katika Utumishi wa Umma unazingatia utu, haki, ushirikishwaji, uwazi, uwajibikaji, tija, ufanisi na ushiriki wa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambayo inapaswa kuzingatiwa na Serikali, ilitoa ahadi kwa wananchi kuwa: Ninanukuu: "*Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha viongozi wanaoteuliwa ni waadilifu, wawajibikaji, wanaoleta matokeo chanya na kutumia rasilimali za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kufuatilia utekelezaji wa Program na majukumu ya Ofisi hii, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi. Naomba kubainisha baadhi ya mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliundwa kwa lengo la kukuza na kusimamia viwango vya maadili ili kuongeza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma na utaratibu wote wa kutoa uamuzi wa Serikali na Utumishi wa Umma.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Taasisi hii ni Idara ya Serikali inayojitegemea na ilianza kazi mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imefanikiwa kuendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuchunguza tabia na mienendo wa Viongozi wa Umma ili kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa ipasavyo. Hata hivyo, usimamiaji wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398 unakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa ukomo wa kutoa Tamko la mwisho wa kutumikia wadhifa wa kiongozi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) ilianzishwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007. Sheria hii illtokana na Bunge kuitisha Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007. Kupitia Sheria hii, Bunge liliweka mazingira bora kisheria, kiutawala na kutekelezaji yenye mwelekeo wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzisha TAKUKURU, sheria imewezesha mambo Makuu yafuatayo: Upatikanaji wa ushauri kuhusu mienendo na taratibu mbalimbali katika utekelelezaji wa shughuli za umma, Mashirika ya Umma na za taasisi binafsi nchini kwa lengo la uwezeshaji wa kung'amua na kuzuia rushwa kwa ufanisi; upatikanaji wa habari au taarifa mbalimbali kuhusu athari za rushwa; kuwezesha au kufanikisha ushirikiano mzuri, wenye manufaa na tija kati ya taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi; kuhimiza ustawi na kuimarisha ushiriki wa umma kwa ujumla katika kupambana na rushwa nchini; na kuwezesha kufanyika kwa uchunguzi, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka dhidi ya watu wanaojihuisha na vitendo vya rushwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Februari, 2021 hadi tunaporipoti, TAKUKURU imeweza kufanikiwa katika maeneo hayo. Hata hivyo, zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kuzingatiwa katika uendeshaji wa TAKUKURU na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mapambano dhidi ya rushwa. Kwa mfano, ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi na vitendea kazi, kukosekana kwa ofisi za TAKUKURU na nyumba za watumishi katika baadhi ya Halmashauri/Wilaya pamoja na upungufu katika sheria iliyoanzisha TAKUKURU. Changamoto hizi zinaathiri ufanisi uliokusudiwa wakati wa kuanzishwa chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Serikali Mtandao iliundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 30, Sura ya 245 ya mwaka 1997 chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Jukumu Kuu la Wakala ni kusimamia Serikali Mtandao na kuratibu maendeleo ya TEHAMA ndani ya Serikali na taasisi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Serikali Mtandao Umefanikisha kubadili na kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao, hususan kwenye maeneo ya sera, sheria, miongozo, usimamizi, utengenezaji wa mifumo tumizi ya kielekroniki na ujenzi wa miundombinu ya pamoja ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala ya Serikali Mtandao, bado zipo baadhi ya taasisi za umma zinazoanzisha mifumo ya ukusanyaji mapato bila kushirikisha Wakala wa Serikali Mtandao, ambao ndio wenyewe mamlaka na dhamana ya uanzishwaji mifumo ya TEHAMA. Aidha, zipo taasisi za umma zinazoendelea kuandaa na kutumia mifumo ya TEHAMA bila kuratibiwa na Wakala ya Serikali Mtandao. Hali hiyo inasababisha kuwa na mifumo isiyofanana katika ukusanyaji wa mapato ndani ya Serikali, hali inayoweza kuongeza kero kwa wananchi na kuathiri udhibiti wa matumizi ya TEHAMA Serikalini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uende kwenye mapendekezo na maoni ya Kamati.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyelekti, kwa kuzingatia muundo wa hoja zinazowasilishwa Bungeni, ulioelezwa katika Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kwa namna itakayowezesha Bunge kuamua kama ifuatavyo: -

Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Serikali nchini:-

Kwa kuwa lengo la Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Serikali ili kuweka mazingira bora ya kufundisha na kufundishia limekwamishwa na Wakandarasi Wakala wa Majengo Serikalini (*TBA*) walioshindwa kukalimisha ujenzi kwa wakati;

Na kwa kuwa kutokamilika kwa ukarabati huo kunachalewesha nia ya uboreshaji mazingira ya walimu ya kufundisha na kufundishia;

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kwamba, utaratibu wa kupata Wakandarasi uwe ni wa ushindani. *TBA* wasitumike kuwa Wakandarasi pekee katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali, bali utumike utaratibu wa kushindanisha Wakandarasi au kwa kutumia "*Force Account*" pale inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyelekti, pili, utaratibu wa Halmashauri nchini kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa makundi maalumu:-

Kwa kuwa imebainika kuwa hakuna mfumo madhubuti wa kudhitibi uendeshaji na usimamizi wa fedha za asilimia kumi katika Halmashauri;

Na kwa kuwa, hali hiyo inazuia mafanikio ya mpango huu;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri kwamba, Serikali kwa kutumia Wakala wa Serikali Mtandao kutengeneza mfumo madhubuti utakaozungumza na kuratibu taarifa za ukopeshaji, urejeshaji pamoja na kutambua vikundi vilivyokopeshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuleta Marekebisho ya Sheria na Kanuni ili Mfuko huu uweze kukidhi mahitaji ya Makundi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mabasi yaendayo haraka:-

Kwa kuwa kukosekana kwa sheria inayosimamia usafiri mijini inaathili shughuli za uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam;

Na kwa kuwa kuzorotesha huduma hiyo kunatokana mifumo ya kikwazo kwa juhudhi ya Serikali kuboresha huduma ya usafiri Jijini Dar es Salaam;

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba, Serikali iandae Muswada wa Sheria utakaoweka Mfumo mzuri wa kisheria unaosimamia usafiri wa umma mijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa masoko nchini:-

Kwa kuwa, kujitekeza kwa walangazi wanaopangisha vizimba vyaa biashara kwenye maeneo ya masoko yanayojengwa na Halmashauri ni jambo linaloongeza gharama kwa wafanyabiashara;

Na kwa kuwa, kuongezeka kwa gharama hizo kunachangia kupunguza uwezo wa wafanyabiashara kupanga katika vizimba, hali inayosababisha kuzagaa kwa uuzaaji na ununuaji ndani ya Halmashauri pamoja na kupotea kwa mapato ya Serkali;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba, Serikali iweke utaratibu madhubuti kisheria utakaobaini ufanyaji kazi wa wahusika wote wakiwemo watu wa kati pamoja na kubainisha bei elekezi ya upangishaji wa vizimba nya Soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo:-

Kwa kuwa mtaji mdogo kwa Shirika la Masoko Kariakoo unasababisha uwezo mdogo wa Shirika hilo kutekeleza majukumu yake ikiwemo kudhibiti na kusimamia masoko na miradi yake,

Na kwa kuwa uwezo huo mdogo pamoja na upungufu uliopo katika sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo, vinaathiri dhima ya shirika hilo,

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba: -

- (i) Serikali iliongezee mtaji Shirika hilo;
- (ii) Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Barara Vijijini na Mijini

Kwa kuwa kasi ndogo ya Mtando wa Halotel inayotumia teknolojia ya *3G* na ambayo inatumwa na Mfumo wa *TeRMIS* wa *TARURA* katika ukusanyaji wa ada za maegesho ya magari, inasabisha ucheleweshaji wa taarifa za ankara na kupotea kwa mapato ya Serikali,

Na kwa kuwa tatizo hilo kwa pamoja na changamoto ya Mikataba ya Wakandarasi kutotekelezwa inavyostahili, ufinyu wa bajeti na ujenzi wa barabara kutozingatia majira inakwamisha dhamira ya *TARURA* kufanikisha Usanifu, Ujenzi na Ukarabati wa barabara Vijijini na Mijini,

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba: -

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) Serikali itafute utaratibu endelevu utakaowezesha *TARURA* kupata fedha za kutosha ili iweze kutekeleza kazi zake za kukarabati na kujenga barabara mpya.

(ii) Serikali iiwezeshe Wakala wa Barabara Vijiji kuwa na mtandao wenye nguvu na kasi zaidi;

(iii) *TARURA* isimamiwe kuhakikisha kuwa mikataba ya wakandarasi inatekelezwa kwa wakati na inavyostahili;

(iv) Mfumo wa manunuzi wa *TARURA* ushushwe kwenye ngazi ya halmashauri badala ya kufanyika mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya Kimkakati katika halmashauri nchini: -

Kwa kuwa mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za Kimkakati hautoi fursa sawa kwa halmashauri zote;

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri ufanisi katika kufanikisha azma ya Serikali;

Kwa hiyo basi Bunge linalishauri kuwa TAMISEMI iharakishe kufanya marekebisho katika mwongozo utakaotoa fursa sawa kwa halmashauri zote nchini ili kukidhi azma ya Serikali ya kuongeza mapato ya halmashauri na kuwezesha ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Kwa kuwa kumekuwa na miradi ya kimkakati inayojengwa na halmashauri (masoko) ambayo haifanyi vizuri kama ilivyokusudiwa;

Na kwa kuwa miradi hiyo haileti tija iliyokusudiwa,

Kwa hiyo basi Bunge linalishauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili miradi inayojengwa iendane na hali halisi ya uhitaji wa wananchi.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: -

Kwa kuwa kukosekana kwa ukomo wa kutoa tamko la mwisho wa kutumikia wadhifa wa kiongozi wa Umma ni jambo linalosababisha ugumu katika kusimamia masharti hayo ya kisheria,

Na kwa kuwa hali hiyo inaleta ugumu kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kusimamia matakwa hayo ya kisheria;

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba, Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili kuweka Ukomo wa Viongozi wa Umma kuwasilisha tamko la mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU): -

Kwa kuwa TAKUKURU ambayo ni miongoni mwa Taasisi za Utawala Bora na Uwajibikaji nichini, inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, uchache wa watumishi, upungufu wa vitendea kazi pamoja na upungufu katika sheria ilioanzisha taasisi hiyo,

Na kwa kuwa changamoto hizo zilizobainishwa zinaathiri ufanisi wa TAKUKURU katika kufanikisha lengo la Serikali la kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na maadili katika utumishi wa Umma;

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba: -

(i) TAKUKURU iwezeshwe zaidi kibajeti ili ifanikishe utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria;

(ii) Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria kwa lengo la kuondoa upungufu katika sheria hiyo.

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(iii) TAKUKURU ijikite zaidi katika kuzuia rushwa badala ya kupambana wakati matendo ya rushwa yameshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Serikali Mtandao:-

Kwa kuwa Wakala ya Serikali Mtandao uliyoundwa kwa madhumuni ya kusimamia Serikali Mtandao na kuratibu matumizi ya TEHAMA Serikalini, unakabiliwa na tatizo la baadhi ya Taasisi za Umma kutotumia wakala huu na kuendeleza mifumo tumizi isiyodhibitiwa wala kuratibiwa,

Na kwa kuwa baadhi ya Taasisi za Umma huendeleza Mifumo tumizi bila kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni, taratibu, viwango na miongozo, inakinzana na mantiki ya kuanzhishwa kwa Wakala hii,

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba: -

(i) Serikali itoe Mwongozo thabiti kwa Taasisi zote za Umma zinazoanzisha program tumizi ikiwemo programu za ukusanyaji wa mapato.

(ii) Serikali Mtandao (*e-GA*) iimarishe na isimamie kikamilifu mifumo mbalimbali;

(iii) Serikali izikumbushe Taasisi zote za Umma kuzingatia kikamilifu, Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kufanikisha azma ya kuratibu matumizi ya TEHAMA Serikalini;

(iv) Serikali Mtandao itengeneze Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zote za Umma, Vyama vya Ushirika, *SACOSS* na kutambua wakulima nchini.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma:-

Kwa hiyo basi Bunge linashauria kwamba: -

(i) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iongeze juhudhi ya kuuelimisha Umma ili kuwanusuru watu dhidi ya utapeli na tatizo la kughushi katika mchakato wa Ajira;

(ii) Serikali iiwezeshe Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuwa na Mfumo madhubuti wenyewe uhakika wa usalama wake.

(iii) Taasisi zote za Serikali na za Umma zianze kutumila mifumo mipya ya ufuatiliaji na utendaji kazi;

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utoe hoja, na taarifa yako yote imeshaingia kwenye *Hansard*.

**MHE ABDALLAH J. CHAUREMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba taarifa yangu yote hii pamoja na pongezi kwa Mawaziri wote waliochaguliwa na pongezi kwa Kamati yangu yote ilionisaidia kuandaa taarifa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelizwa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wake pamoja na maoni ya jumla na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2021 - FEBRUARI, 2022 - KAMA ILIVYOWSILISHWA MEZANI

---

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **1.0 MAELEZO YA JUMLA**

##### **1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Februari 2021 hadi Februari, 2022. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 (Kanuni za Bunge).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge katika ufuatiliaji wa matokeo ya shughuli za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii. Aidha, maudhui ya Taarifa yanalisaidia Bunge kuhakiki hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya Wananchi kwa shughuli za Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimnti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

##### **1.2 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu Kuu Nne zifuatazo:-

- (i) Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelizwa;
- (ii) Sehemu ya pili inayofafanua shughuli zilizotekelizwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Aidha,

sehemu hii inabainisha mafanikio yaliyobainika na changamoto zinazojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inayotoa maoni na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kuamua; na

(iv) Sehemu ya nne na ya mwisho inayohitimisha na kutoa hoja kwa hatua ya Bunge lako Tukufu kujadili na kufanya uamuzi.

### **1.3 Msingi wa Shughuli zinazotekelzwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa shughuli zilizotekelzwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Katiba) inatambulisha lengo Kuu la Serikali la kuwezesha Ustawi wa Wananchi. Aidha, Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa Madaraka yake. Vile vile, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ni mojawapo kati ya Kamati Kumi na Nane za Kudumu za Bunge chini ya Kanuni ya 137 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge na ni mionganini mwa Kamati Tisa za Kisekta. Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Jukumu la Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ni kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Kanuni za Bunge, kimebainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati hii. Majukumu hayo ni:-

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- (iii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- (iv) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazozisimamia; na
- (v) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kujifunza Muundo na majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Lengo lilikuwa ni kuijandaa na kujipanga kwa wigo wa ufuatiliaji wa majukumu ya Wizara zinazohusika;
- (ii) Kupokea na kujadili Taarifa za Uendeshaji na Utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayotekelawa chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- (iii) Kujadili Taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ili kufuatilia utekelezaji wa Bajeti;
- (iv) Kutembelea na Kukagua Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na
- (v) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

#### **1.4 Njia ili yotumika**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge ambayo, pamoja na mambo mengine yanataka Taarifa ya Kamati ibainishe njia au mbinu ili yotumia, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kutekeleza shughuli za Kamati. Njia na mbinu hizo ni:-

- (i) Kuwapatia Wajumbe mafunzo ili kuwawezesha kuwa katika muktadha wa majukumu yao na kujielekeza kwenye matarajio ya Bunge la kumi na mbili kwa Kamati hii;
- (ii) Kufanya uchambuzi wa Taarifa zilizowasilishwa na kutathmini mambo yaliyori potiwa kwa kuoanisha na mtazamo wa Wananchi kuhusu ustawi wao;
- (iii) Kudadavua maudhui ya Taarifa zote zillizowasilishwa ili kupata utoshelevu wa maudhui kwa kulinganisha na mahitaji ya uelewa wa Kamati kuhusu jambo linalohusika;
- (iv) Kutembelea baadhi ya maeneo kwa lengo la kulinganisha yaliyori potiwa na hali halisi uwandani (in the field); na
- (v) Kujumuisha mambo yanayobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano na mahojiano ili kuorodhesha mambo Makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

Aidha, uthabiti wa maudhui ya Taarifa hii umetokana na njia na mbinu hizo.

#### **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MATOKEO**

#### **2.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Kamati kuripoti Bungeni utekelezaji wa shughuli zake ni kuliwezesha Bunge kufuatilia shughuli za Umma zinazotekelzwa na Serikali kupitia Wizara

zinazosimamiwa na Kamati hii. Ili kukamilisha azma hiyo, Kamati inaeleza matokeo ya utekelezaji wa shughuli hii kwa kuchambua yaliyobainika na kulionesha Bunge mafanikio na changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Umma chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii, naomba kufafanua shughuli zilizotekelawa na Kamati kama ifuatavyo:

### **2.1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika uendeshaji wa shughuli za Umma zinazosimamiwa na Kamati hii, Serikali pamoja na mambo mengine hutekeliza Miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa kutambua hilo, mwezi Machi, 2021 Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge na kutembelea baadhi ya Miradi iliyotekelawa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Jumla ya Miradi Tisa ilikaguliwa ambapo miwili ilitekelezwa chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Saba chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mine kati ya hiyo ilikaguliwa kwa upande wa Zanzibar na Mitatu Bara.

### **2.1.2 uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mzwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Machi, 2021, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022. Shughuli hiyo ilitokana na utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa **tarehe 19 na tarehe 22 Aprili, 2021** Kamati iliwasilisha Bungeni maoni yaliyotokana na shughuli hii.

### **2.1.3 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli na Majukumu Mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipokea na kuchambua jumla ya Taarifa kumi na tatu (13) kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taarifa sita (6) kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Shughuli hiyo illenga kuiwezesha Kamati kufahamu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ili kuboresha huduma na kuwezesha maisha bora ya Wananchi. Uchambuzi wa Taarifa hizo uliiwezesha Kamati kuhakiki mafanikio yanayoripotiwa kwa kulinganisha na hali ilivyo ikioanishwa na matarajio ya Wananchi. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu huu unafanikisha dhima ya Kamati kulisaidia Bunge katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

### **2.1.4 Ziara za Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, mbali na ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa taarifa mbalimbali, Kamati ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika mazingira halisi ya programu na mipango mbalimbali ya Serikali. Kamati iliweza kuwianisha taarifa zilizokuwa zikitolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi ilivyo kwenye maeneo yanayohusika. Kufanya hivyo, kuliwezesha Kamati kuhakiki mafanikio na changamoto ikilinganishwa na lengo la Serikali kuwezesha Ustawi wa Wananchi, kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge litaweza kufanya kazi mapendekezo ya Kamati kuhusu uboreshaji wa mambo mbalimbali kama inavyoelezwa katika sehemu ya mapendekezo. Mantiki yake inatokana na nafasi ya Sekta zilizo chini ya Kamati hii kwa maendeleo ya Taifa na maisha ya Wananchi. Sekta ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni Sekta wezeshi katika mafanikio ya Kiuchumi, Huduma bora kwa Wananchi na Ustawi wa maisha yao. Sekta ya Serikali za Mitaa ni kitovu (Hub) cha mafanikio ya shughuli za Umma

chini ya nyingine zote. Aidha, walengwa hasa wa mipango ya Serikali wanafikika kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufanikishwa na Utumishi wa Umma.

## **2.2 Uchambuzi wa Matokeo ya Shughuli zilizotekelizwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la shughuli zilizotekelizwa na Kamati ni kulisaidia Bunge hili kufuatilia na kuhakiki utekelezaji wa Sera, Mipango, Mikakati na Sheria mbalimbali nchini. Kigezo kikubwa ni tija inayopatikana katika maisha ya Wananchi na ufanisi wa huduma inayotolewa kwa Wananchi, ambao ndio Msingi wa Mamlaka na Madaraka yote kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

**Mheshimiwa Spika**, shughuli hizo zilliwezesha Kamati kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ufafanuzi wa matokeo hayo kwa kila Sekta ni kama ifuatavyo:-

### **2.2.1 Ofisi ya Rais - TAMISEMI**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali za Mitaa nchini. Kamati inatambua kuwa Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaanizisha Serikali za Mitaa na madhumuni yake yametajwa katika Ibara ya 146 ya Katiba. Kwa mujibu wa Ibara hiyo, Serikali za Mitaa zimeanzishwa ili kupeleka Madaraka kwa Wananchi. Aidha, vyombo vya Serikali za Mitaa vimepewa haki na Mamlaka ya kuwashirikisha Wananchi katika Mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweka utaratibu mzuri wa utekelezaji wa masharti hayo ya Katiba, Bunge lilitunga Sheria zinazofafanua uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97 (The Regional Administration Act (Cap. 97), Sheria ya Serikali za

Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 (The Local Government (District Authorities) CAP. 287) na Sheria ya Serikali za Mitaa, (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 (The Local Government (Urban Authorities) CAP. 288). Sheria hizo zinagusa moja kwa moja maisha ya Wananchi, jambo lililoifanya Kamati izingatie masharti yake kila ilipofuatilia shughuli za Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, Kamati ilichambua kwa kina yaliyojiri wakati wa kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa unaoratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Uchambuzi ulibainisha mafanikio na changamoto mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge baadhi ya mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

**(a) Ukarabati wa Shule Kongwe**

**Mheshimiwa Spika**, Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari nchini umekuwa na manufaa makubwa katika kuboresha utoaji wa huduma ya Elimu ya Sekondari. Kwa utaratibu huo, mafaniko yaliyopatikana ni pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia ikiwemo kuboresha miundombinu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoongeza morari ya Wanafunzi kujifunza na Walimu kufundisha. Hata hivyo, nia hiyo njema ya Serikali kutekeleza Mpango mzuri inakabiliwa na changamoto ya Wakandarasi kushindwa kumaliza ujenzi kwa wakati. Changamoto hii inachelewesha azma ya Serikali ya kuboresha mazingira ya utoaji huduma ya elimu ya Sekondari katika Shule Kongwe zilizolengwa.

**(b) Utoaji na Urejeshaji wa fedha za mikopo zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa utaratibu wa Halmashauri nchini kutumia asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa Makundi Maalum, umekuwa wa manufaa makubwa katika jitihada za kuboresha Uchumi wa Wananchi na maisha yao. Kamati inazipongeza Halmashauri zinazofanikisha azma hiyo muhimu. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa Mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa Fedha za asilimia 10 una udhaifu, kwa mfano, baadhi ya Halmashauri kutokuwa na kumbukumbu za

kutosha kuhusu fedha zilizokopeshwa, zilizorejeshwa na Idadi ya Vikundi vilivyokopa. Changamoto nydingine ni mapungufu katika Sheria na Kanuni zilizoanzisha Mfuko huu ambapo kuna baadhi ya Makundi yamesahaulika.

**(c) Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es salaam, ulilenga kuwasafirisha watu wengi kwa wakati mmoja ili waweze kufika haraka wanapokwenda. Nia ni kuawawesha watumiaji wa usafiri huo wafike mapema kwenye shughuli zao za uzalishaji mali na utoaji wa huduma. Utekelezaji wa Mradi huo umechangia kuboresha huduma ya usafiri Jijini Dar es salaam. Hata hivyo, zipo changamoto zilizobainika, ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa changamoto hizo ni Udhafifu katika Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa DART kama vile kukosekana kwa Sheria inayosimamia Usafiri wa Umma Mijini na kukosekana kwa Mfumo thabiti wa ukusanyaji wa mapato. Hali hiyo isiporekebishwa inaweza kukwamisha juhudzi za Serikali katika kujenga na kuendeleza Uchumi wa Kati na maendeleo ya Viwanda.

**(d) Mfumo wa Uendeshaji wa Masoko nchini**

**Mheshimiwa Spika**, huduma ya Soko na gulio ni muhimu kwa Wananchi ili kuwawezesha kuuza na kununua bidhaa. Aidha, Halmashauri hufanikisha makusanyo kutoka kwenye huduma hiyo na Wananchi wanaouza na kununua mazao au bidhaa kupata mazingira bora ya uuzaaji na ununuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Februari 2022, Halmashauri nydingi zimefanikiwa katika kuwezesha mazingira mazuri ya masoko na magilio. Hata hivyo, jambo hili limekabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa Walanguzi ambaao wanajihusisha na kupangisha vizimba (mabanda) vya biashara kwenye masoko.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inasababisha tatizo la wafanyabiashara kupangiwa bei kubwa tofauti na ghamama halisi za upangishaji za Soko hali ambayo husababisha

Wafanyabiashara kushindwa kupanga katika vizimba au mabanda hayo. Jambo hili linaathiri mapato ya Halmashauri na Masoko pamoja na kuzagaa kwa uuzaaj na ununuaji ndani ya maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vile vile ipo changamoto ya Masoko yaliyojengwa kwa ghorofa kutoendana na hali halisi ya uhitaji hivyo kuikosesesha Serikali mapato.

**Utendaji wa Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC)**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kutokana na mahitaji ya kuendesha Soko la Kariakoo lililotokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali. Miongoni mwa mafanikio ya Shirika hilo ni kuendelea kudhibiti na kusimamia Masoko ya Kariakoo. Pamoja na mafanikio hayo, Shirika hilo linakabiliwa na changamoto ya Mfumo wa uendeshaji na usimamizi, hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kikamilifu ikiwemo kukarabati miundombinu ya Soko.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine inatokana na upungufu katika Sheria Na. 36 ya mwaka 1974 ilioanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo. Sheria hiyo inasimamia uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Shirika la Masoko Kariakoo.

**(e) Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini**

**Mheshimiwa Spika**, kama tunavyofahamu, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) ulizunduliwa tarehe 02 Julai 2017 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali GN Na. 211 ya tarehe 12 Mei, 2017, takriban miaka mitano sasa. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuwezesha matengenezo endelevu na kuendeleza mtandao wa barabara Mijini na Vijijini. Kwa madhumuni hayo TARURA ina dhima ya usanifu, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara Vijijini na Mijini kwa gharama nafuu na ufanisi mkubwa ili kuweka mazingira ya maendeleo ya Uchumi na Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inaitaka Serikali kuendeleza shughuli za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili ifikie malengo yake ya kuwezesha Wananchi kuendelea na uzalishaji kwa ajili ya kuongeza

kipato chao. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeelekezwa kuimarisha Mfuko wa Barabara ikiwemo kuboresha Mfumo wa ukusanyaji mapato unaotumiwa na TARURA na TANROADS.<sup>1</sup>

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa TARURA imekuwa na manufaa makubwa katika kubuni, kuendeleza, kukarabati na kutengeneza Mtandao wa barabara Mijini na Vijijiini. Mafanikio hayo ni pamoja na kuwezesha maendeleo katika ujenzi wa miundombinu na usimamizi wake Mijini na Vijijiini. Maendeleo hayo yanaendana na kauli mbiu ya TARURA isemayo:

**Ninanukuu:** "TARURA tunakufungulia barabara kufika kusikofikika" **Mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa kauli mbiu hiyo unaendelea kuchangia mazingira wezeshi ya shughuli za Wananchi kiuchumi na Kijamii pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma. Mambo hayo yanaendana na nia ya Serikali kufanikisha Ustawi wa Wananchi na maisha bora kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendelezaji wa Barabara Mijini na Vijini TARURA huzingatia hati ya Uanzishwaji wake ya mwaka 2017 inayoipa jukumu la kutoza ada kwa maegesho ya magari katika hifadhi ya barabara na matumizi ya hifadhi ya barabara (kama vile kupitisha *cable* za mawasiliano). Kwa majukumu hayo, TARURA pamoja na mambo mengine, mwaka 2021 ilianza matumizi ya Mfumo wa TerMIS kwa ajili ya kukusanya ada ya maegesho katika hifadhi za barabara. Kwa kutumia Mfumo huo, TARURA inakusanya mapato kiasi cha **Shilingi Milioni 80** kwa mwezi, kabla ya kuwepo kwa Mfumo ilikuwa inakusanya kiasi cha **Shilingi Milioni 38** kwa mwezi. Makusanyo hayo yameongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Milioni 42** sawa na **asilimia 90.4**.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza TARURA kwa kuongeza mapato kwa zaidi ya mara mbili ya makusanyo ya

awali. Ni rai ya Kamati kwamba ongezeko hili litatumika vizuri katika kutekeleza ukarabati na ujenzi wa barabara mpya na hivyo kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, matumizi ya Mfumo huo yanakabiliwa na changamoto inayotokana na matumizi ya mtandao wa Halotel ambao unatumia Teknolojia ya 3G. Kwa teknolojia hiyo, Mfumo wa malipo unaotumika hufanya kazi taratibu na kuchangia ucheleweshaji wa kuchakata taarifa za Ankara. Changamoto hiyo, husababisha ankara kutolipwa kwa wakati na nyininge kutolipwa kabisa, jambo linalosababisha kupotea kwa baadhi ya mapato ya Serikali. Changamoto zingine ni Ufinyu wa bajeti, ukarabati wa barabara kipindi cha masika bila kuzingatia majira katika maeneo husika, Mfumo wa manunuzi ya vifaa kufanyika Mkoani badala ya Halmashauri na kuchelewa kwa taratibu za manunuzi hali inayoongeza gharama na kuathiri ufanikishaji wa matarajio ya Wananchi kwa wakati na Mikataba kutokamiliika kwa wakati. Jambo hili lilibainika katika kauli aliyoitao Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI aliposema: -

**Ninanukuu:** *"Kumekuwa na changamoto ya Mikataba kutotekelizwa kwa wakati, Mikataba inasainiwa lakini haimaliziki kwa wakati, hivyo tunalazimika kuongeza muda wa utekelezaji wake..."<sup>2</sup> **Mwisho wa kunukuu.***

**(f) Miradi ya Kimkakati katika Halmashauri nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Miradi ya Kimakati inayotekelizwa na Halmashauri nchini inakusudia kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza mapato, kutoa huduma bora kwa Wananchi na kuchangia Ustawi wa maisha ya Wananchi. Kwa utaratibu huo, yapo mafanikio yaliyopatikana tangu kuanza kwa Miradi hiyo ikiwemo ukusanyaji mkubwa wa mapato. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa iliripotiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.25** kutoka katika ghalia mazao tangu mradi ulipoanza kutoa huduma mwaka 2020 katika msimu wa Korosho. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Tunduma iliripotiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Milioni 91.8** kutoka mradi wa maegesho ya malori.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, zipo changamaoto zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kufikia tija iliyokusudiwa kupatikana kutokana na Miradi hiyo. Kwa mfano, Kamati ilibainika kuwa mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za Kimkakati hautoi fursa sawa kwa Halmashauri zote na usimamizi hafifu katika ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya mapato. Athari yake inajitokeza katika utoaji wa huduma kwa Wananchi ndani ya eneo la Halmashauri inayohusika.

**Mheshimiwa Spika** Msingi wa utaratibu wa Miradi ya Kimkakati kwenye Halmashauri zetu, unatokana na ukweli kwamba, upatikanaji wa mapato ya kutosha na yenye uhakika kwenye Halmashauri hizo ni nguzo imara katika kuboresha utoaji huduma nzuri na zenye uhakika kwa Wananchi. Kwa mantiki hiyo, changamoto ya Halmashauri kutopata fursa sawa wa fedha za Kimkakati unaathiri ufanisi katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwezesha ustawi wa Wananchi.

**(g) Fedha za Maendeleo (Asilimia 60/40)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa kwa Kamati haikuonyesha matumizi ya Fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo, badala yake taarifa hiyo imejikita katika matumizi ya fedha zilizotoka Serikali Kuu, kama vile fedha za **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19**, ambao ulizinduliwa na Mhe. Rais tarehe 10 Oktoba, 2021, **Programu Endelevu ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS)**, **Mradi wa Lipa Kutokana na Matokeo (EP4R)**, **Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**, na **Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Elimu Msingi Awamu ya Pili (GPE-LANES)** ambazo kimsingi zimefanya kazi nzuri sana hususan katika Sekta ya Elimu na Afya ambapo imejenga Madarasa, Zahanati na Vituo vya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka TAMISEMI kuziagiza Halmashauri zote nchini kuwasilisha Taarifa za matumizi ya Fedha zilizokuwa zimetengwa kwenye bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2021/2022.

## **2.2.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia msingi katika kutoa huduma zinazowezesha maisha bora ya Wananchi. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma inajumuisha Mfumo wa kiutawala na kimenejimenti uliokabidhiwa dhamana na jukumu la kuhakikisha kuwa, Jamii inapata huduma inayokusudiwa kutoka Serikalini au Taasisi yoyote kwa niaba ya Serikali. Huduma hiyo hutolewa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Azma ya Serikali kufanikisha dhima ya Utumishi wa Umma inategemea uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora, Utawala wa Sheria na Madaraka kwa Wananchi. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayo dhima ya kuhakikisha kuwa, utaratibu wa kufanya uamuzi katika Utumishi wa Umma unazingatia utu, haki, ushirikishwaji, uwazi, uwajibikaji, tija, ufanisi na ushiriki wa makundi mbalimbali. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambayo inapaswa kuzingatiwa na Serikali, ilitoa ahadi kwa Wananchi kuwa:

**Ninanukuu:** *"Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha Viongozi wanaoteuliwa ni waadilifu, wawajibikaji, wanaoleta matokeo chanya na kutumia rasilimali za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi."*<sup>3</sup> **Mwisho wa kunukuu**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilizingatia ahadi na majukumu yake kwa kutumia Taasisi zifuatazo:-

- (i) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU);
- (iii) Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA);
- (iv) Sekretareti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- (v) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa;
- (vi) Wakala wa Ndege za Serikali; na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (vii) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC),
- (viii) Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Tanzania (TASAF)

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kufuatilia utekelezaji wa Mipango, Program na majukumu ya Ofisi hii, Kamati ilibaini mafanikio kadhaa. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kufanikisha azma ya Serikali. Naomba kubainisha baadhi ya mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

### **(a) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliundwa kwa lengo la kukuza na kusimamia viwango vya Maadili ili kuongeza imani ya Wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma na utaratibu wote wa kutoa uamuzi wa Serikali na Utumishi wa Umma. Taasisi hii ni Idara ya Serikali inayojitegemea na illanza kazi mwaka 1996. Kwa sasa Serikali inatarajia kuimarisha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili iweze kuboresha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398.

**Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imefanikiwa kuendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuchunguza tabia na mwenendo wa Viongozi wa Umma ili kuhakikisha kwamba, masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa ipasavyo. Hata hivyo, usimamiaji wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398 unakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa ukomo wa kutoa Tamko la mwisho wa kutumikia Wadhifa wa Kiogoz wa Umma.

### **(b) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU)**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilianzishwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007. Sheria hii ilitokana na Bunge kuitisha Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2007, mnamo tarehe 16 Aprili, 2007<sup>4</sup>. Muswada huo ulisainiwa na Rais na kuanza kutumika tarehe 01 Julai, 2007. Kupitia Sheria hii, Bunge liliweka

mazingira bora kisheria, kiutawala na kiutekelezaji yenyе mwelekeo wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini. Dhamira ya Bunge ilikuwa ni kuhakikisha Ustawi wa Utawala Bora na kuondoa rushwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuanzisha TAKUKURU, Sheria imeweza mambo Makuu yafuatayo: -

- (i) Upatikanaji wa ushauri kuhusu mienendo na taratibu mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za Umma, Mashirika ya Umma na za Taasisi Binafsi nchini kwa lengo la uwezeshaji wa kung'amua na kuzuia rushwa kwa ufanisi;
- (ii) Upatikanaji wa habari au Taarifa mbalimbali kuhusu athari za rushwa na vitendo mbalimbali vya rushwa nchini;
- (iii) Kuwezesha au kufanikisha ushirikiano mzuri, wenye manufaa na tija katika Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi, zinazojihusisha na mapambano dhidi ya rushwa;
- (iv) Kuhimiza ustawi na kuimarisha ushiriki wa Umma kwa ujumla katika kupambana na rushwa nchini; na
- (v) Kuwezesha kufanyika kwa uchunguzi, upelevi na uendeshaji wa mashtaka dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari 2021 hadi tunaporipoti, TAKUKURU imeweza kufanikiwa katika maeneo hayo. Hata hivyo, zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kuzingatiwa katika uendeshaji wa TAKUKURU na mapambano dhidi ya rushwa. Kwa mfano, ufinyu wa bajeti, uhaba wa Watumishi na Vitendea kazi, kukosekana kwa Ofisi za TAKUKURU na nyumba za Watumishi katika baadhi ya Halmashauri/Wilaya pamoja na upungufu katika Sheria iliyoanzisha TAKUKURU. Changamaoto hizi zinaathiri ufanisi uliokusudiwa wakati wa kuanzisha chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Serikali iliahidi kwa Wananchi kwamba itaimarisha Taasisi za Utawala Bora,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Maadili na Uwajibikaji kati ya mwaka 2021 – 2025. Miongoni mwa Taasisi hizo ni TAKUKURU. Kamati inaamini kuwa utatuzi wa changamoto za TAKUKURU ni sehemu ya hatua ya kuimarisha Taasisi za Utawala Bora na Uwajibikaji.

### **(c) Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Serikali Mtandao iliundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 30, Sura ya 245 ya mwaka 1997 chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Jukumu Kuu la Wakala ni kusimamia Serikali Mtandao na kuratibu maendeleo ya TEHAMA ndani ya Serikali na Taasisi zake. Jukumu hili lilitokana na matokeo ya tathmini ya hali halisi ya matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Serikali, ambapo Taasisi nyingi zillionyesha kujitengenezea Mifumo na Raslimali nyingine za TEHAMA bila kujali kuwepo kwa jitihada kama hizo katika Taasisi nyingine. Hali hiyo illichangia kuwa na urudufu wa jitihada za TEHAMA zinazofanana na zisizowasiliana wala kubadilishana taarifa.

**Mheshimiwa Spika**, yote hiyo inatokana na uvumbuzi wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambao umeleta fursa za maendeleo kwa Mtu binafsi au kwa Taasisi inayohusika na faida nyingi zisizomithilika katika uendeshaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali na maisha kwa ujumla. Serikali ilibaini kuwa TEHAMA ni nyenzo muhimu ya kuboresha huduma kwa Wananchi na kuchangia Ustawi wa maisha yao.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Serikali Mtandao Umefanikisha kubadili na kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Serikali imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao, hususan kwenye maeneo ya Sera, Sheria, Miongozo, Usimamizi, utengenezaji wa Mifumo tumizi na ya Kimkakati ya TEHAMA, na ujenzi wa miundombinu ya pamoja ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala ya Serikali Mtandao, bado zipo baadhi ya Taasisi za Umma zinazoanzisha Mifumo ya ukusanyaji mapato bila

kushirikisha Wakala ya Serikali Mtandano, ambayo ndiyo yenyewe Mamlaka na dhamana ya kuanzisha Mifumo ya TEHAMA. Kwa hali hii kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kupoteza mapato mengi kwa kuwa hakuna udhibiti wa e-GA (Mifumo ya makusanyo haiongei na e-GA). Aidha, baadhi ya Taasisi za Umma zinatumia Mifumo ya TEHAMA bila kuzingatia kikamilifu, Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo inayotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, zipo Taasisi za Umma zinazoendelea kuandaa na kutumia Mifumo ya TEHAMA bila kuratibiwa na Wakala ya Serikali Mtandao. Hali hiyo inasababisha kuwa na Mifumo isiyofanana katika ukusanyaji wa mapato ndani ya Serikali, hali inayoweza kuongeza kero kwa Wananchi na kuathiri udhibiti wa matumizi ya TEHAMA Serikalini.

#### **(d) Sekretareti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa. Taasisi hii inahusika na kuiwezesha Serikali kupata Watumishi wenyewe sifa, ujuzi na haiba stahiki. Katika kufanikisha hilo, Taasisi hiyo imeweza kuimarisha mifumo yake mbalimbali ya udhibiti na kiutendaji wakati wa kuendesha mchakato wa ajira.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri iliyofikiwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo, kutopata ubora wa wahitimu walioko katika Soko la Ajira, kutokuzingatiwa kwa uwiano wa waombaji na wanaoitwa kwenye usaili hasa ukizingatia kuwa usaili unafanyika Makao Makuu ya Nchi na Vijana wengi wanatoka Vijiijini na Vijana wengi kutumia gharama kubwa na kupoteza muda mwingi katika usaili. Aidha, kukuwa kwa teknolojia na Mifumo ya mawasiliano kumesababisha baadhi ya watu kuitumia vibaya. Mfano wa matumizi mabaya ya teknolojia ni kughushi nyaraka za Serikali ikiwemo barua za ajira, kutapeli baadhi ya waombaji kazi wakijifanya Watumishi wa Taasisi hii na pia

baadhi ya waombaji kazi wenyewe kutumia teknolojia kama simu wakati wa usaili.

#### **(e) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ni idara inayojitegemea iliyoanza kutekeleza shughuli zake kwa muundo huo, kuanzia mwezi Julai, 2015. Historia ya majukumu yanayotekelawa na Idara hii iliaanza mwaka 1963 wakati Hayati Baba wa Taifa, Rais Julius Kambarage Nyerere alipotoa Waraka Na.7 wa Mwaka 1963 ambao ulioa mwongozo juu ya utunzaji bora wa nyaraka za Serikali. Waraka huo ulielekeza namna ya kutunza, kuhifadhi na kuteketeza nyaraka za Serikali. Baadaye mfumo wa kisheria kuhusu utunzaji wa nyaraka ulirekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Idara hii inahusika na uhifadhi wa Nyaraka ambazo ni urithi andishi wa Taifa letu. Aidha, Idara inafanya kazi ya kuuelimisha Umma juu ya umuhimu wake na kuwezesha Umma ndani na nje ya nchi kutumia Nyaraka hizi kwa tafiti mbalimbali. Vile vile, Idara ina jukumu la kukarabati Nyaraka na kuziweka katika mifumo ya kidijitali ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na kurahisisha upatikanaji wake kwa watumiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Idara hii imeweza kutumia njia za kisasa za TEHAMA katika kutunza kumbukumbu na nyaraka. Hata hivyo, kasi ya kuzihifadhi nyaraka hizo kidigitali ili kuimarisha usalama wake inahitaji kuongezwa. Kufanikisha hilo, Idara inakabiliwa na ufinyu wa bajeti kila mwaka hali inayoilazimu kupanga mipango ya utekelezaji isiyoendana na mazingira halisi jambo linaloweza kuathiri urtoaji wa huduma kwa Wananchi.

#### **(f) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii unatekelezwa katika pande mbili za Muungano, lengo likiwa ni kusaidia Jamii kunyanyua hali za kiuchumi pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu za Kijamii.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwa kuwa TASAF ni mradi wa Kimuungano, tarehe 11-13 Februari, 2022 Kamati ilitembelea Miradi inayotekelizwa Zanzibar ili kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo.

Kamati ilitembelea Miradi minne ambayo ni; Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya – katika Shehia ya Kihanga, Ujenzi wa Ukumbi wa Kufanya mitihani wanafunzi wa Skuli ya Kizimkazi Dimbani, ujenzi wa Ukumbi na Vyoo - Shehia ya Fujoni, na ujenzi wa Jengo la Utawala na Madarasa 3 Shehia ya Mkataleni na Mahonda. Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhidhishwa na Utekelezaji wa miradi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa maono yao mazuri na upendo kwa Wananchi wanaowaongoza kwa kukubali kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kwa mstakabali wa kunusuru Kaya Maskini. Aidha, Kamati inawapongeza kwa dhati kabisa Mawaziri, Mhe. Jenista Mhagama Mb, Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe.Dkt. Khalid Mohamed Salum Mb, Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anayesimamia Ofisi ya Viongozi wa Kitaifa ambao kwa pamoja wanasimamia kwa umahiri utekelezaji wa miradi hii na kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaostahili. Mheshimiwa Spika ni kawaida ya watu kusifia mtu wakati hayupo, lakini Kamati yangu inampongeza sana Mkurugenzi wa TASAF Ndg. Ladislaus J. Mwamanga kwa kazi nzuri anayoifanya katika kutekeleza Mpango wa TASAF.hususan katika Miradi ya Zanzibar. Ni rai ya Kamati kwa Viongozi wote wanaokabidhiwa dhamana ya Uongozi kufanya kazi kwa weledi na uaminifu ili kuleta tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana kutohana na miradi hiyo ni pamoja na; kuongezeka kwa kipato kwa Kaya za Walengwa kuititia Uhaulishaji fedha na malipo ya Ajira za muda, kuimarika kwa afya za Watoto chini ya miaka mitano na mama wajawazito, kupunguza msongamano wa Wanafunzi wakati wa Mitihani, kurahisisha upatikanaji wa

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

huduma za Afya na Elimu kuitia vituo vya Afya, Madarasa na Kumbi za mitihani na Ushikishwaji na ushiriki wa Jamii katika upatikanaji wa mali ya Jamii (*Community Assets Creation*). **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo utekelezaji wa mpango huu unakabiliwa na changamoto ya baadhi ya Kaya kutoingizwa kwenye mpango ingawa wanastahiki. Aidha, kuna changamoto ya uchakavu wa Madarasa yaliyojengwa katika awamu ya I ya TASAF.ambayo Wananchi waliomba majengo hayo yafanyiwe ukarabati.

### **SEHEMU YA TATU**

#### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, nirudie kusema kuwa utaratibu wa Kamati za Kudumu za Bunge kutoa Taarifa ya mwaka Bungeni, unaliwezesha Bunge kupata tawisira ya shughuli zinazotolewa taarifa. Kwa kuzingatia hilo, taarifa hii imefafanua mambo mbalimbali katika Ofisi nya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais -TAMISEMI zilizo chini ya Kamati hii. Ni maoni ya Kamati kuwa kwa maeneo ambayo yametekelezwa kwa ufanisi na tija kubwa, Serikali itaendeleza juhudhi hizo. Lengo ni kuwahudumia Wananchi na kuwezesha maisha bora ili kufanikisha lengo la Serikali lilitotajwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo ni ustawi wa Wananchi.

##### **3.1 Maoni ya jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo:-

(i) Kamati inampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na Maono ya hali ya juu katika kuleta maendeleo kwa mstakabali wa Wananchi. Aidha, Kamati inampongeza Mheshiwa Rais wetu kwa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya, Elimu na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nichini kwa pande zote za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar) Mheshimiwa Spika hatua hii ya

Mhe. Rais kuishirikisha Zanzibar katika miradi ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini unaimarisha kwa kiasi kikubwa Muungano wetu. Hongera sana Mhe. Rais.

(ii) Kutokana na hali ya sintofahamu ya kuungua kwa Masoko inayojitokeza mara kwa mara siku za hivi karibuni, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ichukue hatua madhubuti za kuzuia majanga hayo na kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini sababu za Masoko hayo Kuungua lengo likiwa ni kuondoa hasara kwa Serikali, Wafanyabiashara na watumiaji wengine wa Masoko.

(iii) Ofisi ya Rais TAMISEMI ifanye kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara zinazosimamia Sera ambazo utekelezaji wake unasi mamiwana TAMISEMI, Wizara hizo ni, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya ili kutatta changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu yao.

### **3.2 Ofisi ya Rais – TAMMISEMI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni yafuatayo kwa Ofisi ya Rais –TAMISEMI:-

(i) Hatua iliyofikiwa katika Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari ni jambo la kupongezwa. Aidha, changamoto ya Wakala wa Majengo ya Seriakil (TBA) ambao ni Wakandarasi kushindwa kumaliza ujenzi kwa wakati inapaswa kupatiwa ufumbuzi.

(ii) Manufaa yaliyopatikana kutokana na utaratibu wa Halmashauri nchini kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa Makundi Maalum yanafaa kuendelezwa. Aidha, changamoto ya kukosekana kwa Mfumo madhubuti wa kudhibiti Uendeshaji na Usimamizi wa fedha za asilimia kumi unahitaji ufumbuzi.

(iii) Mfanikio ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es salaam (UDART) yamechangia kuwezesha watumiaji wa usafiri huo wafike mapema kwenye shughuli zao za uzalishali

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mali. Aidha, changamoto ya kukosekana kwa Sheria inayosimamia usafiri wa Umma Mijini inahitaji ufumbuzi.

(iv) Mafanikio yaliyopatikana kwenye Halmashauri zilizowezesha mazingira mazuri ya Masoko na magilio yanafaa kuigwa na Halmashauri nyingine nchini. Hata hivyo, tatizo la watu wa katи (Walanguzi) wa Vizimba kwenye Masoko linahitaji utatuzi.

(v) Mafanikio ya Shirika la masoko ya Kariakoo yamewezesha udhibiti na usimamizi mzuri wa Masoko hayo. Hata hivyo, changamoto ya upungufu katika Sheri iliyoanzisha Shirika hilo pamoja na mtaji mdogo kwa Shirika hilo vinahitaji kutafutiwa ufumbuzi.

(vi) Ufanisi wa TARURA katika kubuni, kuendeleza, kukarabati na kutengeneza Mtando wa Barabara Mijini na Vijiji una manufaa kwa Wananchi. Hata hivyo, ufanis wa shughuli za TARURA unakwamishwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

❖Ufinyu wa Bajeti,

❖Mtando wa Halotel ambao unatumia Teknolojia ya 3G kufanya kazi taratibu hivyo kuchangia ucheleweshaji wa kuchakata taarifa za Ankara na kusababisha ankara kutolipwa kwa wakati na nyingine kutolipwa kabisa, jambo linalosababisha kupotea kwa baadhi ya mapato ya Serikali,

❖ Ukarabati wa barabara kufanyika kipindi cha masika bila kuzingatia majira katika maeneo husika,

❖Mfumo wa manunuzi ya vifaa kufanyika Mkoani badala ya Halmashauri

❖Kuchelewa kwa taratibu za manunuzi hali inayoongeza ghamama na kuathiri ufanikishaji wa matarajio ya Wananchi kwa wakati ; na

❖Mikataba kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Changamoto hizi zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuleta tija na ufanisi wa TARURA.

(vii) Utekelezaji wa Miradi ya kimkakati katika Halmashauri zilizofanikiwa, umejenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora kwa Wananchi, jambo linalofaa kuigwa na Halmashauri nyingine. Hata hivyo, changamoto ya Mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za Kimkakati kutotoa fursa sawa kwa Halamashauri zote kunakwamisha utekelezaji bora wa Mkakati huu hivyo inahitaji ufumbuzi.

### **3.3 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Utaratibu wa kuchunguza tabia na mwenendo wa Viongozi wa Umma kwa lengo la kukuza na kusimamia viwango vyaa maadili unafaa kuendelea ili kuendeleza imani ya Wananchi kuhusu uandilifu wa Viongozi wa Umma. Hata hivyo, kukosekana kwa Ukomo wa kutoa Tamko la mwisho wa kutumikia Wadhifa wa Kiongozi wa Umma ni jambo linalohitaji kupatiwa ufumbuzi.

(ii) Utendaji wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha Ustawi wa Utawala Bora na kuondoa rushwa nchini. Kwa sababu hiyo, changamoto zinazoikabili TAKUKURU zinatafaa kupatiwa utatuzi.

(iii) Hatua iliyofikiwa na Serikali katika utekelezaji wa Serikali Mtandao (e-GA) kwenye maeneo ya Sera, Sheria, Miongozo na Usimamizi pamoja na utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA ni jambo la kupongezwa. Hata hivyo, tatizo la baadhi ya Taasisi za Umma kuanzisha Mifumo ya kukusanya mapato bila kushirikisha Mamlaka ya Serikali Mtandao ni jambo linalohitaji kutatuliwa.

(iv) Uimirishaji wa Mifumo ya TEHAMA kwenye Sekratarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma imechangia kuiwezesha Taasisi hiyo kufanikisha azma ya Serikali ya kupata Watumishi wenye sifa, ujuzi na haiba stahiki. Hata hivyo, tatizo la upatikanaji

wa Wahitimu wenye ubora wa elimu katika Soko la Ajira ni tishio kwa mafanikio ya azma ya Serikali.

(v) Elimu iendelee kutolewa kwa Umma ili kuukumbusha Umma juu ya kuchukua tahadhari dhidi ya watu wanaotumia vibaya teknlolija ya TEHAMA kurubuni Wananchi.

(vi) Juhudi za Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka ya Taifa katika uhifadhi wa nyaraka ambazo ni urithi andishi wa Taifa letu zinapaswa kuungwa mkono. Aidha, changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa Idara hii inaathiri kasi ya kuhifadhi nyaraka kidijitari pamoja na usalama wa nyaraka hizo.

(vii) Baadhi ya Kaya maskini kutoingizwa katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, linaleta doa kwa kazi nzuri inayofanywa na TASAF

(viii) Uchakavu wa Madarasa yaliyojengwa katika Awamu ya Pili unatakiwa kutafutiwa ufumbuzi.

### **3.1 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, Hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu inahusu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati hii kwa kipindi cha Februari, 2021 – Februari, 2022. Taarifa hii imebainisha matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kuonesha mafanikio na changamoto zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia muundo wa hoja zinazowasilishwa Bungeni, ulioelezwa katika Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kwa namna itakayowezesha Bunge kuamua kama ifuatavyo:-

#### **3.1.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**(i) Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali**

**KWA KUWA**, lengo la Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari ili kuweka mazingira bora ya kufundisha na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kujifunza limekwamishwa na Wakandarasi Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) walioshindwa kukalimisha ujenzi kwa wakati,

**NA KWA KUWA**, Kutokamilika kwa ukarabati huo kunachalewesha nia ya kuboresha mazingira ya Walimu na Wanafunzi na kuzuia mafanikio ya juhudhi za Serikali kuongeza morari kwa Wanafunzi kujifunza na Walimu kufundisha,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, utaratibu wa kupata Wakandarasi uwe ni wa ushindani, TBA wasitumike kuwa Wakandarasi pekee katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali, bali utumike utaratibu wa kushindanisha Makandarasi au kwa kutumia "Force Account" pale inapobidi ili kupunguza gharama za ukarabati na kuongeza ufanisi katika utekelezaji.

**(ii) Utaratibu wa Halmashauri nchini kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa makundi maalumu**

**KWA KUWA**, imebaikina kwamba hakuna Mfumo madhubuti wa kudhitibi Uendeshaji na usimamizi wa fedha za asilimia kumi (10%) katika Halmashauri;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inazuia mafanikio ya mpango huo katika kuboresha hali ya maisha na Usatawi wa Wananchi katika maeneo ya Halmashauri nchini,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Serikali kwa kutumia Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) kutengeneza Mfumo madhubuti utakaozungumza na kuratibu taarifa za ukopeshaji, urejeshaji pamoja na kutambua Vikundi vinavyokopa. Vile vile Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuleta Marekebisho ya Sheria na Kanuni ili Mfuko huu uweze kukidhi mahitaji ya Makundi yote.

**(iii) Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

**KWA KUWA**, kukosekana kwa Sheria inayosimamia Usafiri wa Umma Mijini inaathiri shughuli za uendeshaji wa Mradi wa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam na kuzorotesha huduma ya usafiri inayotolewa na Mradi huo;

**NA KWA KUWA**, kuzorota kwa huduma hiyo kutokana na ombwe la kimfumo ni kikwazo kwa juhudzi za Serikali kuboresha huduma ya usafiri Jijini Dar es salaam,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Serikali iandae Muswada wa Sheria utakaoweka Mfumo mzuri wa kisheria unaosimamia Usafiri wa Umma Mijini.

### **(iv) Uendeshaji wa Masoko Nchini**

**KWA KUWA**, kujitokeza kwa Walangunzi wanaopangisha Vizimba vyatia biashara kwenye maeneo ya Masoko yanayojengwa na Halmashauri ni jambo linaloongeza gharama kwa Wafanyabiashara,

**NA KWA KUWA**, kuongezeka kwa gharama hizo kunachangia kupunguza uwezo wa Wafanyabiashara kupanga katika Vizimba, hali inayosababisha kuzagaa kwa uuzaaji na ununuaji ndani ya Halmashauri pamoja na kupotea kwa mapaton ya Serkali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Serikali iweke utaratibu madhubuti kisheria utakaobainisha ufanyakikazi wa wahusika wote wakiwemo Watu wa Kati pamoja na kubainisha bei elekezi ya upangishaji wa Vizimba vyatia Sokoni.

### **(v) Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**KWA KUWA**, mtaji mdogo kwa Shirika la Masoko Kariakoo unasababisha uwezo mdogo wa Shirika hilo kutekeleza majukumu yake ikiwemo kudhibiti na kusimamia Masoko na miradi yake,

**NA KWA KUWA**, Uwezo huo mdogo pamoja na upungufu uliopo katika Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo, vinaathiri dhima ya Shirika hilo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) Serikali iliongezee mtaji Shirika hilo ili limudu majukumu yake kikamilifu na kuchangia pato la Taifa na Ustawi wa maisha ya Wananchi;
- ii) Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo ili kusahihisha upungufu katika Sheria hiyo;

### **(vi) Wakala ya Barara Vijijini na Mijini**

**KWA KUWA**, kasi ndogo ya Mtando wa Halotel inayotumia teknolojia ya 3G na ambayo inatumwa na Mfumo wa TeRMIS wa TARURA katika ukusanyaji wa ada za maegesho ya magari, inasabisha ucheleweshaji wa taarifa za Ankara na kupotea kwa mapato ya Serikali,

**NA KWA KUWA**, tatizo hilo kwa pamoja na changamoto ya Mikataba ya Wakandarasi kutotekelawa inavyostahili, ufinyu wa bajeti na ujenzi wa barabara kutozingatia majira inakwamisha dhamira ya TARURA kufanikisha Usanifu, Ujenzi na Ukarabati wa barabara Vijijini na Mijini,

### **KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba:-

- i) Serikali itafute utaratibu endelevu utakaowezesha TARURA kupata fedha za kutosha ili iweze kutekeleza kazi zake za kukarabati na kujenga barabara mpya.
- ii) Serikali iiwezeshe Wakala wa Barabara Vijijini kuwa na Mtando wenye nguvu na kasi kubwa ili kuwezesha Mfumo wa malipo kuwa na ufanisi na tija;
- iii) TARURA isimamiwe kuhakikisha kuwa Mikataba ya Wakandarasi inatekelezwa kwa wakati na inavyostahili;
- iv) Mfumo wa manunuzi wa TARURA ushushwe kwenye ngazi ya Halmashauri badala ya kufanyika Mkoani ili kurahisisha utendaji kazi na kupunguza gharama;

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati katika Halmashauri nchini**

**KWA KUWA**, Mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za Kimkakati hautoi fursa sawa kwa Halmashauri zote na kuwa na usimamizi hafifu katika ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya mapato;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaathiri ufanisi katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuongeza mapato na kuwezesha ustawi wa Wananchi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kuwa TAMISEMI iharakishe kufanya marekebisho katika Mwongozo utakaotoa fursa sawa kwa Halmashauri zote nchini ili kukidhi azma ya Serikali ya kuongeza mapato ya Halmashauri na kuwezesha ustawi wa Wananchi.

**KWA KUWA**, kumekuwa na Miradi ya Kimkakati inayojengwa na Halmashauri (Masoko) ambayo haifanyi vizuri kama iliyokusudiwa;

**NA KWA KUWA**; Miradi hiyo haileti tija iliyokusudiwa ya kuleta maendeleo kwa Wananchi na kuongeza Mapato ya Halmashauri kwa maendeleo ya Wananchi na Nchi kwa ujumla,

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaishauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili miradi inayojengwa iendane na hali halisi ya uhitaji wa Wananchi.

**3.1.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

**(i)Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

**KWA KUWA**, kukosekana kwa Ukomo wa kutoa Tamko la mwisho wa kutumikia Wadhifa wa Kiongozi wa Umma ni jambo linalosababisha ugumu katika kusimamia masharti hayo ya Kisheria,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaleta ugumu kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kusimamia matakwa hayo ya Kisheria;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili kuweka Ukomo wa Viongozi wa Umma kuwasilisha Tamko la mwisho.

### **(ii) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU)**

**KWA KUWA**, TAKUKURU ambayo ni miongoni mwa Taasisi za Utawala Bora na Uwajibikaji nchini, inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, uchache wa Watumishi, upungufu wa vitendea kazi pamoja na upungufu katika Sheria iliyoanzisha Taasisi hiyo,

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo zilizobainishwa zinaathiri ufanisi wa TAKUKURU katika kufanikisha lengo la Serikali la kuimarisha Utawala Bora, Uwajibikaji na Maadili katika Utumishi wa Umma;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba:-

- i) TAKUKURU iwezeshwe zaidi kibajeti ili ifanikishe utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria;
- ii) Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria kwa lengo la kuondoa upungufu katika Sheria hiyo.
- iii) TAKUKURU ijikite zaidi katika kuzuia rushwa badala ya kupambana wakati matendo ya rushwa yameshafanyika.

### **(iii) Wakala ya Serikali Mtandao**

**KWA KUWA**, Wakala ya Serikali Mtandao uliyoundwa kwa madhumuni ya kusimamia Serikali Mtandao na kuratibu matumizi ya TEHAMA Serikalini, unakabiliwa na tatizo la baadhi ya Taasisi za Umma kutotumia Wakala huu na kuendeleza Mifumo tumizi isiyodhibitiwa wala kuratibiwa,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NA KWA KUWA**, baadhi ya Taasisi za Umma huendeleza Mifumo tumizi bila kuzingatia kikamilifu Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo, inakinzana na mantiki ya kuanzishwa kwa Wakala hii,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba Serikali:-

- i) Itoe Mwongozo thabiti kwa Taasisi zote za Umma zinazoanzisha program tumizi ikiwemo program za ukusanyaji wa mapato, zianzie kwa Wakala ya Serikali Mtandao;
- ii) Serikali Mtandao (e-GA) iimarishe na isimamie kikamilifu Mifumo mbalimbali iliyoanzishwa na iliyopo Serikalini na kwenye Taasisi zake ili kuondoa kasoro na dosari katika utendaji wa Mifumo hiyo kwa lengo la kuleta ufanisi;
- iii) Serikali izikumbushe Taasisi zote za Umma kuzingatia kikamilifu, Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kufanikisha azma ya kuratibu matumizi ya TEHAMA Serikalini;
- iv) Serikali Mtandao itengeneze Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zote za Umma, Vyama vya Ushirika, SACOSS na kutambua Wakulima nchini.

### **(iv) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

**KWA KUWA**, maendeleo ya TEHAMA yametoa nafasi kwa watu wanaoitumia vibaya teknolojia hiyo kuweza kughushi nyaraka za Serikali ikiwemo barua za Ajira, kutapeli baadhi ya waombaji kazi pamoja na baadhi ya wasailiwa wanaoomba Ajira kutumia simu katika usaili,

**NA KWA KUWA**, matumizi hayo mabaya ya TEHAMA yanaweza kuathiri azma ya Serikali kupata Watumishi wenye sifa, ujuzi na haiba stahiki kupitia michakato ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauria kwamba:-

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iongeze juhudi ya kuuelimisha Umma ili kuwanusuru watu dhidi ya utapeli na tatizo la kughushi katika mchakato wa Ajira;
- ii) Mafunzo ya mara kwa mara yatolewe kwa Watumishi wa Wekretarieti ya Ajira ili kuweza kuendana na teknolojia ya kisasa;
- iii) Serikali iiwezeshe Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuwa na Mfumo madhubuti wenyewe uhakika wa usalama wake.
- iv) Taasisi zote za Serikali na za umma zianze kutumia Mifumo mipyaya ufuatiliaji na utendaji kazi;

### **(v) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

**KWA KUWA**, Maendeleo ya kazi nzuri ya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa yanakwamishwa na tatizo la ufinyu wa Bajeti,

**NA KWA KUWA**, Mkwamo huo unaathiri azma ya kuimarisha na kuendeleza uhifadhi wa nyaraka ambazo ni urithi andishi wa Taifa letu,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iwezeshwé zaidi kibajeti ili ifanikishe kazi muhimu ya kuhifadhi nyaraka na kuimarisha usalama wa nyaraka zinazohifadhiwa.

### **(vi) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**KWA KUWA**, Kuna Walengwa ambao bado hawajaweza kupata namba/vitambulisho vya Taifa, na hivyo kushindwa kufungua akaunti, kusajili simu au kuhakikiwa na kupokea ruzuku kwa njia ya Mfumo wa malipo wa Kielektroniki,

**NA KWA KUWA**, Hali hii inawasababishia Wlengwa kushindwa kupokea ruzuku hiyo kwa wakati, jambo linalokwamisha juhudi za kuwawezesha Wananchi kujinasua kiuchumi,

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba, Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa Wanufaika hao wanapatiwa Namba/Vitambulisho vya Taifa ili kuwawezesha kupata huduma muhimu pale inapobidi ikiwemo kupokea ruzuku kwa njia ya Kielekroniki ili waweze kujikwamua kiuchumi.

**KWA KUWA TASAF** imefanya vizuri sana katika miradi ya kunusuru Kaya Maskini Zanzibar;

**NA KWA KUWA** hali hiyo imeboresha huduma za Afya, Elimu na kuwainua Walengwa kiuchumi;

**KWA HIYO BASI:** Bunge linashauri kwamba, TASAF iendelee kupatiwa fedha za kutosha ili iweze kuwakomboa Wananchi wengi kiuchumi na kuboresha huduma katika Jamii ikiwa ni pamoja na kukarabati Madarasa ya zamani..

### **SEHEMU YA NNE**

#### **4.0 HITIMISHO 4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika nafasi hii ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakuombea afya njema na tunaahidi kukupa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu ya kuisimamia na kuishauri Serikali kwa lengo la kuwalettea Watanzania maendeleo yenye tija, huku tukizingatia Sheria, Taratibu na Dhana nzima ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, nitoe shukrani za dhati kwa Mhe. Azan Zungu Mb, Naibu Spika kwa kuaminiwa na kuchaguliwa katika nafasi hii ya kukusaidia Mheshimiwa Spika katika kuongoza na kusimamia Mhimili wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika

kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Mwaka Mmoja uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwashukuru Mawaziri wote waliohudumu chini ya Ofisi Rais kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb), - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb), - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Deogratius John Ndejembia (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais – Utumishi na Utawala Bora, Mhe. David Ernest Silinde (Mb) na Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb), - Manaibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Aidha, niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais wakiongozwa na Makatibu Wakuu Prof. Riziki Silas Shemdoe – Ofisi ya Rais- TAMISEMI, Dkt. Laurean Ndumbaro Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ndg. Kusiluka, na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi ambazo Kamati inazisimamia. Natambua kuwa ushirikiano wao ndio uliofanikisha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wapya walioteuliwa hivi karibuni kusimamia majukumu ya Ofisi ya Rais, Mhe. Jenista J. Mhagama Mb, Waziri - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mhe. Innocent L. Bashungwa Mb, Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kamati yangu iko tayari kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha Mawaziri hawa wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati.

**Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo: -**

1. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb - Mwenyekiti

## ***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- |   |   |              |
|---|---|--------------|
| 2. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb         | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb        | - | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb     | - | -Mjumbe      |
| 5. Mhe. Dkt.Thea Medard Ntara, Mb       | - | Mjumbe       |
| 6. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb   | - | Mjumbe       |
| 7. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb         | - | Mjumbe       |
| 8. Mhe. Rehema Juma Migila, Mb          | - | Mjumbe       |
| 9. Mhe. Dkt Alice Karungi Kaijage, Mb   | - | -Mjumbe      |
| 10. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb   | - | -Mjumbe      |
| 11. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb     | - | Mjumbe       |
| 12. Mhe. Michael Costantino Mwakamo, Mb | - | Mjumbe       |
| 13. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb      | - | -Mjumbe      |
| 14. Mhe.Mwantakaje Haji Juma, Mb        | - | - Mjumbe     |
| 15. Mhe. Omary Issa Komba, Mb           | - | Mjumbe       |
| 16. Mhe. Mwantum Dau Haji, Mb           | - | Mjumbe       |
| 17. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb       | - | Mjumbe       |
| 18. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb       | - | Mjumbe       |
| 19. Mhe. Seif Salum Seif, Mb            | - | Mjumbe       |
| 20. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb   | - | Mjumbe       |
| 21. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamisi, Mb    | - | Mjumbe       |
| 22. Mhe. Tunza Issa Malapo              | - | -Mjumbe      |
| 23. Mhe. William Vagimembe Lukuvi, Mb   | - | - Mjumbe     |
| 24. Mhe. Prof. Palamagamba J.A. Mwaluko | - | Mjumbe       |

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumwamini na kumteua Mjumbe mwenzetu wa Kamati Mhe Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana Mb, kuwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Tunampongeza sana Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana kwa nafasi hiyo, tunamwombea utendaji kazi uliotukuka.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, ndc, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, ndc, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili.

Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Angelina L. Sanga na Ndg. Sikudhani A. Mbinga, wakisaidiwa na Ndg. Paulina Mavunde, kwa umakini katika uratibu na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

#### **4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelawa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wa wake pamoja na maoni ya jumla na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja **kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Abdallah Jafari Chaurembo, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA**

14 Februari, 2022

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti. Hoja imeungwa mkono, nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa kuchangia, kwa hiyo ninaanza na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, baadaye Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae. Upande wa CCM wote dakika tano tano.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuanza kuchangia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nijielekeze kwenye kuipongeza Serikali ya mama Samia kwa kazi nzuri ambayo imefanya ya ujenzi wa madarasa, vituo vya afya na zahanati. Lakini kuna kazi kubwa ambayo inaendelea chini ya TARURA. Pamoja na kazi hii kubwa, lakini pia tunaona *impact* ya hii mikopo ya asilimia 10 kwenye halmashauri zetu. Ni kazi nzuri ambayo inahitaji uungwaji mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo fedha ambazo zinakwenda kwenye mikopo kwa ajili ya makundi maalum ya hiyo asilimia kumi ni nyngi sana. kwa mfano kwenye bajeti ya mwaka huu ni zaidi ya bilioni 69 na kitu ambazo zinakwenda kwenye mikopo kwa ajili ya makundi haya maalum. Fedha hizi ni nyngi, ni vizuri tuka-review uendeshaji na usimamizi wa fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kujua ni kiasi gani ambacho kipo kwenye mikono ya vikundi ambavyo vimekopeshwa; ni kiasi gani ambacho kimerejeshwa na nini mpango endelevu wa hizi fedha? Kwa sababu hatuwezi kuendelea kutoa fedha hizi kwa maisha yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujue ni kiasi gani ambacho kipo ambacho kinaweza kikawa mtaji wa kutosha tukaingiza kwenye *revolving fund* ikazunguka yenye bila ya kuendelea kuchota tena kwenye bajeti kuu. Kwa hiyo ni vizuri tukajielekeza namna bora ya kuangalia uendeshaji wa hizi fedha za asilimia kumi ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, halmashauri zetu kimsingi zinahitaji mipango Endelevu, hasa ujenzi wa miundombinu ambayo inaweza kwenda kutoa ajira Endelevu kwa wananchi wetu. Ukiangalia reli ambayo inatengenezwa ya SGR kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, Makutupora, unaweza kuona mashimo makubwa ambayo yanatumika kama chanzo cha kokoto za ujenzi wa reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashimo haya makubwa yanaweza sana kutusaidia kutengeneza mabwawa ambayo yanaweza kwenda kutumika kwa ajili ya shughuli za uvuvi, mifugo na kilimo kwa ajili ya umwagiliaji na ika-save fedha nyingi sana za Serikali. Ninapenda kujua ni kiasi gani cha mashimo ambayo yamechimbwa ambayo tunaweza tukabadiilisha kuwa mabwawa na ikawa sehemu nzuri ya kutengeneza miundombinu kwa ajili ya wavuvi, wakulima na umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili linahitaji mahusiano ya karibu kati ya halmashauri zetu (TAMISEMI), Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji na huku kwenye mifugo. Kazi nzuri ambayo inafanyika katika Serikali za Mitaa inahitaji mahusiano ya karibu kati ya TAMISEMI, Wizara ya Kilimo na Mifugo ili kuleta matokeo chanya kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ambayo ipo sasa hivi na mahusiano yaliyopo hayatoshi kwa sababu ukiangalia idara ya mifugo kwenye halmashauri zetu, ukiangalia uvuvi kwenye halmashauri zetu ukiangalia kilimo kwenye halmashauri zetu,haziakisi umakini katika suala zima la kuhakikisha kwamba sekta hizi zinakwenda kutoa ajira ya maana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; tutengeneze mfumo madhubuti ambaao Wizara hizi zinaweza zikakaa pamoja kuona namna bora ya kuboresha masoko na biashara zetu. Kwa mfano unaweza ukaangalia suala zima la ghala au stakabadhi ya ghala jinsi gani ilivyo *sensitive* katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado hatujui *role* ya halmashauri katika usimamizi wa maghala; hatujui *role* ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika usimamizi wa maghala; hatujui *role* ya Wizara ya Kilimo katika usimamizi wa maghala. Tunahitaji kujua nani ambaye ana dhamana ya kusimamia maghala na biashara, hasa katika suala zima la bidhaa na usambazaji wake.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kadhia ambayo imetokea kwenye soda inaweza ikatokea kwenye pembejeo, inaweza ikatokea kwenye viuatilifu, inaweza ikatokea hata katika usambazaji wa mazao. Hii *scarcity* ama *deficit* inaweza ikawa *created* kwa sababu hatuna taasisi ambayo inakwenda kusimamia maghala. Tunahitaji kuwa na sheria ambayo inatoa majukumu ya nani anakwenda kusimamia na kuratibu haya maghala.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Londo, tunaendelea na Mheshimiwa Edward Olekaita baadae Mheshimiwa Rashid Shangaza ajlandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu ya muda, niwapongeze Mawaziri wote ambao wanakuja kwenye Kamati yetu, wote, kuanzia Ofisi ya Waziri Mkuu, *Chief Whip, Attorney General*, Waziri wa Sheria, Ofisi ya Waziri Mkuu mambo ya Ajira, Muungano – wote kwa ujumla wenu, kwa kazi kubwa ambazo kwa kweli mmefanya kwa utekelezaji wa kazi katika Wizara zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Katiba na Sheria kwa muda wa mwaka mmoja imeweza kufanikiwa kurekebisha sheria karibu 58, siyo kazi ndogo sana; utungwaji wa sheria siyo kazi ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye sheria hizo, kati ya sheria maarufu sana ambazo tumebadilisha ni kuruhusu Kiswahili kitumike kwenye mahakama zetu na kutafsiri sheria zetu ziende kwa Kiswahili. Kwa kweli kati ya sheria ambazo

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

nazikumbuka na mabadiliko mazuri sana kwa Watanzania ni kuruhusu Kiswahili kianze kutumika ili watu waanze kufuatilia mashtaka kwenye kesi za mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonifurahisha zaidi ni kwamba llani ya Chama Cha Mapinduzi baada ya sisi kusema kwamba tubadilishe sasa sheria ziende kwa Kiswahili, Wizara ya Katiba na Sheria walitakiwa kwa mujibu wa ilani yetu wawe wametafsiri sheria 157. Lakini kwa kasi yao wamerekebisha na kutafsiri sheria 208; hongereni sana. kasi hii ikiendelea mtakipa Chama Cha Mapinduzi heshima kubwa sana kule. Kama ilivyo kwenye ilani, ukurasa wa 167. Na ninaomba ninukuu: -

*"Kuungeza uelewa wa wananchi kuhusu sheria mbalimbali kwa kutafsiri sheria 157 kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *big up*. Ninyi mmevuka lengo. Najua mna kazi kubwa sana, kwa sababu hata mnatakiwa kutafsiri *subsidiary legislation* na zile nyingine karibu 39,000; mtakuwa na kazi kubwa sana. kwa hiyo, naamini Wabunge watawaelewa wakati wa bajeti, mkileta bajeti hapa mpewe pesa nyngi muendelee kuchapa kazi kubwa zaidi. Kwa hiyo kwa miaka mitano ninyi mmeshaturahisishia kazi. Sheria zile *principal* zipo karibu 449, ninyi meshavuka kabisa; hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara ya Katiba na Sheria ilitakiwa, kwa mujibu wa llani yetu, kuboresha majengo ya mahakama. Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria tulipata nafasi ya kutembelea mikoa mbalimbali kuona miradi ya mahakama; tumeanza Kongwa, tumekwenda Morogoro, tumekwenda Njombe, tumekwenda Dar es Salaam, tumekwenda Arusha na leo tumekwenda Dodoma kuona jengo kubwa la mahakama, *Judiciary Square* ambayo inasadikiwa litakuwa jengo bora kuliko *Central and Southern Africa*, na Waheshimiwa Wabunge tunawakaribisha. Wizara ya Sheria wanatuambia mwaka huu Desemba, watafungua hili jengo. Jengo zuri halijawahi kutokea; hongereni sana. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mabadiliko mengine ambayo ni muhimu sana ni mabadiliko ya kuwaruhusu mawakili kwenda kwenda kwenye mahakama za mwanzo. Hii siyo tu inafungua fursa ya ajira lakini inawafanya wananchi wapate huduma za uwakilishi kwenye vijiji vyao; *excellent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini kati ya sheria zilizobadilika ni kuweka *break ile nolle prosequi* na *amicus curiae* kwenye mambo ya sheria, itaongeza, na itapunguza mashtaka yale ambayo yanawasumbua wananchi sana. na vilevile kusema upelelezi ukamilike ndiyo tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema hivi...

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho Mheshimiwa Olekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sentensi moja. Na kwa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria mna kazi maalum ya kufanya, naomba niseme Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 29, alipokuwa akihitubia *UN*, na mimi nasema *he for she*; alisema yafuatayako: -

*"Aware that being passionate about gender equality is not sufficient, my government is reviewing policy, legal framework in order to come up with actionable, measurable plans to ensure economic empowerment for women but also aspects pertaining to gender equality and gender parity."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlete sheria hizi tuzibadilishe. Nakushukuru sana, naunga mkono hoja asilimia 100; ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olekaita, sasa hivi ni zamu ya Mheshimiwa Rashid Shangazi na baadaye Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa nafasi hii. Kabla ya kusema lolote

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

nipongeze kwanza Kamati zote mbili kwa taarifa ambazo kimsingi ndizo kazi tunazozifanya katika Kamati na ndizo kazi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo machache ya kutoa mchango wangu katika Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Ninaomba nishauri jambo; tumepokea miradi mingi sana ya maendeleo katika maeneo yetu kupitia Serikali za Mitaa lakini kuna changamoto kubwa kwamba wataalam wetu walioko katika Wizara hii ya TAMISEMI wamekuwa wakigawa mafungu haya kwa ulingano, kwa maana ya kwamba kama tunajenga shule ya msingi au darasa la shule ya msingi ama sekondari, tunaletewa pesa ambayo inafanana nchi nzima, lakini mazingira ya nchi nzima hayafanani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wilaya za Lushoto, Makete, Kyerwa nadhani na Tarime, yale maeneo ambayo zaidi yanalinwa kahawa ni maeneo ambayo ni ya milima. Ukiwapa pesa sawa na sehemu ambayo ni tambarare maana yake haziwezi zikawa na tija ile iliyokusudiwa. Kwa hiyo, tuwaombe sana wataalam wetu waangalie haya wakati wanapanga mipango hii ya Serikali wazingatia jiografia ya baadhi ya maeneo ili tusipewe pesa ambayo inalingana na maeneo mengine hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine ambalo ningependa kutoa mchango wangu ni eneo la mapato ya halmashauri kwa maana ya mapato ya ndani asilimia 20 ambazo zinapaswa kurudi kwenye Serikali za Vijiji. Fedha hizi zilikuwa kipindi cha nyuma wakati halmashauri nyingi zilikuwa zinawajibika kuwalipa Madiwani, zilikuwa hazipatikani vizuri kurudishwa katika vijiji. Sasa kwa kuwa Serikali imebeba mzigo wa kulipa posho za Madiwani tungependa kuona sasa asilimia 20 ikisimamiwa kurudi kwenye Serikali za Vijiji. Maana huko ndiko ambako miradi hii ya Serikali inakwenda kutekelezeka na wasimamizi wakubwa ni Wenyeviti wa Serikali za Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa na ambao wenyewe wanachaguliwa kama sisi, wanakuwa hawapati ruzuku yo yote kutoka Serikalini. Hata hivyo, tunaamini kwa mwongozo uleule uliopo ambao mwanzoni ulikuwa unatumika kulipa Madiwani na sasa dhamana ya Madiwani imekwenda Serikali Kuu hii asilimia 20 basi ni vyema ikarudishwa kwenda kulipa Wenye viti kwa msisitizo na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulichangia katika mchango wangu ni suala la asilimia 10 ya fedha hizi za halmashauri ambazo zinakwenda kwenye Mfuko wa Vijana na Wanawake na zile asilimia mbili kwa Wenye Ulemavu. Eneo hili bado lina changamoto, nipo katika Kamati ya LAAC ambako mara kadhaa tumekuwa tukizihoji halmashauri. Unaona mara zote fedha hizi zinaonekana zinaendelea tu kutoka Japokuwa kwa tafsiri Mfuko huo unaitwa *Revolving Fund*, ni fedha ambayo inatakiwa itoke kisha irudi, lakini mara zote tukija tunaona tu kwamba zinatoka zile zinazorudi halmashauri zimekuwa na usimamizi hafifu katika kusimamia sheria na kufanya zile fedha zirudi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ningependekeza, kwamba hili jambo kwanza msisitizo uwepo kwenye *Revolving Fund* kwamba fedha zikishakopesha zirudi. La pili, Serikali itazame *model* nzuri zaidi ya kuja na jambo hili. Sasa hivi halmashauri zote zinatenga sawa asilimia 10, lakini hazilingani mapato, nadhani wangetumia *model* ya Mfuko wa Jimbo ambao unatumia *population*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli inawezekana Wilaya ya Lushoto ina *population* kubwa lakini mapato yake ni madogo na kuna wilaya nyingine ni ndogo, lakini mapato yake ni makubwa. Sasa huu wingi wa vijana ukawa unatofautiana, hivyo wa Lushoto pamoja na wingi wao wakapata kidogo kwa sababu mapato yao ni madogo. Kwa hiyo ni lazima kuja na mpango wa ku-centralize haya mapato yote labda katika Mfuko Maalum halafu sasa yaende kwenye makundi haya ya vijana kwa kuzingatia hata fani ambazo wanasona katika Vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan, sasa hivi tuna vyuo ambavyo wame-*graduate* mainjia wengi, tunaweza tukaanzisha kampuni ndogo za mainjinia, wakapelekwa katika miradi midogo midogo labda ya barabara, ya usambazaji umeme vijijini, ya maji na kadhalika kwa kupitia Mifuko hii na baadaye tunaweza tukaiona tija kubwa zaidi kuliko ambayo tunayoiona sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja Kamati zote mbili. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Rehema Migilla ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mwenyekiti kwa wasilisho lake zuri, lakini pia niimpongeze Serikali kwa maana ya Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, hasa hasa Waziri wa TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuchangia ambayo yamejikita kwanza kwenye upungufu wa wafanyakazi. Kwanza tuipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya ya kujenga vituo vya afya lakini pia kuongeza ujenzi wa madarasa katika sehemu mbalimbali za nchi hii. Hata hivyo, changamoto kubwa ambayo tumekuwa nayo ambayo tunaipata hadi sasa hivi ni wimbi kubwa la vijana kukosa ajira ambapo mimi kama Mbunge ningependa kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watu wengi kustaaifu, lakini pili kumekuwa na wenzetu ambao wanafariki na kutangulia mbele ya haki. Hawa wote tungetamani nafasi zao ziwe zinajazwa kwa wakati, kwa sababu wanakuwa wako kwenye *payroll* ya Serikali. Hii ingeweza kusaidia kuendelea kupunguza *gaps* liliopo la watumishi kwenye nchi yetu ambalo limekuwa ni kubwa. Kuna watu ambao wamemaliza toka miaka 2012, 2013, 2014 hawajaajiriwa hadi

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanakuwa wazee, wamekosa ajira. Kwa hiyo, tungeiomba Serikali na ningeishauri Serikali iijtahidi kutoa vibali mapema kwa hizi *gaps* ambazo zinakuwa zipo za watu ambao wamestaafu na wangine wametangulia mbele ya haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine, ni kwenye suala la fedha za miradi. Kwanza tuipongeze sana Serikali, mama yetu anaupiga mwingi sana. Mama Samia anaupiga mwingi sana kwenye ujenzi wa miradi kwenye nchi hii. Unaweza ukaangalia kwa asilimia 100 kama siyo 90 na kitu halmashauri zote nchini zimepata fedha za maendeleo za bajeti ambazo walikuwa wameomba, ni kitu ambacho hakijawahi kutokea kwa miaka mingi toka tumepeata uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambayo tunaipata, kwenye uwiano wa kugawa fedha hizi. Watu walioko Makete, Kiteto, Nyamagana kule Mwanza, Musoma, Mbanga na watu waliopo maeneo mbalimbali anapewa milioni 20 ajenge darasa, wakati huo huo hiyo milioni 20 anapewa mtu aliyopo Dar es Salaam ajenge darasa. Halafu tunategemea hawa watu wote wawe na darasa sawa la Dar es Salaam na la Makete kule Ipepo, na la Makete kule Matamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokuja kujitokeza, watu waliopo kule mikoa ya mbali kama Kigoma, Makete Wilayani wanahangaika kuhakikisha wana-meetkile kiwango ambacho Serikali imetaka darasa likamilike, lakini si kwa zile fedha ambazo muda mwingine zimetolewa na Serikali, wanakwenda kuingia hadi mifukoni mwao kuhakikisha wanatekeleza lile jambo ambalo Serikali inataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetumia mfumo ambao *EWURA* wanavyofanya kwenye kugawa mafuta. Bei ya mafuta Dar es Salaam ni tofauti na bei ya mafuta iliyoko Mwanza. Ndivyo ambavyo tunatakiwa tufanye hivyo hata kwenye miradi hii ya Serikali, angalau tungetambua kwamba

Zone hii ya Mwanza au *Lake Zone* au Zone ya Mbeya, ujenzi wa madarasa siyo milioni 20 kwa darasa moja, ni milioni 25. Wangefanya hivi ingeweza kusaidia kwa watumishi na wafanyakazi wetu waliopo kule chini, kwa sababu wana-suffocate, wanapata wakati mgumu, kuhakikisha kwamba wana-meet kile ambacho Serikali inataka, lakini usawa huu ungeondolewa ili kuweza kuwasaidia ndugu zetu ambao wapo huko wanahangaika na kutekeleza miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ningeomba sana watumishi walizingatie, wanateseka sana Watendaji wa Kata, wanabana sana na Wakurugenzi kuhakikisha kwamba hii miradi inakamilika kwa uwiano wa kugawa fedha kwenye majimbo yote nchini, wangetenga kwa *zone* ingetusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho, ni kwenye suala la Sekretarieti ya Maadili ya Utumishi wa Umma. Hii Sekretarieti imeanzishwa kwa sheria, ibara ya 132 kwenye Katiba yetu, ndiyo ilianzisha hii Sekretarieti ya Maadili ya Umma. Changamoto ambayo tunaipata kwenye hii Sekretarieti ya Maadili ya Umma. Tumekuwa na changamoto ya Viongozi wengi na watumishi wengi wa Serikali kutokuwa na maadili ya umma kama ambavyo tunatoka kwenye sheria, lakini hii Sekretarieti imekuwa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majukumu yake wanasema, kuna mojawapo wanasema, Sekretarieti ya Maadili ya Umma inasema *to conduct investigation into allegations or complex against any public leader*. Sasa tumeanza kushangaa kwamba hadi anakwenda Rais anasema hadharani kwamba kiongozi huku amefanya moja, mbili, tatu, nne, tano au hadi watu waweke bango barabarani kwamba kiongozi huyu ana moja, mbili, tatu, nne, tano, lakini hii Sekretarieti ya Maadili ya Umma ilikuwa na kazi hiyo ya kufanya *investigation* kujua viongozi wapi wanafanya moja, mbili tatu ili achukuliwe hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna vijana ambao wanahangaika mahakamani kwa kesi mbalimbali, lakini kuna mambo yalikuwa wanayafanya hadharani na hii Sekretarieti

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ilikuwa kimya, lakini leo hao viongozi wanahangaika kwenye hayo mambo.

Kwa hiyo, nasema Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha kwamba Sekretarieti ya Maadili ya Watumishi wa Umma inafanya kazi kwelikweli kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa Wakurugenzi na wateuliwa wengine wa Rais ambao wamekuwa wakikiuka maadili na tunawaona wapo kimya na hii Sekretarieti ya Maadili ya Umma ipo kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ingefanya kazi vizuri, ingewasaidia hatu vijana ambao wanakua wajue kuna chombo ambacho kinafanya kazi kabla ya Mheshimiwa Rais kuchukua hatua. Hiki chombo ambacho kiliundwa na Sheria na ni chombo huru, kina uwezo wa kufanya kazi hadharani na watu tukaona tukajua nchi yetu ukikosea hiki unachukuliwa hatua hili, lakini sasa tumeona kwamba kumekuwa na ukimya huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo nikushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Festo. Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla baadaye atafuata Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu, lakini nikushukuru pia wewe kwa kunipatia nafasi ya kuchangia jioni hii. Nianze kwanza kwa kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati hizi mbili kwa mawasilisho mazuri. Nianze moja kwa moja kwa kwenda kwenye *point*.

Mheshimiwa mwenyekiti, leo nitajikita hasa hasa kwenye mambo mawili. Jambo langu la kwanza ni kwenye utengaji wa asilimia 10 kwa ajili vijana, wanawake na wenye ulemavu. Ni ukweli usiopingika kabisa hili suala la utengaji wa hizi fedha asilimia 10 liko kisheria. Hata hivyo, tunaona katika baadhi ya halmashauri nydingi utengwaji wa hizi fedha hauendi na unakwenda kwa kusuasua mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inajitokeza pale ambapo tunaona kuna baadhi ya vikundi vingi sana nya akinamama, vikundi nya vijana lakini nya wenyewe ulemavu kila siku wanakwenda kule halmashauri kufuatilia hawapati, kina mama wanasumbuka mno na isitoshe kuna baadhi wanatoka mbali mno. *Imagine* kama mimi halmashauri yangu ipo mbali na jimbo langu, kwa hiyo kila siku wanagharamika kwenda halmashauri kufuatilia lakini hawapati majibu. Hii inatokana na ukweli kwamba hivi vikundi vingi vinavyopewa hizi fedha ni vikundi nya watu binafsi. Watu wengi wanaopewa hivi vikundi *eitherni* viongozi wa vyama, lakini vikundi vingi ukivichunguza hivi wamiliki wa hivi vikundi ni watumishi wa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sasa, nataka nitoe ushauri ili takwa la hizi fedha ziwalenge walengwa kabisa. Moja ya ombi tunalomba Serikali kwanza iwe na *database*, kila halmashauri ituambie ni vikundi vingapi vimeomba, lakini ni vikundi vingapi vimepatiwa fedha na ni vikundi vingapi vimerejesha hizo fedha, tunataka tuzione.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwepo na ufuatiliaji; hawa Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo hawafiki kule kwenye vile vikundi matokeo yake kuna vikundi hewa vingi mno. Kwa hiyo, kuwepo na *model* ya ufuatilia ili tuvijue vikundi halisi ni vipi? Kwa sababu kama hawa wananchi ambao tunaishi nao vijana na akinamama hawapati, hivi vikundi vinavyopata ni nya wapi? Ina maana kuna vikundi hewa vingi ambavyo vinamilikiwa na watu. Kwa hiyo, uwepo huo wa ufuatiliaji na *data* zijulikane. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uendeshaji wa masoko yetu na kuungua kwa masoko. Masoko yetu kwa sasa tunapata taarifa kila siku yameungua, yameungua, yameungua, lakini hatuambiwi nini chanzo cha kuungua masoko haya. Hata huvyo, tunajua kabisa haya masoko yamegharimu fedha nydingi sana katika ujenzi wake. Tukiangalia tu mfano wa Soko la Ndungai, lile soko ni mionganoni mwa masoko yaliyogharimu fedha nydingi sana, lakini haya masoko hata uzalishaji wake kiukweli hauleweki na pamoja

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

na kwamba yanatumia gharama kubwa lakini bado yanaungua kila siku. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwanza ije na mpango, pamoja na kwamba inayajenga lakini yawe na mpango wa kuya-rescue haya masoko yetu kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali pamoja na kwamba inayajenga haya majengo, tunaambiwa tuweke *fire extinguishers* kila sehemu zinasaidia nini zile *fire extinguisher* wakati kila siku yale masoko yanaungua. Ningeshauri kila masoko basi ziwekwe zile *fire detectors* ili angalau hata kama kuna viashiria vya moto viweze kutoa ashirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapo hapo kwenye masoko, ningeweza kushauri Serikali kama inaweza inapofanya usajili wa hawa wafanyabiashara basi iweze kuweka na takwa la lazima la kila mfanyabiashara aweze kuwa na bima ya biashara. Hii bima ya biashara itawasaidia pale inapotokea majanga ya aina mbalimbali mfano pale inatokea moto. Tunaona wafanyabiashara wanawekeza mitaji yao mingi sana, wanakopa kwenye mabenki na sehemu mbalimbali ili kuendesha biashara zao. Linapotokea suala la moto soko limeungua, wanaambiwa tu mabenki wawaongezee muda wa kulipa *so what?* Wakati watu wameshaweka mitaji yao na imepotea, kwa hiyo nafikiria suala la bima litakuwa ni mkombozi kwa hawa wananchi ili waweze kufanya biashara vizuri, lakini wawe na uhakika wa kulinda mitaji yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ameweza sasa kutuletea miundombinu ya elimu, maji na afya. Tumeona kwenye suala la UVIKO tumeletewa madarasa mengi sana, vituo vya afya lakini na kwenye miradi ya maji. Hata hivyo, huwezi kuwa unaongeza tu kitu bila ya kuangalia *population*, tumeongeza madarasa ya kutosha *well and good* lakini je, hawa watumishi ambao watakwenda kufanya kazi kule wapo wapi? Niiombe sasa Serikali pamoja na juhudhi hizi nzuri inazozifanya lakini iende sambamba na kuongeza watumishi katika hii miradi ambayo imeianzisha. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehema Migila. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na baadaye Mheshimiwa Salum Shaafi ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuchochea maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Nimesimama hapa nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria nami napaswa kuzungumza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kazi ambazo zilifanywa kwa mwaka mzima, napenda zaidi kuzungumzia taasisi ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inahusiana na masuala ya majanga ya usalama mahali pa kazi (*OSHA*) wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana. Pia Kamati ilibaini kwamba *OSHA* wana kila sababu ya kuongezewa watumishi kwa sababu watumishi walionao kwa sasa ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia pia kwenye suala zima la taasisi ambazo zinashughulika na majanga mbalimbali ikiwemo Zimamoto. Kamati imebaini kuwa wenzetu hawa wa Zimamoto bado kimsingi hawajajipanga vizuri, kwa sababu hawana vitendea kazi, lakini pia maeneo mbalimbali ambayo majanga yanatokea wanashindwa kufika kwa wakati. Basi tumeona ni vizuri sana sasa tuishauri Serikali, iweze kuwezesha maeneo hayo ili mwisho wa siku haya majanga ambayo yanatokea na yamekuwa yakiwa yanaathiri sana uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla; basi yaweze kusimamiwa vizuri na kuweza kuondokana na hiyo hali ambayo kimsingi huwa inaleta hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na umeme mpaka vijiji kule, umeme wa *REA* umekwenda

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mpaka vijijini tunaishukuru sana Serikali kwa kufanya kazi nzuri namna hiyo, lakini sasa umeme huu umekwenda vijijini. Kuhusiana na masuala ya majanga mbalimbali wananchi je, wamepewa mafunzo maalum kuhusiana na masuala ya umeme? Faida zake na hasara zake *incase* kama hawatautumia vizuri umeme, nani ametoa maelekezo haya? Basi tumeona ni vizuri kuishauri Serikali kwamba, iweke kipaumbele kwenye kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na suala zima la umeme ambao umekwenda mpaka kule vijijini chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la taasisi nydingine ambayo iko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, PSSSF. PSSSF wamefanya kazi nzuri sana, tulikwenda pale Moshi kukagua Kiwanda cha Viatu ambacho PSSSF wana asilimia 86 na Magereza wana asilimia 14 kwa maana ya ubia. Kazi wanayoifanya ni nzuri sana lakini bado kuna changamoto kubwa sana kwenye vile viatu wanavyovitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viatu wanavyovitengeneza ngozi yake ni ngumu sana. Kwa mfano kama unamnunulia mtoto kiatu, basi unaweza kukuta katika viatu pea nne ulizonunua ukaribuni na hicho ambacho kinatengeneza na kiwanda kile, ukakuta mtoto anapenda kuvali viatu vingine lakini kile anakiacha kwa sababu kile kiatu ni kizito. Pia bei zake *is not affordable* kwa wananchi wa kawaida. Kwa hiyo watakaonunua vile viatu ina maana ni wale watu ambao wana uwezo. Kwa hiyo sasa tumeshauri kwamba wenzeru hawa wajipange vizuri waweze kutengeneza viatu kuendana na hali ya sasa ili waweze kupata masoko ya watu wa kada tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani ya halmashari ni asilimia 10. Nimemsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumza sikusudii kurudia lakini nadhani nikazie hapo hapo. Haya mapato ya ndani nia ilikuwa ni kuwasaidia makundi mbalimbali kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi, lakini kwa sasa hivi tunapata mashaka huenda fedha hizi zinatumika vibaya. Kwa mfano; tumesikia maeneo mbalimbali na juzi nimeona kwenye mtandao, mdogo wangu

Jokate Mwegelo pale Temeke ameingiliwa na watu ambao kimsingi katika halmashauri ile unakuta Diwani mmoja ameweza kujiwezesha mpaka milioni 300 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Maana yake amekwenda ameunda vikundi vikundi hatimaye amekwenda kujiwezesha ye ye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya vikundi vile ambavyo vimepewa fedha yaani havina mahusiano ya ukaribu na halmashauri. Vikundi vingine viro mbali, ni nje ya halmashauri husika. Kwa hiyo, niombe CAGaende akakague katika halmashauri zote ili aweze kujiridhisha kuhusiana na hii fedha ambayo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani. Nia ni kumwezesha mwananchi ili aweze kujikwamua kiuchumi, lakini sasa inakuwa tofauti watu wanataka kujinufaisha wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie suala la Madiwani. Madiwani wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana kwenye maeneo husika, sisi tupo hapa Bungeni muda wote wako kule na wananchi. Kwa misingi hiyo, wanatakiwa kwa hali na mali tuwatetee ndani ya Bunge hili ili waweze kuongezewa posho kwa sababu kazi wanazifanya lakini pia hawana usafiri wa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine hasa wale Madiwani wa vijijini ambao kimsingi wanakuwa wanatoka kijiji fulani kwenda kijiji kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya machache, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline, tunaendelea na Mheshimiwa Salum Shaafi, baadae Mheshimiwa Michael Mwakamo ajiandae.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nami nitumie fursa hii kukushukuru wewe. Pia kipekee niipongeze Kamati yangu ya Katiba na Sheria kwa namna ambavyo inasimamia na kutekeleza majukumu yake ya Kikamati.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende katika mchango wangu mfupi kwa taarifa ambayo imewasilishwa mbele yetu. Mimi nitajadili mfumo wa utoaji wa haki nchini. Kwanza naomba niipongeze Mahakama kwa namna ya kipekee wanavyojitahidi katika masuala mazima ya utoaji wa haki na uendeshaji wa kesi Mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya pongezi hizi, bado zipo changamoto, bado yapo malalamiko mengi kwa wananchi juu ya mhimili wetu huu wa Mahakama katika masuala mazima ya utoaji wa haki na usimamizi wa kesi ama uendeshaji wa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, wananchi hawawezi wakalalamika tu juu ya Mahakama hii, maana yake ni kwamba kuna sababu za msingi ambazo zinawafanya wailalamikie Mahakama. Mimi kama Mbunge naomba nichukue fursa hii kuiomba Serikali sasa, ipo haja na sababu za makusudi za kuongeza watendaji katika Mahakama yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tutakapotumia nafasi hii ya kuongeza watendaji katika Mahakama, itakuwa ni sababu ya kupanua wigo, itakuwa ni sababu ya kurahisisha usikilizaji wa kesi na utoaji wa hukumu kwa kipindi kifupi baada ya kesi kusikilizwa. Kama tutafanya hivyo, tutawasaidia na kuwapunguzia kero wananchi hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kuna watu wanatoka masafa ya mbali kwenda katika Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya na katika Mahakama za Mikoa kusikiliza kesi ama hukumu za kesi zao, lakini wanapofika katika Mahakama zile wanaambiwa leo Jaji ama Hakimu ana kesi nydingi, kwa hiyo, warudi wanapangiwa tarehe nydingine. Hiyo tarehe ikifika, wanapangiwa tarehe nydingine. Mwananchi yule maisha yake ni duni, maisha yake ni magumu, anatoka masafa ya mbali, anakuja bila mafanikio. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nadhani ili kutatua changamoto hii, ipo haja Wizara ya Katiba na Sheria sasa kufikiria upya namna ya kuwaongezea maslahi Mahakimu hawa. Utakapowaongezea maslahi Mahakimu hawa tutapunguza kero na malalamiko kwa wananchi. Itakuwa ni sababu ya kuepuka vishawishi kwao na watafanya kazi kwa ufanisi, weledi na watatenda haki kiukweli kabisa na wananchi hawatalalamika. Katika hilo, naamini vishawishi vipo na zipo namna za kutatua vishawishi hivi na njia pekee, tuwaongezee maslahi watendaji wa Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la msingi, ni moja tu; kwenye Magereza zetu kumejaa mahabusu. Mahabusu ni wengi mno! Sasa kama Mahakama, kama Wizara au kama Serikali itafanya jambo la kusudi, kwenda katika Magereza yale kutafiti na kuhakiki ni mahabusu wangapi ambao wamo ndani ya Magereza yale, halafu wakafanya utaratibu; wale ambao wanaona kwamba ipo haja ya kuwatoa, wakawa wapo uraiani na upelelezi wa kesi zao unaendelea, basi nadhani ipo haja ya kufanya hivyo ili kupunguza mzigo kwa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale mahabusu wakiwemo mle Magereza Serikali inatoa fedha kwa ajili ya kuwalisha; na wale wanapotoka baadaye Serikali ama Mahahama inapowaambia ninyi mmetoka, hamna kesi. Wamekaa miaka mitatu, minne, nane. Wakija uraiani, maisha kwao yanakuwa ni magumu, wanakosa uaminifu na ushirikiano na jamii inayowazunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, wafanye jitihada za makusudi na za kipekee kabisa, kufanya uhakiki Magerezani. Ambao tunaona wanafaa tuwatoe nje, wakati wa wako nje upelelezi wao unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salum Shaafi. Tunaendelea na Mheshimiwa Michael Mwakamo na baadaye Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae. (*Makof*)

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo nami kuwa sehemu ya wachangiaji kwenye siku ya leo. Kwanza naanza kwa kuwapongeza sana Mawaziri wa Ofisi ambazo zinawasilisha taarifa zao kwenye Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa namna ambavyo leo wamewasilisha taarifa zao na wameweza kujibu changamoto mbalimbali ambazo Wajumbe tumeweza kushirikiana nao. Nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nichangie maeneo mawili tu. Eneo la kwanza, naishukuru Serikali juu ya fedha za miradi mbalimbali ambayo imepelekwa kwenye maeneo yetu. Hata hivyo, fedha hizi Wabunge wengi wamezungumza hapa, zinaweza zikaenda kwenye maeneo mbalimbali katika nchi hii lakini zikienda kwa uwiano ulio sawa zinaweza zikashindwa kufikisha malengo ya kumaliza matatizo ya wananchi kwenye maeneo tofauti ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo yana changamoto mbalimbali za ujenzi kutokana na umbali wa kupata bidhaa zinazoweza kutufanya shughuli za ujenzi kwenye maeneo hayo. Tunapopeleka fedha kote zikifanana kunakuwa na changamoto mbalimbali za kuweza kufanikisha miradi hii, na badala yake tunaacha manung'uniko na wananchi wengi wakiona kwamba miradi mingine inakuwa hajakamilika; au kuzipa Halmashauri majukumu mengine makubwa ya kuangalia ni namna gani wanaharibu bajeti nyininge za kutoka kwenye *own source* na kumalizia miradi iliyobaki.

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema Serikali ikaendelea na utaratibu wa kuangalia gharama halisi ya mahitaji ya kuweza kukamilisha miradi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nami nataka nichangie leo, ni hili eneo la asilimia 10 ambazo zinakwenda kutoka katika maeneo mbalimbali ya makundi ya vijana, wanawake na watu wenyewe ulemavu. Mfuko huu ni mzuri sana na unakwenda kumaliza matatizo mengi ya wananchi hasa pale kwenye kupata mitaji ya kuweza kufanya shughuli zao ili waweze kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo zipo changamoto mbalimbali tukiwa kwenye Kamati, TAMISEMI wamejaribu kuzieleza. Changamoto hizi zinakwamisha baadhi ya jithada na malengo ya mfuko huu. Kwa mfano, utakuta kuna baadhi ya maeneo kuna vikundi vimeundwa, vina watu wenyewe rika tofauti. Ni wamama lakini wana rika tofauti, lakini kwenye vikundi vyao humo kuna wababa nao wako kwenye sehemu hiyo. Ila kwa mujibu wa mwongozo uliopo, wanalahazimika wale wababa wakae pemberi, wapewe wamama, japo kwenye kikundi chao hicho miaka yote na siku zote wanazalisha bidhaa zao wakiwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ijaribu kutazama namna bora ya kuweza kusaidia; lengo la huu mfuko ni kuinua kipato cha wananchi kwenye maeneo yetu. Sasa tunapokuwa tunakwenda tukiangalia maeneo fulani fulani inaweza ikapunguza ile nguvu ya kufikisha huduma hii kwa wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye rika pia la vijana. Vijana wamepewa pale kuanzia miaka 18 mpaka 35. Hebu tuangalie kwa ukweli, sisi sote ni Wabunge, tunafahamu. Majimboni kwetu, ukiangalia rika linalozalisha au lililojikita kwenye kufanya biashara mbalimbali, linapita hili eneo na ndio wenyewe mahitaji makubwa sana ya mitaji. Kwa hiyo, naishauri Serikali irudi iangalie mfumo ule vizuri, iangalie ile sheria ili ikae vizuri. Kwa sababu hili kundi la vijana, wengi wanashindwa kuzichukua hizi fedha kwa sababu rika lao wengine ni dogo; miaka 18 mpaka 20 wengine bado wako katika mazingira ya shule, lakini wanayoihitaji mitaji hii ili waweze kukuza biashara zao na kutunza familia zao wako zaidi ya hili rika la miaka 35. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikajielekeza, kwa sababu dhamira ya kuuanzisha mfuko siyo tu ikakae kule ikawe kama ni maigizo fulani, lengo ni kutatua matatizo ambayo wananchi wanayo. Tunalo rika la kati linaloanzia miaka 35 mpaka 45 ambalo ndilo limejikita kwenye biashara ndogo ndogo, ndio limejikita kwenye kilimo, ndio lina shida kubwa sana ya kupata mitaji yao. Kwa hiyo, Serikali ni vyema ikaangalia upya, ije na namna ambavyo inaweza ikalisaidia hili kundi kubwa; na sio kazi ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hata Mheshimiwa Rais amezungumza kwenye zile fedha za UVIKO ambazo amepata, ameelekeza baadhi ya fedha kwenda kwa Wamachinga. Hebu tujiulize, wamefikiriwa wale kwa sababu lile kundi ni kubwa na lilikuwa halina sehemu linaweza likapata fedha kama isingekuwa kufikiriwa kupangiwa fedha hizi. Naamini kwa kutumia *own source* inawezekana kabisa asilimia 10 ingewasaidia hawa na wangkuza mapato yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna vikundi vya vijana ambavyo vipo vijiji, lakini wengi wanapewa fedha; wakishamaliza kupewa fedha, unaweza kukuta baada ya siku mbili tatu wamegawana, wamemaliza shughuli, hawana cha kufanya. Mimi nafikiri Serikali ingetoa mwongozo maalum, wapewe vikundi ambavyo wana jambo wanafanya ili wakaongeze tija kwenye jambo lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda kwenda bonde la watu wa Ruvu, watu wanalima; vijana wanalima kule. Ni vyema mkawaangalie wanaolima bila kujali rika lao, wawezeshwe ili walime kwa ubora, wavune wafanye biashara wapate kukidhi mahitaji ya maisha yao. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiriakwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisikia kengele, basi kwa machache haya, naunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael. Tunaendelea na Mheshimiwa Tunza Malapo na baadaye Mheshimiwa Joseph Tadayo ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uhai siku ya leo tukakutana kwenye Bunge hilli. Napenda kuunga mkono hoja ya Kamati kwa sababu nami ni Mjumbe wa Kamati hii ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni machache. La kwanza, hoja ya asilimia 10; ukiangalia karibia kila Mjumbi aliyesimama kuchangia ameiongelea. Ukiona watu wengi wanaongelea jambo moja, ujue aidha jambo hilo limefanyika vizuri ama jambo hilo limefanyika vibaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya asilimia 10, pamoja na lengo lake jema, hatuwezi kuisema vibaya moja kwa moja. Ina lengo jema na kuna baadhi ya watu wamefaidika na wanaendelea kufaidika; hilo tunalifahamu. Tatizo linakuja kwenye uendeshaji wake, kuna konakona nyingi sana. Kuna matatizo mengi sana hizi fedha, unapozungumzia mapato ya ndani maana yake ni kodi za wananchi. Serikali inakusanya kodi, inapata mapato, inatenga asilimia 10. Tunachotarajia ni kwamba zile fedha ziende zikatumike kweli kuwakwamua wananchi kiuchumi kama lengo au makusudi tuliyoyakusudia sisi Wabunge au Wawakilishi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo inakuja tofauti; tunapokuwa kwenye Kamati tukihoji, tupate vikundi vingapi vimekopeshwa? Wamekopeshwa fedha kiasi gani? Wamerudisha fedha kiasi gani? Je, huu mfuko kila siku tutakuwa tunatoa tu fedha asilimia 10 hazirudi zikaenda

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuzunguka? Zile za mwanzo ziko wapi? Hatupati majibu ya kueleweka. Unaambiwa mara kumbukumbu hazipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zinatolewa benki, yaani ili mwanakikundi apate fedha, lazima wasajili. Sasa fedha imepitia benki, inakuwaje leo mtu anakwambia hakuna kumbukumbu? Kwa sababu, kumbukumbu ingekuwa ni fedha tu ambayo mtu anatoa mfukoni, haina maandishi, haina nini, tungeelewa. Maana yake kuna tatizo. Kwa hiyo, naiomba Serikali, tunajua hili jambo ni zuri, lakini uzuri huu unakwenda kutiwa dosari na watendaji ambao sio waaminifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea kwa mwaka, kwa mfano huu mwaka wa fedha 2021/2022 karibia shilingi bilioni 70, ambapo zingeingia kwa wananchi ipasavyo, tulitegemea tuone mabadiliko kwa wale wananchi wetu katika Halmashauri. Kuna Halmashauri, mfano zile za Jiji la Dar es Salaam, kawaangalie kwa mwaka mapato yao ya ndani asilimia 10 ni fedha kiasi gani? Hata hivyo, ukienda kuangalia ufanisi, haupo. Kwa sababu gani? Ni kama kijewe, watu wamekaa kupiga fedha. Serikali inabidi iangalie suala hili kwa jicho la tatu. Fedha hizi ni nydingi, zingekwenda kubadilisha uchumi wa haya makundi ambayo tumeyakusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko yanaungua. Limeanza kuungua Soko la Kariakoo; tukakaa kidogo tukasikia Moshi soko limeungua; hatujatulia, Karume likaungua; hatujatulia Mbagala soko limeungua. Wakati soko la Kariakoo linaungua mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kipindi kile alikuwa Waziri wa TAMISEMI, alikwenda. Tukaambiwa imeundwa Tume, watatupa majibu. Naomba niwalize Wabunge wenzangu, hivi ninyi wenzangu mlisikia majibu ya uchunguzi uliofanyika Soko la Kariakoo? Mimi binafsi sijasikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kulisema hili ni nini? Unapofanyika uchunguzi, mimi nafikiri lengo; tujue kwa nini soko limeungua, ni sababu gani zimepelekea soko kuungua

na kuna utaratibu gani wa kuzuia masoko mengine yasiungue? Kwa sababu, hizo fedha za asilimia 10 zinazochukuliwa mikopo nyngine zinaingia kwenye masoko humo; bidhaa/mali za watu zinaungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanakwenda kuchukua fedha benki wanakwenda kufanya biashara, mtu hawesi kurudisha kwani mali zake zimeungua. Maana yake kule nyumbani sisi tunasema ni sawa na unasuka ukambaa jikoni; huku unasuka, huku unaungua. Mwisho wa siku ukiinuka pale ukindu wako umeisha, hauna chochote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema hapa, haya masoko ndiyo wananchi wetu wanafanya biashara zao huko. Tuangalie namna ya kuyaweka katika hali ya usalama. Yanapoungua, wanaoathirika ni wengi. Hizo fedha za Halmashauri kwani leo mtu kama ulimpa asilimia 10, kama mtu leo alikopa benki halafu bidhaa zake zimeungua, analipa kutoka wapi wakati ye ye alitegemea auze pale halafu akalipe? Wewe utamfanya nini? Kweli soko limeungua; kwani hata huyo wakimwongezea muda wa kulipa miaka mitano kama hana biashara, atalipa kutoka wapi? Kwa hiyo, suala hili la kuungua masoko liangaliwe kwa jicho la tatu; hii *trend* siyo sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitaki kuongea sana. Jambo langu lingine ni kuhusu Sekretarieti ya Ajira. Tungekuwa *serious* hii nchi sasa hivi ilibidi itangaze janga la wafanyakazi kwenye sekta ya afya na kwenye sekta ya elimu. Leo tunakaa hapa tunasema ufaulu kwenye hisabati asilimia 19, wakati kwenye sayansi huko nako hakueleweki, lakini Serikali inataka viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu anakwenda kuchanganya *chemical*/kama hajasoma *physics*, hajasoma *chemistry*na kadhalika? Sasa Sekretarieti ya Ajira Mheshimiwa Jenista iko chini yako; tunafanya kazi na wewe vizuri tu, janga la walimu mashulenii, janga la watumishi wa afya; umejenga vituo, hakuna watoa huduma, yatageuka magofu. Kila kitu inabidi kiende kwa *plan*. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo ni janga ama ni upungufu wa hao watumishi?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa asilimia 19 ufaulu, utasemaje upungufu? *To me, hilo ni janga tu, yaani hakuna namna ya kuisema.* (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hiyo siyo tafsiri ya janga. Haya malizia.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwambia dada yangu Mheshimiwa Jenista, wakae wajipange. Tunataka tuone walimu na watumishi wa afya ili iendane na ile nguvu na jitihada za fedha za walipa kodi ambazo zimekwenda kujenga yale majengo ya vituo vyaa afya na madarasa, yatufae katika kuendeleza vizazi vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Tadayo na baadaye Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naungana na wenzangu kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zetu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, wataalam na wadau wote ambao tumeshirikiana nao kwenye Kamati zote kufanya hii kazi, pia kipekee na kwa upendeleo, wale ambao wanaangukia kwenye Kamati yangu ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo liko wazi kwamba pamoja na majanga yote ya kidunia na nini lakini uchumi wa nchi yetu umeendelea kukua na Mheshimiwa Raisi Mama Samia Suluhu Hassan katika Awamu yake ya Sita

amekuja na kauli moja ya kusema kwamba tunaifungua nchi yetu kwa ajili ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii sio kauli ndogo, ni kauli kubwa sana; na mimi ninachofurahia juu ya Wizara na wadau wote wanaoingia kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ni kwamba wamejitali kufanya kazi kubwa sana katika kupata mambo mawili; jambo la kwanza kujenga mazingira katika kuifungamanisha nchi yetu na dunia kwa sababu ndiko teknolojia na mitaji iliko, lakini pili kujenga mazingira ya sisi wenyele Watanzania kwenda na hiyo hali mpya ya kujifungamanisha na dunia. Kwa sababu unajua unapofungua dirisha hewa iingie hata papasi na panzi huwa wanaingia kwa hiyo lazima pia ndani ujipange, ukishajifungamanisha na dunia yako mengi yanayoingia kwa hiyo lazima ujipange kwenda nayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa nazungumzia mfano wa taasisi zetu za usalama kazini; *OSHA* na *Workers Compensation* pamoja na hifadhi ya jamii (*pension*). Taasisi hizi zimefanya kazi nzuri na hata ukizipima kwenye vigezo vya *blue prints* wametekeleza kwa kiwango kikubwa sana na ndio maana kama taasisi ya *OSHA* imeweza kujifikisha kwenye viwango vya kimataifa kiasi cha kuweza kupata dawati katika mambo ya usalama kazini pale *SADC*, hii ni hatua kubwa ambayo kwa kweli tunapaswa kuiona kwamba taasisi imetuwalilisha vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *OSHA* ikifanya kazi yake vizuri, majanga yakapungua mahali pa kazi, mzigo unapungua *Workers Compensation* kwenye fidia, kwa sababu kunakuwa hakuna ajali ajali. Mzigo ukipungua kule wale wanapata nafasi ya kuwekeza na kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Hali kadhalika watu wa *pension* wakifanya kazi zao vizuri inaongeza ufanisi kwenye kazi na inapunguza hata matatizo ya rushwa kwa sababu wakati mwengine ufanisi na mambo ya kudaidai rushwa pia yanatokana na hofu ya kustaafu. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anajuliza *fine* nafanya kazi leo nna mshahara mzuri lakini nikishaafu kesho itakuwaje. Kwa hiyo kama kuna taasisi hizi za hifadhi za jamii ambazo zipo *stable* hiyo pia zinatusaidia hata katika mambo kama haya ya kupunguza rushwa na kuongeza ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja ambapo tumepata fursa ya kuziangalia taasisi hizi, kazi imefanyika vizuri na tunazipongeza na tunadhani kwa viwango vya *blue print* na viwango vingine wanapaswa kuigwa kwa ufanisi mzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta wa utoaji haki; Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu pamoja na *DPP* pia wamefanya kazi nzuri, zipo changamoto za upungufu wa watumishi pamoja na masuala ya kibajeti, hali hiyo sasa ni jukumu letu kushirikiana nao kwamba wakati wa bajeti ikija tuwapitishie bajeti nzuri kwa sababu wameshaonyesha uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sheria ambazo tumezipitia, tumeangalia jumla ya Miswada sita ambayo inarekebisha sheria 58 *almost*. Hizi zote zimekaa kimkakati wa kuisaidia nchi yeti katika kupiga hatua za kiuchumi, kwa sababu tuseme yote lakini uchumi ndio kila kitu, hali ya nchi itakuwa nzuri uchumi ukiwa vizuri. Kwa hiyo, zipo sheria kubwa ambazo zimezungumzwa hapa na wenzangu kama mabo yale ya *nolle prosequi* na mambo mengine ya kukamilisha upelelezi kabla ya kupeleka watu Mahakamani ni mambo mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ziko sheria nyengine ambazo sio rahisi kuzi-*note* lakini bado zina-*impact* sana katika masuala ya uchumi wa nchi. Kwa mfano marekebisho ya Sheria ya Makampuni ambayo tuliyapitisha. Ooh! Naona kengele imelia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Basi labda tu niseme kwamba sheria zote ambazo zimepitishwa kwa kweli nimekuwa nimejiandaa kuzitaja zote zimekaa kimkakati kusaidia nchi yetu kuweza kujifungamanisha na dunia na kurahusisha mambo ya biashara za kimataifa, lakini pia kulinda haya mafanikio yanayokuja na kuwalinda Watanzania katika mchakato huu unaokuja wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo na kwa ajili ya muda basi nuinge mkono hoja kwa asilimia zote ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tadayo tunaendelea na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na baadae Asha Abdalla Juma ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye taarifa za Kamati hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, tumepokea taarifa kutoka halmashauri zote nchini juu ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Raisi Mama Samia Suluhi Hassan, kwa kazi kubwa kwa kweli aliyoifanya na ubunifufuu mkubwa sana, lakini niwapongeza Mheshimiwa Waziri na watumishi wote kwa namna ambavyo wamesimamia fedha hizi. Tumepokea taarifa kutoka kwenye halmashauri kwa kweli wamefanya kazi nzuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo madarasa yamejengwa, vituo vya afya vimejengwa, miradi ya maji imekwenda, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya na niseme kwa *style* hii hii Mheshimiwa Rais atafute fungu lingine alitupie kule kilimo. Kule kilimo tukipata kama shilingi trillioni

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

moja naamini sasa tumemaliza kazi nchi hii itasonga kwa speed kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwenye eneo la asilimia 10; fedha hizi ambazo ni nyingi tumeambiwa hapa ni karibu ni bilioni 70 zimekopeshwa. Utaratibu wake bado hauridhishi, tumepokea taarifa kwenye kamati yetu, tunaona namna halmashauri inavyojikanganya wengine wanakiri kabisa hawana taarifa sahihi kwenye jambo hili. Sasa mimi nashauri mambo yafuatayo:-

(i) Taasisi yetu inayohusika na TEHAMA kwa maana ya *e-government* watengeneze mfumo wa *ku-capture* taarifa zote kutoka kwenye Halmashauri ili tuweze kujua fedha ambazo zimepatikana ni asilimia 10, fedha za marejesho ni kiasi kadhaa, vikundi viliviyokopeshwa ni kiasi kadhaa na majina yao ili kukwepesha ujanja ujanja, hii kazi *e-GA* wanaweza kuifanya waifanye ili tuweze kufanya maboresho. (*Makofi*)

(ii) Pia tutazame sheria, hii sheria imefanya vizuri, lakini kuna kundi linaachwa, tunasema vijana wanaokopeshwa ni kuanzia umri wa miaka 18 mpaka 35, lakini miaka 35 na kuendelea na tunaamini miaka 35 – 45 ndio kundi lenye sasa limetulia linataka kufanya kazi, kundi hili la wababa halimo. Niombe tutazame namna ya kufanya marekebisho ili na hao wanaume nao waweze kukopesheka wafaidi fedha hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana na mimi kwenye jimbo langu la Hai wamenituma, wakina baba wanasema tumeaacha kwenye eneo hili. Tafadhalini sana tulete hiyo sheria tuifanyie mabadiliko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hili ambalo limejitokeza, sasa hivi tunapokea taarifa ya masoko yetu kuungua na wenzangu wamechangia hapa. Niende kwenye suluhu, baada ya matukio haya nimejifunza kitu nikaenda kwenye historia; kwanza nikatazama majukumu ya Jeshi letu la Zimamoto, nikajuliza hivi tunahitaji makamishna, tunahitaji

mabrigedia, tunahitaji maafisa kwenye kuzima moto kweli. Nikagundua mwaka 1950 kazi ya kuzima moto na uokoaji ilikuwa inafanya na halmashauri, na ilifanya vizuri, baadae mwaka 1982 wajibu huu ukahamishwa TAMISEMI, wakaendelea kufanya vizuri. Sasa hivi naijuliza *administrative cost* za chombo hiki zingeweza kuhamishwa zikaenda kukunua magari ya *fire*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri sasa Serikali itazame upya namna ya kurudi kule kwa mwaka 1950, jukumu hili lishushwe halmashauri ambayo inakusanya, inaweza ku-manage na kuajiri watu ambao wanaweza kufanya kazi ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini watumishi au vibarua wanaweza kufundishwa ukiancha ile *top layer* wakafanya kazi hili kuliko kuwa na maafisa wengi wana *consume a lot*, halafu tunashindwa ku *operate*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana watuletee sheria tuone upya namna ya jukumu hili lirudishwe kwenye Halmashauri, mfano Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam zikipewa jukumu hili zinaweza kufanya vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niishie hapo na niunge hoja mkono, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwia Saashisha. Mheshimiwa Asha Abdulla Juma na baadae Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge ajandae.

**MHE. ASHA ABDULLA JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima leo nikaweza kusiamama mbele ya Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza sana Jemedari wetu Mama Samia Suluhu kwa jinsi anavyochapa kazi na kutuongoza vizuri na mambo yetu yanaenda vizuri. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nawapongeza Mawaziri ambao wanatuongoza kwenye Wizara zetu hasa hii yetu ambayo tunashughulika nayo moja kwa moja kuanzia kwa Waziri Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa kweli tumekuwa tunafanya kazi kwa mashirikiano na masikilizano makubwa, naweza kusema ni Kamati ambayo tunajiona kama tunafanya kazi *heaven on earth*, tunafanya kazi peponi katika dunia jinsi tunavyoweza kufanya kazi na ku-deliver.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kupongeza sana Wakala wa Usalama na Afya Sehemu za Kazi. Kwa kweli wakala huu umeweza kufanya kazi vizuri sana kwa mujibu wa sheria iliyoianzishwa ya mwaka 2003; kwanza jambo la muhimu sana lile la kupunguza tozo na kuwaondolea wadau kero, halafu urasimu wa kupata huduma kwa kutumia nyenzo hizi za kisasa kwa matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine waliloweza kufanya watu hawa ambalo ni la heshima sana ni lile la kusimamia kumaliza jengo la Wakala na Usalama Sehemu za kazi hapa Dodoma. Jengo la uhakika lenye viwango lenye kutimiza masharti yote, lenye kurahisisha watu wa aina yoyote kuweza kutumia, kwa hivyo wale wote waliloweza kusimamia katika kazi nzuri hii nawapa kongole zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto katika *OSHA* nayo ni uhaba wa watumishi, sijui kwa nini; kwa sababu tunaona huko nje tunaona wamezagaa ma-*graduate, mechanical engineering, ma-electrical engineering*, watu wa afya na nini, sielewi inakuaje mpaka watumishi ikawa tabu kuchukuliwa kwenye Wizara hiyo kwenda kufanya hiyo kazi. Kwa upande wa *OSHA* nawapongeza sana na waendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sehemu yangu ya pili ninayotaka kuzungumzia ni hii ya Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo; hii nayo imepiga hatua kweli kweli kwa sababu zamani ilikuwa shida kidogo, lakini wameweza kuongeza vituo kutoka 139 ambayo ilikuwa kwa kuititia kwa Mkuu wa Wilaya hadi vituo 8,817 katika vituo vya tiba, huko kote watoto

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanaandikishwa. Kwa hiyo hii imewapunguzia wananchi usumbufu na vilevile Watoto wanaweza walokuwa chini ya miaka mitano wanaandikishwa bila ya kutoa ada yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo changamoto ambazo *RITA* imewakabili ni zile za kushindwa kuandikisha watoto wanaozaliwa nje ya nchi, kwa sababu bado sheria hajatoa mamlaka kwa *RITA* kutekeleza hiyo. Sasa ninaushauri na ushauri wangu kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo Nchi za Nje, waje na mpango mkakati wa kutatua changamoto hii haraka iwezekanavyo ili hili jambo liweze kufanyaika na watu wapate vyeti vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile liko jambo moja ambaa linawasonenesha sana, ni hili watendaji wa *RITA* kuwa wanakaimu miaka kadhaa, yuko mwanadada pale tangu tumeingia sisi Bungeni hapa yeye anakaimu, kaimu, kaimu, sasa kama hafanyi kazi vizuri huyu kwa nini mnamuacha na sisi tunaamini anafanya kazi vizuri kwa sababu ripoti zinapokuja kwenye Kamati yetu tunaona anafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe mamlaka husika dada huyu apewe nafasi yake kwa sababu anaweza kufanya kazi vizuri. mwisho utamkuta anastaafu yupo pale pale, sasa hivyo ndio nini mnafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ninachotaka kuzungumzia sasa hivi ni kuhusu dawati la kuwasaidia kwenye sheria. Kuna watu wanapata taabu sana, sasa imetolewa huduma na Wizara hii ya kuwapa watu *training* wakawasaidie watu kuanzia Mahakama ya Mwanzo mpaka Mahakama ya mwisho. Wasiwasi wangu kama hawa watu waangaliwe vizuri isijekuwa tunatengeneza vishoka vyengine kwenye Mahakama. Wapate *training* nzuri ili waondolewe, kwa sababu wananchi wengi wa Tanzania hawana uwelewa mzuri wa mambo ya kisheria, kwa hivyo nifurahie kwa hili na ninaunga mkono na ninaomba Serikali izidishe iwaondolee wananchi shida zao.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ninaunga mkono hoja hii, ahsanteni. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ulenge* na baadae Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia, leo nitachangia Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu. Lakini pia kipekee kabisa niwapongeze Kamati hii ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kwa mapendekezo yao mazuri kabisa wallyoyatoa hasa kwa asilimia 10 ya fedha zile za Serikali za Mitaa. Kiukweli kabisa ni wakati sahihi sasa kuhakikisha tunakuwa na mfumo madhubuti ambaao uta-*enhance transparency*, ita-*enhance accountability* ili fedha hizi ziweze kuleta tija kwa makundi yale yaliyolengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi iliyotolewa na Wizara ya Fedha ya mwaka 2020 imesema kwamba ili Taifa letu libaki katika uchumi wa kati wa chini au ili tusonge mbele kitu kimojawapo ni kuhakikisha tunatengeneza uchumi shirkishi na kuondoa umasikini, na mimi ninaamini kabisa kabitia kupitia asilimia 10 tunakwenda kufanya uchumi shirkishi na kupunguza umasikini kwa wanawake wa Taifa hili na makundi maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotoka kwa ajili ya asilimia 10 kwa Tanzania yetu hii ni fedha nyingi, ni fedha ambazo zinapangwa kupangiwa utaratibu mzuri na maalum ili zilete tija na athari chanya kwa makundi yaliyolengwa. Ukiangalia takwimu mwaka 2019/2020 Serikali yetu imokusanya zaidi ya shilingi bilioni 717, inamaana asilimia 10 ni bilioni 71 *point*, lakini mwaka 2021 Serikali yetu imokusanya kwa Tanzania nzima shilingi bilioni 757, asilimia 10 ni zaidi shilingi

bilioni 76; lakini mwaka 2021/2022 Serikali yetu imepanga kukusanya shilingi bilioni 863 inamaana asilimia 10 ni itakuwa shilingi bilioni 86 za Kitanzania, ni fedha nyingi sana ambazo ni lazima tutengeneze utaratibu mzuri kuhakikisha unaleta tija kwa makundi yaliyopagwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kanuni zetu ambazo zimetolewa kwa ajili ya asilimia 10 zina madhaifu, pamoja na mwongozo ambao ultolewa Machi, 2020 nao unahitaji maboresho. Kwa mfano katika mwongozo pamoja na kanuni kifungu cha 21(d), imeitaka TAMISEMI iwaelekeze Wakurugenzi wa Halmashauri kufungua akaunti moja tu ya kuhifadhi zile fedha pamoja na marejesho. Sasa fedha za marejesho zile ni fedha nyingi tukichanganya kwenye akaunti moja maana yake tunakwenda kupunguza uwajibikaji na *accountability*. Nashauri kanuni ielekeze kuwepo na akaunti ya marejesho pamoja na akaunti ya mikopo ile ya makusanyo ili ya asilimia 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukiangalia kanuni ya 21 kifungu cha 37(a), kinasema kwamba Halmashauri zote zitoe mafunzo kwa wale wanaopata mikopo. Lakini mafunzo yake yanalenga ujasiriamali, yanalenga uongozi, hayazungumzi namna ambavyo wapewa mikopo watazijua hizi kanuni na taratibu ambazo zimewekwa. Kwa maafisa maendeleo ya jamii wengi na maafisa ustawi wa Jamii wengi wana *take advantage* kwa sababu hawaelekezwi yale makundi maalum namna ambavyo kanuni hizi zinaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kumekuwa na malalamiko mengi, wanawake wanasesma tunaomba mikopo kila mara lakini hatujulishwi kwamba nimepata au nimekosa ninaahangaika nakwenda na kurudi kila mara. Lakini kanuni inaelekeza ndani ya siku saba mpe taarifa mwanamke yule kwamba umepata mkopo au hujapata, inamaana siku saba zikipita mwanamke yule ata *assume* amepata mkopo. Kwa hiyo, tunaomba sana kanuni hizi zielekezwe kwa akinamama na makundi yaliyolengwa, ili wawewe kutumia fursa hii ipasavyo.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, oooh! Kumbe muda umeisha nakushukuru sana ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimtaja Mheshimiwa Kasalali Mageni na baadae atafuata Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya. Pia niwapongeze Wajumbe wa Kamati zote mbili kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuleta mapendekezo na ushauri wa namna ya kufanya katika mambo haya ambayo tunayajadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nipongeze Wizara zinazohusika na mjadala tunaoujadili hapa, hususan Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa usimamizi mzuri wanaoufanya huko kwenye halmashauri zetu, lakini pia Wizara ya Utawala Bora kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kusimamia Utumishi na kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo kama sitampongeza Mheshimiwa Rais kwa pesa nydingi alizotuletea kwenye halmashauri zetu hususan pesa zilizotokana na mkopo nafuu maarufu kama pesa za Mama Samia ambazo zimefanya kazi kubwa ya maendeleo huko Wilayani kwenye elimu, afya na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungezi hizi zinaendana na ushauri ambao nataka niutoe hasa kwenye Wizara ya TAMISEMI na Utawala Bora kwenye namna ya kufanya majukumu yaende vizuri huko kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyosemwa awali katika Ibara ya 145 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, majukumu ya usimamizi yameshushwa kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Katika Serikali zetu za Mitaa zipo hizi halmashauri za Wilaya, Majiji na Manispaa, wasimamizi wakuu wa halmashauri hizi ni Mabaraza ya Madiwani. Mabaraza la Madiwani ndiyo yametamkwa kama wasimamizi wakuu wa halmashauri zetu na Serikali za Mitaa, lakini kwa jinsi hali inavyokwenda tunaweza tukajikuta tunatengeneza mipango huku juu tukiiteremsha huko chini haifanikiwa vizuri kwa sababu hawa wanaosimamia hizi halmashauri zetu bado hatujawawezesha kiasi cha kutosha ili waweze kusimamia vizuri halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hapa kwenye Bunge la Bajeti tulizungumza kuhusu kuhamisha malipo ya Madiwani yatoke kwenye halmashauri kwa mapato ya ndani na yalipwe na Serikali Kuu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Viongozi wa Serikali kwa kulikubali suala hili. Limesaidia kwa kiwango kikubwa sana ingawaje bado malipo yale ni madogo, lakini limesaidia sana. Sasa hivi kuna tatizo moja kwenye halmashauri huko kuhusu posho za vikao vya Madiwani, Wakurugenzi wengi wanafanya kazi hizo kwa kutumia vichwa vyaao na siyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefikia wakati nikitoa mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ksimba, sasa hivi viko vya Baraza la Madiwani, Madiwani wanaenda tu ili liende kwa sababu Madiwani wote wanaotoka Jimbo la Sumve ambalo halina hata Makao Makuu ya Wilaya hawalipwi pesa ya kulala, wanalipwa pesa anaambiwa Diwani aende kwenye kikao cha halmashauri amalize kikao arudi nyumbani, ukimuuliza Mkurugenzi anasema kuna wakara. Hizi nyaraka za Serikali zinazozungumza kuhusu posho za Madiwani, nimejaribu kuzipitia nimekuta zipo nyaraka karibu tisa na inaonekana yingine sijazona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuwasaidie hawa Madiwani imefika wakati Bunge hili la Serikali tuamue kutoa utaratibu wa aina moja unaosimamia maslahi ya Madiwani

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ili halmashauri zetu ziweze kusimamiwa na watu ambao wana uhakika na wanachokifanya, vinginevyo sasa hivi Madiwani wanaenda kwenye vikao kutimiza wajibu tu wanawayhi warudi nyumbani. Sasa wasimamizi wa halmashauri wasipokuwa na uhakika na wanachokifanya mwisho wa siku ndiyo mwanya wa wizi na ubadhirifu tunaendelea kuuona unaendelea kwenye halmashauri zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kushauri, Serikali na Bunge tutoe maelekezo ya aina moja, yanayofanana nchi nzima ya namna ya kushughulikia maslahi ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Costantine Kanyasu na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Wenzangu waliotangulia kwenye Kamati wamezungumza kuhusu usimamizi wa asilimia 10, nami naomba tu kuongezea jambo dogo kwamba ukilisikiliza unaona ni jambo dogo lakin nataka nitoe mfano wa halmashauri yangu. Halmashauri yangu inakusanya takribani bilioni nane mpaka bilioni 11 kwa mwaka, maana yake inatenga kati ya milioni mia nane na bilioni 1.1 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudisha miaka mitatu nyuma ukawaambia naomba tuangalie akaunti hii ina shilingi ngapi hakuna hela na wanasubiri maombi mapya ya vikundi, wanasubiri makusanyo ya halmashauri ya *quarter* hiyo ndiyo wawagawie walioomba. Maana yake ni kwamba fedha hizi takribani bilioni tatu za miaka mitatu nyuma hazijarudi na kwa sababu zilifunguliwa akaunti ya kujitegemea maana yake ni kwamba hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni kubwa kuliko tunavyofikiri na tumeshauri kwenye Kamati, inawezekana

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

watumishi wanaopewa kazi ya kusimamia Mfuko huu, ujuzi na uwezo wa kusimamia mafungu makubwa haya ya fedha hawana. Sasa ni juu ya Wizara kuangalia utaratibu mzuri wa kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili nilizungumza mwaka jana wakati wa *briefing* kwamba Sheria ya Kodi Na. 332, sehemu ya kumi ambayo inawapa mamlaka *TRA* ya kukusanya fedha inagongana na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 290 na Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 288 na matokeo yake inasababisha wapangaji kwenye majengo ya halmashauri kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liko ofisini kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sheria hiyo ambayo imezipa mamlaka Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya kubuni na kuanzisha vyanzo vya mapato imeipa pla Mamlaka ya Kodi ya Mapato kutokutozwa kodi. Sheria inasema kwenye Kifungu cha 6(1) kwamba *all assets vested in the urban authority by virtue of this section...* zimetajwa pale, anasema ni *all moneys derived from any trade, industry, works, services and other undertaking properties owned by the Council*, zimeelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida inakuja sasa tafsiri ambayo wanakuja nao halmashauri wanasema kwamba pamoa na sheria kutoa mamlaka hayo, nashindwa kuisoma sheria kwa sababu ya muda, wanasema iwapo halmashauri imewekeza majengo makubwa na wameweka wapangaji wao wanakwenda kukusanya kodi kutoka kwa wale wapangaji kwenye kodi ya pango ambayo halmashauri inalipwa. Kwa hiyo, yule mpangaji anapolipa pango la halmashauri asipolipa *withholding tax* ya *TRA* wanafunga account.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yake imeeleza vizuri lakini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tuliomba ufanuzi kwenye jambo hili na ikaeleza vizuri ikasema kwamba kwa maoni yao wao wanafikiri kwamba sheria iko *clear* na *TRA* hawapaswi kutoza kodi.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwanasheria Mkuu atusaidie, Wizara ya Fedha itusaidie, halmashauri yangu wapangaji wanahama kwenye majengo kwa sababu wanalipa kodi mara mbili. Sisi hatutaki kujua kwa sababu sheria inatulinda kwa sababu tunataka tulipe hela tulioelewana nayo, anapotulipa anaambishi akate hela ya halmashauri na matokeo yake asipolipa anafungiwa akaunti. Hii ni Serikali moja ni lazima tukubaliane, jambo hili kwa nini lifanyike Geita peke yake na lisifanyike sehemu nytingine? Kama ni sheria iwe *uniform* itangazwe ijulikane.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kama utaniruhusu...

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni jambo la ajira, limezungumzwa vizuri kabisa na wenzangu. Tunaishukuru Serikali imeajiri Walimu 11,000, lakini Wizara ilikuja ikatufanya *presentation*, mahitaji ya walimu ni 120,000 wa *primary* na sekondari.

Kwa hiyo utaona ni asilimia kumi ya walimu walioajiriwa, sasa ukiwa na *deficity* 90 percent ukategemea kutengeneza *quality* inayofanana na ujue hii 90 percent *deficit* ipo zaidi vijijini ambapo wale waliopo vijijini hawana *access* na *tuition* na mengine lazima utegemee *product* ambayo haifanani kwenye mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili liangaliwe vizuri. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage na tutamalizia na Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuipongeza Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri; na Mheshimiwa Deo Ndejembie, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushughulikia masuala yote ya maslahi kwa ujumla ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja na miezi kadhaa tumeona kuna changamoto kubwa ya wafanyakazi na ajira, lakini tumeona takribani watumishi 180,000 wamepandishwa vyeo na kubadilishwa kada, lakini suala zima la madai pamoja na malimbikizo ya mishahara pia Serikali imeendelea kuhakiki pamoja na kulipa. *So far* mpaka sasa hivi watumishi takribani 37,000 wamelipwa madai yao na malimbikizo jumla ya shilingi trillioni 65 zimetumika, kwa hiyo tumeona nia thabiti ya Serikali kuendelea kushughulikia maslahi ya wafanyakazi, tunawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zima la uhuishaji wa miundo ya maendeleo ya utumishi wa wafanyakazi. Hili suala nimekuwa nikilisema sana kwenye michango yangu, lakini sasa hivi kumekuwa na uhuishwaji wa miundo ya watumishi takribani 22 kwenye Wizara na 47 kwenye Wakala wa Serikali na Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zima la kutoa vibali. *So far* wametoa vibali karibu mia tisa kwa ajili ya kutoa ajira kwa nafasi zilizokuwa wazi, pia wametoa vibali karibu mia tano kwa ajili ya nafasi za uongozi, pia wametoa vibali 550 kwa ajili ya ajira ambazo sio za mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wameshughulikia miundo mbalimbali, kwenye utumishi wa umma kuna miundo mingi, lakini sasa hivi kuna muundo mpya umetoka unasimamia utendaji wa kazi na upimaji wa Mtumishi.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Muundo huu utakuwa na tija sana kwa sababu mtumishi atapimwa, atajiandalia kazi zake na mwisho atapimwa kutokana na kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundo iko mingi lakini kuna suala zima pamoja na pongezi nilizozitoa kuna suala ambalo limekuwa kero ambalo wenzangu pia wamelisemea ni kukaimu kwa muda mrefu. Watumishi wanakaimu kwa muda mrefu, naishauri Serikali sasa inaweza kuandaa kanzidata ili kupata uelewa wa watumishi ambao wana mwelekeo wa uwezo wa kupata hizi nafasi. Kwa hiyo, kuwe na mkakati maalum wa kuandaa hili jambo, limekuwa ni kero kubwa kwa watumishi. Watumishi wamefanya kazi kwa bidii wana uwezo, sasa ifikie sehemu wapate kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la watumishi Serikali imejitahidi kuajiri sasa, lakini bado kuna changamoto. Naishauri Serikali kama inawezekana kuanzia halmashauri zenye uwezo basi itoe vibali waajiri angalau kwa muda kwenye shule zetu na zahanati zetu, lakini zinapotoka ajira rasmi wale watu walioajiriwa kwa vibali hivi vya muda wapewe kipaumbele ya kuajiriwa kwenye ajira zitakazotoka. Hii itasaidia kuleta huduma njema ambayo sasa hivi inakosekana, japo tumepata hospitali na madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa tunamalizia na Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Niseme kwanza naunga mkono hoja za Kamati zote mbili ambazo zimewasilishwa kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia kwa namna ambavyo ametupatia pesa nyingi kwenye Majimbo yetu na wananchi wamenufaika, wanashukuru

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sana. Pamoja na pongezi hizo naomba nami nitoe mchango wangu kwenye maeneo mawili kama siyo matatu kama muda utakuwa rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza kabisa nataka kuongelea kuhusiana na *TASAF*. Kwenye majimbo ambayo ni ya kijiji haifanyi vizuri sana kama ambavyo Serikali ina picha halisi. Wanufaika wengi wa *TASAF* kule Vijiji kiukweli siyo wale ambao walipaswa waingie kwenye Mfuko wa *TASAF*. Watu wengi ambao ni wazee na wengine ni walemauvu hawana hata uwezo wa kukopeshwa kwenye ile asilimia mbili yao ambayo inapatika asilimia kumi kwenye Halmashauri wameachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine niwaombe sana Viongozi wa Serikali, Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri wakubali tufanye ziara za kushtukiza twende kule ili wajonee uhalisia namna gani ambavyo wananchi wanalamika. Tumeona wakati mwingine wakitembelea kwenye maeneo yetu wanapata ule msururu wanazongwazongwa hawapati picha halisi. Wakati mwingine wanapewa taarifa ambazo siyo sahihi kulingana na uhalisia ambao upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* wananchi wengi ambao wanapaswa kunufaika ambao kweli hawapati mlo na wengine hawawezi kuijendeleza kabisa hawajapata na wengine ambao ni watendaji hawafiki kwenye yale maeneo ili kuchukua takwimu halisi, wanawaachia Wenyeviti wa Vijiji, wanawaachia Wenyeviti wa Mitaa na wengine pia ni binadamu wanaingia kwenye tamaa wanawaingiza ndugu zao ilihali hawakuwa wanufaika na *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kwenye *TASAF*, sehemu nydingine nydingi ambazo tumeona kwenye *TASAF*, ile miradi ya maendeleo ambayo imeubuliwa imeisaidia jamii kwa ujumla hata ambao hawakupaswa kunufaika na *TASAF*. Zipo baadhi ya halmashauri za vijiji watalaam wake hawana utalaam wa namna gani ya

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuandaa haya maandiko ili wayalete *TASAF* Makao Makuu waweze kunufaika na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusiana na *TARURA*. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu tena kwa namna ambavyo alimpatia kila Mbunge wa Jimbo bilioni 1.5 ili ziweze kwenda kumsaidia kwenye miundombinu. Kwa upande wangu kwenye Jimbo langu tumeanza kuona mwanga kutoka kwenye bilioni 1.5 hii. Ombi langu na ushauri kwa Serikali, wakati natoa ombi nisisahau kumpongeza *Chief* wa *TARURA* Injinia Seif kwa kweli amekuwa ni mtu mwema sana anawasaidia Wabunge wengi na nimesikia watu wengine wakimsemea. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *TARURA* tunaiomba Serikali kupitia Wizara yenye dhamana wawapunguzie *TARURA* mambo mengi wanapokuwa wamepata hela, kuwawekea vitu vingi mara sijui zabuni, vitu gani, inafika wakati wanaanza kutekeleza miradi hii wakati mvua zimekuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi kuna mafuriko, mkandarasi ameanza kulima barabara mwezi wa Pili, tarehe Mosi, leo tunavyoongea tarehe 14 Februari, barabara zote zimekwishasombwa na maji. Kwa hiyo, tunaomba pesa zinapotoka *immediately* watu wa *TARURA* waanze kufanya kazi mapema iwezekanavyo ili wafanye kipindi ambacho ni cha kiangazi, itatusaidia barabara zile zinapopitiwa na magari, zinapopitiwa na watu zinajishindilia lakini sasa hivi barabara zinaanza kutengenezwa mwezi wa Kumi na Mbili unapowauliza ni *corrugations* nyingi ambapo taratibu nyingi zinafanya hata zile pesa ambazo tumepewa na Mheshimiwa Rais zimepoteza thamani yake kwa sababu pale walipolima maji yamechukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tunashukuru Serikali kwa kutujengea madarasa mengi lakini pia na watoto wakapata madawati. Walimu walisahaulika kwenye eneo hili, Walimu hawajapata fenicha, wamepata ofisi lakini hawana mahali pa kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na upungufu wa Walimu kwenye madarasa ambayo tumeyapata, naiomba Serikali, kama Serikali Kuu imekubali kwamba itawalipa Madiwani posho zao, tunaomba zile halmashauri ambazo hazina uwezo kwa sababu sisi wengine tunatoka kwenye halmashauri ambazo hazina uwezo, kwa hiyo hawataweza kuwaajiri watoto wao kupitia mapato yao ya ndani, tuombe hii iwe *replaced* na Madiwani kama watapata posho kutoka Serikali Kuu, kile ambacho walikuwa wanapata Madiwani basi wale vijana wenzetu ambao wako mtaani wamekaa zaidi ya miaka minne hadi mitano na watoto wamekaa bila kusoma basi tunawaomba vija hao wakachukue hizo nafasi hata wakilipwa shilingi laki nne ninaamini zitawasaidia sana. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia upande wa Waheshimiwa Mawaziri nao pia nitawapa dakika tano tano. Nitaanza na Mheshimiwa Jenista Mhagama na baadaye Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, vilevile nishukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na imani na mimi na Msaidizi wangu Mheshimiwa Deo Ndejemb na hasa kutuamini kwamba tunaweza tukafanya kazi ndani ya ofisi yake. Tunamwahidi kutembea katika kiapo ambacho tulikula mbele yake utii, uaminifu, uzalendo na utendaji kazi uliotukuka, tutafanya kazi kwa bidii sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na Wabunge, Naibu Spika na kipekee nipongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati kwa kuchaguliwa na Kamati yetu kuongoza Kamati hiyo na

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Makamu Mwenyekiti, pia na Wenyeviti wengine wote wapya naamini tutakwenda sawasawa. Nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati kwa kweli nimekutana na Kamati inayoweza kufanya kazi kwa nguvu sana, naomba niwahakikishie ushirikiano mimi na timu nzima ya Ofisi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nianze kwanza kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wanaompongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan. Naomba nikiri kwamba tunaye Rais mwenye maono, Rais mzalendo, Rais ambaye anatamani kuiona nchi yake inapata maendeleo kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyasemi hayo kwa unafiki, naomba hayo kwa mifano halisi ya namna ambavyo Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa kweli. Ninayo mifano hasa inayotoka ndani ya Ofisi yangu, Ofisi ya Rais ambayo inashughulika na masuala ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa mwaka mmoja tu, Taifa letu limeweza kushika nafasi ya 87 kwa kufanya vizuri kwenye masuala la utawala bora ikizishinda nchi nyingi tu duniani kati ya nchi 180; na imeshika nafasi ya pili katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Tunafanya vizuri. Tunaposema masuala ya utawala bora ni masuala pia ya utendaji haki kwa kutumia vyombp na taasisi zilizoko ndani ya Ofisi ya Rais. TAKUKURU iko ndani ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, mmetuambia tuongeze *resources*; tuongeze watumishi. Tumeshaajiri watumishi wapya, tunaongeza wengine. Vilevile tumekubaliana na TAKUKURU tutaongeza fedha ya mafunzo. Tunataka tuwe na wapelelezi, waendesha mashitaka wabobezi ili kweli tatizo la rushwa liweze kuzuiwa vizuri na liweze kukomeshwa ndani ya nchi yetu ya Tanzania, ukizingatia tunayo miradi mingi, mikubwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya kimkakati. Mama anatafuta fedha nyingi sana, zinatakiwa kulindwa na wale wote wanaozikodolea macho washindwe kuzipata na Taifa liweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika ujenzi wa madarasa, ujenzi wa zahanati na ujenzi wa vituo vya afya. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais ameshatuagiza, hatutakubali, naye hayuko tayari miundombinu hiyo ianze kufanya kazi bila kuwa na rasilimali watu, yaani watendaji na watumishi katika miundombinu hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakubaliana na tunatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kabla ya mwaka huu wa fedha ni lazima tuwe tumeajiri watumishi, walimu, madaktari, manesi na wahudumu wote katika vituo hivyo vyote ambavyo tumevijenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Waheshimiwa Wabunge kaeni tayari, hayo maeneo ye nu na Majimbo yote ni lazima tutekeleze agizo la Mheshimiwa Rais. Tutaleta hao watumishi waanze kufanya kazi katika hivyo vituo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii imejidhihirisha katika kipindi kifupi sana cha mwaka mmoja; Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa kweli kwenye sekta hii ya rasilimali watu. Rasilimali watu ndio inayotunza rasilimali nyingine zote nchini. Kama siyo rasilimali watu, hata rasilimali nyingine haziwezi kufanya kazi. Katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja, ameeleza Mheshimiwa Mbunge Dkt. Alice, ameweza kupandisha madaraja watumishi 190,781, haijapata kutokea. Tumetumia fedha za Kitanzania zaidi ya shilingi bilioni 39 kwa kazi hiyo. Naomba niwahakikishie Watumishi wa Umma, kazi inaendelea, tutaendelea kuwapandisha madaraja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ameweza kufanikiwa kubadilisha kada za watumishi 19,386. Tumetumia zaidi ya

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

shilingi bilioni 1,330. Waheshimiwa Wabunge kazi inaendelea, ni lazima tujenge hiyo rasilimali watu tuliyonayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na kero kubwa ya malimbikizo ya mishahara kwa walimu, manesi na wafanyakazi wengine kwenye kada mbalimbali. Mheshimiwa Rais huyu lazima apongezwe. Kwa muda mfupi sana; na tumekaa muda mrefu kazi hiyo hajafanyika; ameweza kulipa malimbikizo kwa watumishi 65,394 na tumetumia fedha za Kitanzania karibu shilingi bilioni 91,087, kazi inaendelea, hatutaishia hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kazi inaendelea kwa sababu gani? Waheshimiwa Wabunge mwezi huu Februari tayari Mheshimiwa Rais amesema ni lazima tulipe shilingi billioni 32,690 kama malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wengine 19,226. Kazi inaendelea, Waheshimiwa Wabunge, haturudi nyuma na tuko imara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza eneo hilo la ajira mpya. Kama nilivyo sema tumeshapokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tunajipanga. Kabla ya mwaka wa fedha huu haujaisha, ni lazima tutoe ajira mpya nyiningine. Tumetoa ajira mpya kwa awamu iliyopita takribani kama watumishi 12,236, lakini tutaa jiri watumishi wa kutosha kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha na tutakuja kutoa taarifa hapa Bungeni baada ya kuwa maelekezo yote ya Mheshimiwa Rais tumeshayatekeleza na tumeyaweka sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana katika kujenga rasilimali watu nchini. Sasa tumekubaliana, pamoja na ujenzi wa rasilimali watu nchini ni lazima pia na watumishi wa Serikali sasa waanze kuwajibika ipasavyo ili kuleta tija katika maendeleo ya Taifa. Ndiyo maana tumeamua kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kufanya maboresho ya mfumo wa upimaji wa utendaji wa kazi kwa watumishi. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa *OPRAS* ambao uliasisiwa mwaka 2004 tunaufanya maboresho na kuitengeneza upya. Tunakuja na mifumo miwili; mfumo mmoja utapima utendaji kazi kwa mtumishi mmoja mmoja na mfumo mwingine utapima utendaji wa taasisi zetu zote nchini, tuone taasisi hizi tulizokasimu kusimamia matamko ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Dira ya Maendeleo na Mipango yao ya Kitaasisi katika kuendeleza Taifa letu. Tunataka kuona taasisi hizo zinatekeleza na hazizembe katika kufanya kazi hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawapima kila mwaka taasisi moja mpaka nyingine na tutazitangaza nchi nzima ya Tanzania zilizofanya vizuri na ambazo hazifanyi vizuri katika kufanya kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatengeneza mfumo mwingine ambao utatusaidia kufanya tathmini ya hali ya rasilimali watu tuliyonayo nchini. Lazima tufanye *manpower audit* tujue tumejipangaje? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa nikipokea malalamiko kwamba maeneo ya vijiji hakuna watumishi, maeneo mengine watumishi wamejaa, wako wengi. Tunataka kupata hii picha, hali ikoje? Tumepanga vipi rasilimali watu katika nchi yetu ya Tanzania ili kila mtu alipo aweze kufanya kazi na tuwe na tija. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Taasisi yetu ya *Watumishi Housing*. Tumeamua taasisi hiyo sasa ianze kujenga nyumba mpaka kwenye Wilaya mpya na Halmashauri mpya kupunguza tatizo la nyumba... (*Makof!*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa e-GA kushughulikia mikopo ya asilimia 10 na tumeshaanza kutengeneza mfumo utakaotusaidia kusimamia hayo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi na kazi inaendelea na Mheshimiwa Rais anatusimamia. Tunaahidi kutekeleza yote kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tunaendelea na Mheshimiwa Suleiman Jafo, baadaye Mheshimiwa George Simbachawene ajindae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikupongeze wewe kwa kuendesha Bunge hili. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na uzima.

Leo hii tumeposta wasilisho la kamati mbili; nampongeza sana *Comred* Mheshimiwa Chaurembo, ndugu yangu wa Mbagalwa, wa Mbande, wa Chamazi na kule maeneo ya Maji Matitu. Vile vile nampongeza sana *Comred Dkt. Joseph Mhagama*; Daktari huyu mpya mpya sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kama nilivyo sema awali na pia kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwenendo na utaratibu wa utendaji kazi ambao kila Mbunge anashuhudia. Katika Kamati yetu ya Katiba na Sheria kama mnavyofahamu ni kwamba inashughulika vilevile na suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja za Kamati kwa kweli nami napenda kuchangia humo. Kwanza naipongeza Kamati kwa kazi kubwa sana ambayo imeendelea kuifanya. Kamati hii imechambua mambo mengi, lakini niseme

kwamba, Kamati hii imefanya kazi kubwa sana katika suala zima la kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Amri Abeid Karume walivyoasisi Muungano wetu, umeweza kupita katika vipindi mbalimbali na viongozi wetu wote wamefanya mambo makubwa. Viongozi waliopita tokea Awamu ya Kwanza mpaka sasa Awamu ya Nane na Awamu ya Sita, kazi kubwa sana imeendelea kufanyika. Tunapozungumzia katika kipindi cha sasa hivi, naishukuru sana Kamati, hasa kwa maelekezo yake muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia tulikuwa na kero takribani 20 hadi 35 za Muungano. Katika kero hizo tuliweza kufanikisha kutoa kero saba mpaka mwaka 2010. Tulibakiza kero 18. Nawashukuru sana viongozi wetu wa Taifa, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kazi kubwa waliyoifanya katika kutuekeza, ambapo ndani ya muda mfupi tumeweza kufanikisha kuondoa kero 11 za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya Kamati hilo mmelizungumzia. Naishukuru sana Kamati yako, imeweka *legacy* na kwamba chini ya usimamizi wa Kamati yenu tumeweza kuondoa kero 11 za Muungano. Tunashukuru sana katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuhakikisha kwamba mustakabali wa Taifa letu la Muungano tunaenda kulisfanya kazi hasa, kama Kamati ilivyozungumza ajenda mbalimbali na hasa kushughulikia yale mambo mengine ambayo ni kero ndogo ndogo za kimuungano, lazima tuweze kuziondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafahamu Wabunge wengi sasa hivi kuna vitu *petty*; mfano, anakuja pale bandarini, ana pasi yake, ana TV yake, anakamatwa, inazuiliwa. Hizi ndizo kero ndogo ndogo ambazo kati ya kero saba ndani yake ndiyo ziko hizo nyingine ndogo ndogo. Imani

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

yetu ni kwamba, kama maelekezo ya Kamati ilivyotoa, tutaenda kuzishughulikia hizi. Kama tumefanya 11, sasa tunaenda kuhangalika na hizi kero saba zilizobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu kubwa ni kwamba, *trend* tunayoondokanayo, tunaenda vizuri. Mpangokazi wetu ni kwamba, kama Kamati ilivyoelekeza, ndani ya mwaka huu 2022 tuna imani tutaenda kufanya mambo makubwa sana. Yale mambo ambayo yamekuwa ni kadhia siku zote, inawezekana mengi yao yataweza kuondoka. Kubwa zaidi, katika mchango wa Kamati hii ni nini wanajadili kwa kina na hasa kero za Wabunge wanaotoka Zanzibar, hasa katika Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu, leo hii nilikuwa na Mheshimiwa Sheikh Cassim na Mheshimiwa Zahor, wameniambia mambo mengi sana. Mambo haya mengine tunaenda kuyafanya kazi kwanza. Kwa mfano, fedha za Mfuko wa Jimbo, mwaka jana 2021 tulifanya kazi kuhakikisha kwamba zile zilizotoka Desemba, baadaye sasa tukahangaika mwezi wa sita zikatoka. Mwaka huu tulihakikisha kwamba fedha za Mfuko wa Jimbo zote zinatoka katika muda unaofanana. Bahati nzuri kwa mara ya kwanza fedha zote zimetoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimepata taarifa kwamba, bado upelekaji wa fedha hizi kule kwa Wabunge katika Halmashauri kuna changamoto kidogo. Hili nikuhakikishie tutaenda kulifanya kazi. Sisi tunachotaka ni kwamba, kila Mbunge ajisikie ana raha katika Bunge lake hili, afanye kazio vizuri. Maana yetu ni nini? Tunapoudumisha muungano wetu, tuhakikisha kwamba, yale mambo ambayo ni madogo madogo yamekuwa kadhia, tuweze kuyaondoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba, Kamati ilivyotoa maelekezo, sisi jukumu letu Wizara ya Muungano ni kuhakikisha kwamba yale mambo yote iliyotolea maelekezo tunaenda kuyafanya kazi. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu, naomba niwashukuru Wabunge wote, lakini na Wabunge kutoka upande wa Zanzibar kwa mara nyingine. Kwa kweli wamekuwa na mchango mkubwa sana kwa yale mambo mbalimbali kuweza kuyatatua. Ndiyo maana siku ile kaka yangu Mheshimiwa Ahmed Idrissa Abdul Wakil tulifanya kazi kubwa sana, na amenikaribisha kuzindua lile jengo. Nitakuja kaka yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wabunge wote kwa kweli. Niwaambie Wabunge kutoka Zanzibar, kwa sababu mimi kazi yangu ni huku Bara na Visiwani; nimepata taarifa kwamba, wakati mwininge hata tukitoa taarifa Wabunge wa Majimbo hawapati taarifa. Tutahakikisha kwamba ziara zetu zile tunazofanya kila ziara Mbunge anapata taarifa. Lengo kubwa ni ionekane kazi ya Mbunge, anafanya ni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa haya machache, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili zilizowasilishwa hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Jafo. Tunaendelea na Mheshimiwa George Simbachawene na badaye Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ajiandae.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Vile vile kipekee sana namshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na sasa amenipa kuisimamia Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nampongeza tena Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizipongeze sana Kamati zote mbili; Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Utawala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, dakika moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(5), ninaongeza muda bila kulihoji Bunge mpaka shughuli yetu itakapomalizika.

Endelea Mheshimiwa. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati zote mbili; Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Utawala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri wanazofanya. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Chaurembo, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ambao kimsingi kwa upande wetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati ya Katiba na Sheria ikiongozwa na Mheshimiwa Mhagama, na wewe mwenyewe Makamu Mwenyekiti, mmekuwa watu wa karibu sana nasi, mnafanya kazi yetu iwe nyepesi, nanyi ni walezi wazuri. Kwa hakika mara zote hata wakati mwingine msipotuita tunajikuta tunawa-*misskwa* sababu, tukifika kwenye Kamati yenu mnatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba jukumu letu la Serikali linakwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi na Kamati. Kwa hakika kama ingekuwa hakuna ulazima wa kusema, wala hakukuwa na sababu ya kusema. Ilikuwa ni kusema amina, amina, amina, kwa sababu, tunatakiwa tu tuyachukue, tuyapokee na kwenda kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimeona niguse tu maeneo machache, hasa moja tu la hatua kubwa ambayo imefikiwa na Mhimili wa Mahakama. Katika jukumu ambalo pia ninalo kama Waziri wa Katiba na Sheria ni pamoja na kusimamia mhimili huu. Unaposimamia mhimili ni kitu kikubwa sana, na hasa mhimili huu wa Mahakama.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilifahamishe Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwamba, mhimili huu umepiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya kmtandao. Wamepiga hatua kubwa sana kiasi kwamba, sasa unaweza ukasajili kesi yako ukiwa nyumbani na simu yako na ukasajili shauri lako, lakini unaweza ukapata majibu yote ukiwa nyumbani wala usitoe hata hatua moja nje ya nyumba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna uwazi mkubwa katika uendeshaji wa mashauri ambapo unaweza ukasikiliza shauri lako na wala usifike hata Mahakamani. Maendeleo haya ni makubwa na wakati mwingine tunasema tumeenda mbele kuliko hata uelewa wa wananchi wa kupokea huduma yenye hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameenda zaidi sana kwamba, yako malalamiko ya wananchi kuhusu kutokutendewa haki au rushwa na mambo mengine na mhimili huu wa Mahakama. Yenye hio wameweka ukurasa mahususi ambao unaweza ukaingia na ukaandika uko wapi? Umetendewa nini? Uki-posttu pale, mfumo mzima wa Mahakama, viongozi wote wanaona, kwamba kuna mahali, mfano Tandahimba au wapi, kuna hakimu au kuna mtu mwenye wajibu wa kutoa haki amefanya hiki na hiki. Ni hatua kubwa mno Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunafikiri ikitupendeza na nilikuwa naongea na Mkuu wa mhimili huu, Jaji Mkuu - Prof. Ibrahim Juma, pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Ole-Gabriel, wakasema ikipendeza na kama kutakuwa na nafasi tupate fursa ya kuja kutoa semina kwa Wabunge ili muone mifumo hii na *system* hizi zinavyofanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hio, tutakapopata muda na kama muda utaruhusu, basi Bunge lijalo tupate *slot* hata angalau siku moja tuje tufanye semina hio ili Wabunge mwelewe iwe rahisi kwenda kuwaeleza wananchi hatua kubwa ambayo imefanywa na mhimili huu wa Mahakama.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Yamesemwa pia maeneo mengine ya namna ambavyo taasisi kama ya *RITA*, *NIDA*, Uhamiaji, *PSSF*, Bima ya Afya, Bodii ya Mikopo na mifumo mingine kwamba, iunganishwe ili iweze kusemana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba, maandalizi ni makubwa. Hatua kubwa imefikiwa na sasa mifumo hii inasema kwa pamoja na mawasiliano yapo na mahusiano yapo, yanaendelea kujengwa kwa mifumo zaidi ili kuhakikisha kwamba, mawasiliano ya vifo, usajili, utambuzi na vyote hivi vinapatikana katika mfumo wa pamoja katika Serikali.

Niwahakikishie tu kwamba, hatua hii imefikiwa na Wajumbe wa Kamati mmelisema hili sana na nirudie kusema, tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, yote mliyoyasema hakuna hata moja ambalo tutafuta. Tunayachukua kama yalivyo na tunahakikisha kwamba tunayatekeleza. Tutakapokutana mwezi wa Tatu tutawapa mrejesho wa hatua tutakayokwenda na ninyi mtatshauri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene kwa *commitment* nzuri hiyo. Namkaribisha sasa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana na baadaye Prof. Joyce Ndalichako, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa nami ni mara yangu ya kwanza kuongea kwa kuchangia katika Bunge hili kwa leo, naomba nianze kwa kumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa imani kubwa aliyonipa mimi na Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Nderiananga. Tunamuahidi hatutamwangusha. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, kwa mara nyingine tena niendelee kumpongeza sana Spika wetu, Mheshimiwa Tulia Ackson, kwa kupita kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono hoja zote mbili ambazo zimevasilishwa kutoka Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya USEMI. Naunga mkono mambo yote yaliyoandikwa na yaliyochangiwa kwa mdomo. Masuala yote ni ya msingi na niwahakikishie kwamba tutayachukua na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi wangu huu, ninaomba nizungumze *point* mbili kwa haraka sana. Kamati ya Katiba na Sheria imezungumzia juu ya suala zima la Sheria ya Maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze pointi mbili kwa haraka sana, Kamati ya Katiba na Sheria imezungumzia juu ya suala zima sheria ya maafa. Tunayo sheria ya maafa sheria hii ya maafa tulikuwa nayo mwaka 1990 ilikuwa ni Sheria Na. 9 na tukafanya maboresho makubwa sana mwaka 2015 Sheria Na. 7 ya maafa na kamati imesema tuendelee kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bunge lako hili la sasa *session* hii tutaisoma sheria hii kwa mara ya kwanza inakuja na maboresho makubwa sana sheria ya maafa. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na kamati juu ya maboresho katika sheria ya maafa na maboresho ambayo kamati wamesema kwanza wamesema ni muhimu kuwa na mfuko maalum wa maafa. Mfuko huu utaweka utaratibu wa namna gani ya kuchangia fedha za maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wabunge wamezungumza umuhimu wa kuwa na Waheshimiwa Wabunge ndani ya kamati za maafa. Muundo wa kamati tutakuwa na kamati za maafa ngazi ya Taifa, ngazi ya mikoa, wilaya kata hadi ngazi za vijiji kuona ni namna gani tunaratibu suala zima la maafa. Maana maafa yanatugusa sisi wenyewe ni jambo ambalo linatokea katika jamii zetu. Kwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

hiyo, tutakuwa na hizi kamati, kwa hiyo Wabunge watakuwa ni sehemu ya hizi kamati za maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu sana kamati wamezungumzia kuhusu elimu juu ya maafa. Nikuhakikishie kwamba sasa hivi katika mitaala ya shule zetu za Msingi, za Sekondari wanatoa elimu juu ya maafa kuna masomo mbalimbali pale katika shule zetu ni namna gani kujilinda na maafa kwa mfano janga la njaa tunafanyaje udhibiti wa mafuriko tunafanyaje kutokata miti namna gani ya kudhibiti namna gani ya kukabiliana na suala zima la maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la elimu ni jambo la msingi sana, hadi Vyuo Vikuu kuna taaluma za *degree* zinazohusiana na masuala ya maafa masuala ya *disaster management*, kwa hiyo, sasa hivi tumepiga hatua suala hili la maafa linapewa kipaumbele cha hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kamati pia imezungumza ni suala zima la utekelezaji wa mapendekezo ya kamati. Kamati mara nyngi inatoa maelekezo mbalimbali mapendekezo kwa hiyo, zinatoa kwa niaba ya Bunge na sasa kamati imeshauri kwamba Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu upo katika ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo nanukuu "*kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba Bunge ndicho chombo cha kuishauri*". Sasa kwa kuwa kamati hii ya Katiba na Sheria inasimamia pia masuala ya sera, uratibu na Bunge imeshauri kwamba tuone ni namna gani mapendekezo haya yanazingatiwa. Sualo hili pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu mpewda Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli amekuwa akituelekeza kwamba ushauri unaotolewa na Bunge Serikali

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

lazima tuuzingatie. Utakumbuka bajeti iliyopita kuna ushauri wa aina nyingi sana ultolewa na Bunge na ushauri ule wote kwa kweli ulikuwa umezingatiwa na Serikali. Kwa hiyo, suala la Bunge kuishauri Serikali katika taasisi na Wizara ni jambo la kikatiba ni jambo la msingi lakini pia siyo tu kutekeleza ule ushauri, baada ya utekelezaji wa ule ushauri pia Serikali tunakuja kutoa majibu ni namna gani imetekelezwa, na ndiyo maana katika kuitisha bajeti kila tunapoenda kwenye kamati tunasema utekelezaji wa maagizo ya kamati unawekwa pale na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jukumu la kikatiba na kwa kweli tunashukuru na tunaunga mkono suala hili na ni suala ambalo lipo tumekuwa tukifanya hivyo mara kwa mara lakini kamati imefanya vizuri sana kukumbusha kwamba tunaomba tuendelee suala hili kulizingatia na kama nilivyosema kwa kweli ni maelekezo ya Rais wetu mpandwa kwamba suala hili ni lazima tupate kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya maoni yote ambayo yametolewa na kamati zote mbili tunakwenda kuzingatia na vile vile tunakwenda kufanyia kazi na kama tulivyosema kwenye ibara hii ya 63 na majibu yanakwenda kuwasilishwa kwenye muhimili huu wa Bunge naomba kuunga mkono hoja nasema ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na baadaye Mheshimiwa David Silinde ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja za kamati mbili ambazo ziko mezani.

Kwanza nianze kwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, inayoshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba nitafanya kazi yangu kwa bidii yote na kwa uadilifu wa hali ya juu ili kuhakikisha kwamba malengo ya Wizara hii yanatekelezwa kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kupongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuongoza muhimili huu muhimu lakini pia niwapongeze wenyeviti wa kamati hizi mbili kwa sababu nao wamechaguliwa hivi karibuni nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba niishukuru kamati zote mbili kwa taarifa zao nzuri ambazo kwa hakika zimesheheni maoni na mapendekezo mazuri ambayo yanaonyesha jinsi gani wajumbe wa kamati hizi wana uweledi wa hali ya juu na wamechambua kwa kina masuala ambayo yanahusiana na kamati na mimi nazungumzia hususan yanayohusiana na eneo la Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na kama alivyosema jirani hapa kimsingi yote ambayo wameyashauri ni mambo ambayo yanakwenda kujenga kuongeza tija katika utendaji wetu wa kazi kwa hiyo niseme kwamba tumeyapokea na tuwahakikishie kwamba yote tutayafanya kazi kwa ukamilifu na tutatoa taarifa ya namna ambavyo tumefanya kazi maoni na mapendekezo ya kamati nawashukuru sana wajumbe kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nzungumzie baadhi ya maeneo kwa uchache katika taarifa ya kamati ya Katiba na Sheria wamezungumzia suala la kiwanda cha viatu kule Kilimanjaro na kiwanda hiki ni muhimu kwa sababu kinachochaea upatikanaji wa soko la ngozi kwa wafugaji wetu ina maana kwamba kadri kitakavyofanya vizuri basi tutaongeza na kipato kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaona umuhimu wa kiwanda hicho na tunashukuru kwamba wametushauri tuendelee kuongeza masoko jambo hilo

tunalifanyia kuhakikisha kwamba tuna masoko endelevu na kwa kuanzia kiwanda tayari kimetangaza nafasi za mawakala watanzania ambao wako tayari kuwa mawakala wa kuza bidhaa zinazotengenezwa na kiwanda hicho viatu pamoja na bidhaa nyingine za Ngozi. Kwa hiyo. niwahamasishe kwamba wachangamkie hiyo fursa kwa sasa hivi tunafanya uchambuzi wa maombi yaliyopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tumeshauriwa tuhakikishe kwamba tunajitangaza kupitia maonyesho hilo Ofisi ya Waziri Mkuu itasimamia kuhakikisha kiwanda kinatumia fursa zote za maonyesho zinazokuwepo lakini hata kuja hapa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni jeshi kubwa wanawakilisha watanzania. Kwa hiyo, akifahamu vizuri bidhaa hizi watakuwa mabalozi wazuri wa kusaidia kututangazia, kwa hiyo, hilo tutallizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo ambalo limezungumziwa pia sana ni kuhusiana na hii 4% inayokwenda kwa vijana fedha za halmashauri pamoja na mfuko wa maendeleo ya vijana kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshauri kwamba Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na TAMISEMI tufanye ufuatilaji wa hizi fedha zinazoenda kwa vijana. Hilo nalipokea na niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba hili lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais alipoongea na vijana kwenye uwanja wa Nyamagana siku ya tarehe 15 Juni, 2021 kule Jijini Mwanza alizungumzia suala hili fedha zinazotolewa kwa vijana kwamba Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa vijana lakini wakati mwingine vijana wanakuwa hawana taarifa sahihi za hizi fedha kwa hiyo wanakuwa hawanufaiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alihoji kwamba wale wanaonufaika wanafanyaje kufanya marejesho ili vijana wenzao waweze kunufaika. Ni dhahiri kwamba kauli ya Mheshimiwa Rais inatutaka sisi ambao tunahusika moja kwa moja na kusimamia vijana pamoja na TAMISEMI ambao

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inahusika na kutoa hizi fedha tufanye ufuatiliaji na kutoa miongozo na hata kutoa elimu kwa wale wanaopata hizi fedha tutoe elimu ya ujasiriamali na mafunzo ili kuhakikisha kwamba zinakuwa na tija na zinazunguka ili ziweze kwenda kuwakopesha vijana wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia ni changamoto ambazo baadhi ya vijana wanapata kuhusiana na fursa ambazo zinatolewa za kukuza ujuzi. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametupatia bilioni 9 kwa ajili ya kukuza ujuzi na kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge baadhi ya vijana wanapata changamoto kwa sababu wako mbali niwaambie kwamba Serikali ni siku jambo hilo tumeshaanza kulichukulia hatua wale wanaofanya mafunzo ya kilimo kitalu nyumba tunawalipa shillingi elfu 10 kwa siku kuwawezesha kwenda kuhudhuria na wale ambao wanapata mafunzo ya uzoefu kazini tunawalipa 150,000 kwa mwezi na tutaendelea kufanya kazi changamoto hii na kuangalia namna bora zaidi ya kuhakikisha tunafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimalizie kwa kuunga mkono hoja kwa kamati zote mbili nashukuru sana kwa ushauri tutaufanya kazi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako tunamalizia na Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipatia fursa hii kuchangia taarifa za kamati mbili zilizoletwa hususan kamati ya USEMI ambayo ndiyo wasimamizi wakuu wanaotusimamia sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya USEMI na nikiri wazi kabisa moja ya kamati ambayo imekuwa ikitushauri vyema kabisa sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni Kamati

ya USEMI imekuwa karibu nasi nyakati zote na sisi bila kinyongo chochote haya yote waliyoyaandika hapa tumeyapokea na tutayafanya kazi kama ambavyo yameletwa na kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mambo machache sana ya kuchangia kwa maana ya kuongezea tu. Jambo la kwanza ni kwamba kuna hizi fedha za maendeleo 40% kwa 60% zinazotokana na mapato ya ndani katika halmashauri zetu na sasa hivi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni alitupatia fedha kupitia fedha za Mradi wa Mapambano Mhidi ya UVIKO-19 na fedha nyingi tulipeleka katika madarasa na inaonyesha kabisa kuna baadhi ya halmashauri kule wanataka kujifichia humu ndani ili miradi ya maendeleo iliyopangwa katika asilimia 40 na 60 waingizie katika hizi fedha za UVIKO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kamati ilivyoagiza na sisi tumeshaziagiza halmashauri zote nchini kuleta taarifa ya fedha za maendeleo ya zile asilimia 40 kwa 60 zinazotokana na mapato ya ndani zisihusishwe na fedha ambazo alizozitoa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, hilo tulishaliagiza na kabla ya mchakato wa Bunge la Bajeti kuanza taarifa hiyo tutakuwa tunailleta kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili suala la 10% ambazo zinatokana na mikopo katika makundi maalum kwa maana ya wanawake, vijana pamoja na watu wenye mahitaji maalum kamati imeomba kwamba tulete marekebisho ya sheria pamoja na kanuni zake kwa sababu hilli tumeliona ni changamoto kwetu sote na Waziri wangu Mheshimiwa Bashungwa ameniambia kwamba tulipokee na kwamba hili tutaleta marekebisho ya sheria kamati itatushauri pamoja na Bunge lako tukufu ili tupate namna bora ambayo hizi fedha kila wakati zitakapokuwa zinatoka ziende zikafanye kazi ama tija ile ambayo imekusudiwa na Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais mwenyewe.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni kuhusu ajira ambalo tayari Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ameshalizungumzia. Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeomba ajira sasa hivi kama nafasi 10,000 tumeomba kibali ambapo tukishapatiwa maana yake tutazitangaza ili ziende zikaongeze idadi ya walimu katika yale madarasa 15,000 ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa. Kwa hiyo, tusubiri Serikali ipo katika mchakato wake na inafanya kazi kwa kusikilizana litakapokuwa limekamilika Bunge lako Tukufu litapewa hiyo taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu *TARURA* watu wengi wamezungumzia sana na Bunge lilishatuagiza hapa wiki iliyopita kwamba tulete taarifa ya tathmini ambayo tayari taarifa ya awali tumeshapatiwa kwa hiyo sasa hivi tunaandaa taarifa ya kina na tutaleta kwako katika Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tu niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge moja ya kazi nzuri ambayo amefanya Mheshimiwa Rais ni kupeleka fedha za kutosha kwenda kwenye halmashauri zetu pamoja na Majimbo hizi hela kwa ajili ya ujenzi wa barabara, na mfano mzuri zile shilingi milioni 500 kwenda kwenye Majimbo Mheshimiwa Rais ametoa fedha zote milioni 500 kwenda katika Majimbo 214 sawa sawa na bilioni 107. Kwa hiyo, zile ambazo tulishapitisha ndani ya Bunge kupitia mfuko wa Hazina Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ametimiza ahadi yake na zipo katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kinachofanyika huko tu ni kuhakikisha zifanye ile kazi iliyokusudiwa na Wabunge hawa wanapaswa na wao kutusaidia kuhakikisha kwamba wanazifuatilia hizi fedha zifanye ile kazi ambayo Mheshimiwa Rais amekusudia ifanyike kwa watanzania wote. Tuwaahidi tu kwamba tutakuwa tunatoa taarifa kwa kila Mbunge na sasa hivi tunaandaa mfumo ambao utasaidia sasa kuwa tunatoa taarifa kila fedha ambayo inatoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI iwe ni kama kwenye darasa iwe ni kama kwenye barabara iwe ni kama kwenye zahanati tunataka

tutoe taarifa kama unavyopata zile *automated mesages* za kwenye simu zile tunataka tuwe tunawafikishia Wabunge ili wahakikishe wao wanauwezo wa kufanya hiyo kazi na kufuatilia himo fedha kwa urahisi. Kwa hiyo nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja za kamati zote mbili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde sasa niwape fursa wenyeiti wa kamati zote mbili nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ili waweze kuja kuhitimisha hoja na baadaye kutoa hoja, karibu Mwenyekiti.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja. Kwanza kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kuchangia hoja hii jumla ya Wabunge sita walichangia hoja hii na niwatambue kwa majina Mheshimiwa Olelekaita Edward, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Salim Shafii, Mheshimiwa Joseph Tadayo na Mheshimiwa Asha Abdulla Juma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali nimepata fursa ya kufafanua hoja mbalimbali lakini pia imepokea maoni na ushauri wa kamati na ipo tayari kwenda kutekeleza na niwatambue Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mheshimiwa George Simbachawene Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi Daktari. Pindi Chana Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenyewe Ulemavu kwa kufafanua baadhi ya hoja na kwa kukubali kuchukua hoja za Kamati ya Katiba na Sheria kwenda kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaielekeza au sijaiomba Serikali kuhusu hizi hoja za kamati katika ujumla wake, kuna mambo kadhaa ambayo ni vizuri kamati ikaweka msisitizo kwa kuzingatia ushauri wa wajumbe wa kamati lakini

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Wabunge walioweza kuchangia kwenye Bunge lako na hoja ambazo zimetolewa na Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kuna suala la uwezeshaji vijana, Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Ndalichako ameeleza vizuri kwenye eneo hili lakini ni vizuri tukaiomba Serikali izingatie na kutekeleza mpango kazi mpango mkakati ambao unao wa miaka mitano ambapo Serikali imekubali kutenga bilioni 550 ambapo kila mwaka itatoa bilioni 102 kwa ajili ya vijana 681,000 kuwawezesha katika sekta ya ajira. Tunadhani hili ni jambo muhimu sana Serikali ikalizingatia na hili litakuwa limeboresha sana sana huduma kwa vijana kwa sababu kabla yake tulikuwa tunawahudumia vijana 20,000 tu kwa mwaka lakini sasa tutaweza kuwafikia vijana 136,000 kwa mwaka ni mapinduzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwa kibali chako eneo lingine ambalo limejadiliwa sana na Wabunge humu ndani ni eneo hili la *OSHA*. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani amelisema, Mheshimiwa Tadayo lakini Mheshimiwa Asha Abdulla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii ya *OSHA*, kwa ridhaa yako niiombe Serikali iichukulie kama mionganini mwa taasisi za mfano, ikibidi taasisi nyingine za Serikali zikajifunze kwenye taasisi hii. *OSHA* imeweza kuitambulisha Tanzania *SADC* na sasa ina dawati, kwa sababu inafanya kazi vizuri, lakini pia wana matumizi bora ya fedha wakati wa ujenzi wa jengo lao hapa Dodoma, imefanya vizuri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo haya tumeiomba *OSHA* ijaribu kuji-align na *blue print* ili kuona namna gani inaweza kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Tulitaka tutambue mchango mkubwa sana wa Mtendaji Mkuu wa taasisi hii. Nirekebishe hoja ya mjumbe wangu mmoja, alisema kwamba Mtendaji Mkuu hajathibitishwa; Mtendaji Mkuu amethibitishwa na anafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu lilikuwa ni kuhusu Kiwanda cha Viatu na Bidhaa za Ngozi (*Kilimanjaro International Leather Industry Company Limited*) na hapa pia kumekuwa na mchango wa Mheshimiwa Waziri. Sisi tunaamini kiwanda hiki, kwanza, kina fedha nyingi sana za wananchi kwa kupitia Mfuko wa PSSSF asilimia 86 ziko hapo, lakini kina tija kubwa sana kwa Watanzania wote wanaozunguka Mikoa ya Kilimanjaro, hasa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo kiwanda hiki kitafanya vizuri kitatoa ajira kubwa sana kwa Watanzania. Zaidi ya Watanzania 3,000 wanategemea kupata ajira ya moja kwa moja na Watanzania 7,000 watapata ajira zisizo za moja kwa moja. Haya ni mapinduzi makubwa sana na ni mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu kama Kamati, waangalie teknolojia tunayotumia kutengeneza viatu hivi ili tuweze kupata teknolojia bora na shindani zaidi katika masoko ya ndani na ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne, ukipenda, ni mfumo wa utoaji haki nchini. Mionganoni mwa maeneo ambayo tungependa *tu-draw attention* ya Wabunge ni namna ambavyo Serikali ya awamu ya sita imokusudia kwa dhati kabisa kusimika miguu Dodoma kama Makao Makuu. Ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu ambalo sisi kama Kamati tumetembelea leo ambalo lina *three courts* katika *campus* moja, maana yake kuna *High Court, Supreme Court na Court of Appeal*, ni kielelezo kwamba sasa mihimili yote mitatu ipo Dodoma, Serikali imesimika miguu Dodoma. Hilo tulidhani ni muhimu kulisema. Hili sasa linajibu hoja za wachangiaji walioonesha kwamba tuna changamoto kidogo kuhusu mfumo wa utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo hili na upatikanaji wa watumishi kwenye eneo hili utaongeza kasi ya utekelezaji wa jukumu hili. Nliombe Wizara sasa, tuna upungufu wa watendaji, Wizara ilifanyie kazi hili. Vile vile kuna eneo muhimu la kukamilisha Sera ya Taifa ya Mashtaka,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ilitakiwa iwe imekamilika *by December*, 2021, lakini mpaka sasa bado, pamoja na uharakishaji wa kanuni baada ya sheria kutungwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ayachukue haya na ayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwanza niiombe Serikali iyafanyie kazi maoni na mapendekezo yote ya Kamati ya Katiba na Sheria kama yalivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako lipokee Taarifa ya Kamati na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofî)*

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, hoja imeungwa mkono, acha tumalizie sasa na Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, naye aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii tena ili kuweza kujumuisha yale yote ambayo yamechangiwa na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati yetu tumpata wachangiaji 13. Kwa haraka haraka naomba niwataje, Mheshimiwa Londo, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Migilla, Mheshimiwa Jacqueline, Mheshimiwa Mwakamo, Mheshimiwa Tunza, Mheshimiwa Saasisha, Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Dkt. Alice na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Wabunge wote waliochangia katika Kamati hii, michango yao inaendelea kutuimarisha sisi kama Kamati ili kuweza kuisimamia na kuishauri Serikali katika mambo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yote yapo mambo muhimu ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyagusia na walitoa msisitizo na sisi kama Kamati tunaendelea kutoa msisitizo kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zile za asilimia 10 endapo Serikali itazisimamia vizuri zitaweza kuondoa umaskini katika nchi yetu. Ukiufigilia takwimu, zaidi ya bilioni 70 zinatolewa kila mwaka kwa kuwakopesha vijana, kina mama na watu wenye ulemavu. Fedha hizi zikitungiwa sheria na kanuni madhubuti pamoja na mifumo thabiti ya kudhibiti vikundi visiweze kukopa kiholela, vikundi viweze kurudisha, nina hakika fedha hizi zitamkomboa Mtanzania kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge pia walizungumzia sana kuhusu fedha za maendeleo. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu hapa, ameelezea namna ambavyo atatuletea kwenye Kamati. Kiukweli kama Kamati tumeona ipo haja ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ziende zikatekeleze miradi ya maendeleo. Takwimu zinaonesha kwamba bado kuna upungufu mkubwa wa madarasa kwa wanafunzi ambao watamaliza darasa la saba mwaka huu. Sasa fedha zile tutakapoamua kuzibadilishia matumizi, tukazipeleka kwenye matumizi mengine ambayo si ya miundombinu ya elimu na wala si ya miundombinu ya afya; tatizo hili tutaendelea kuwa nalo. Hivyo basi, kama Kamati tunaendelea kusisitiza kwamba, fedha hizi ziendelee kutumika katika miradi ya maendeleo hasa miundombinu ya elimu na miundombinu ya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumzia sana suala la Walimu wastaaafu, Walimu waliofariki na kada nyingine mbalimbali zilizostaafu na kufariki.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kamati tutaendelea kusisitiza, nafasi hizi za watu ambao wamestaafu na kufariki ziweze kujazwa mara moja. Kwa maana nafasi hizi zikijazwa tunaendelea kuondoa upungufu mkubwa wa Walimu na kada mbalimbali ambazo zinatokana na mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa sana suala la majanga ya moto. Tumeona, majanga ya moto yamekuwa kizungumkuti sana nchini kwetu, hasa katika maeneo ya masoko. Kamati itaendelea kusimamia na kuishauri Serikali namna bora ya kufanya ili majanga haya ya moto yasiendelee kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia majanga haya ya moto utaona kila mahali ambapo moto umetokea tunaambiwa chanzo ni umeme. Tunajiuliza, je umeme huu unatoa hitilafu usiku tu na mchana unakuwa haupo? Sasa, ni moja ya majukumu ya Kamati hii kuona ni namna gani tutaendelea kufuatilia na kuikomesha hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la mifumo mbalimbali, hivyo basi Mamlaka yetu ya Serikali Mtandao (*eGA*) tutaendelea kuisimamia na kuhakikisha maeneo yote ambayo mitandao ya kielektroniki inatakiwa iwekwe, basi *eGA* ishiriki katika kuweka mitandao hiyo ili kuepusha mitandao isiendelee kutosomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ina mambo mengi na kwa sababu ya muda, naomba sasa Bunge lako lipokee taarifa hii na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati hii ili iweze kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofifi*)

**MHE DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Hoja imeungwa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mkono, sasa kwa ujumla wake naomba niwahoji Wabunge, kwamba taarifa, maoni na mapendekezo ya Kamati zote mbili kama yaanafikiwa kuwa Maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na Maoni na mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa yalipitishwa kuwa Maazimio ya Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nawashukuru sana. Kwa mujibu wa kanuni ya 92 (3)(4) nitamke rasmi kwamba taarifa zote hizi mbili za Kamati hizi mbili pamoja na maoni na mapendekezo yake sasa yamekuwa ni maazimio ya Bunge. Kwa hiyo nitarajie sana kutoka Serikalini kwa jinsi ambavyo mmeonesha ushirikiano wenu kwenye Kamati hizi katika mijadala mbalimbali na jinsi ambavyo Mawaziri mmepokea na kuona kwamba maoni haya ya Kamati hizi ni muhimu, basi niwatakie kila la kheri kwenye utekelezaji na baadaye kuweza kuleta mrejesho kwenye Kamati zetu.

Baada ya kusema hayo, kabla sijamaliza kazi naomba tena niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kwamba, Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwenda kuangalia afya zetu kwa ajili ya kliniki maalum ya uchunguzi wa afya ya moyo, macho, kinywa na meno, masikio, pua na koo pamoja na huduma za ushauri wa afya. Huduma hii itatolewa kuanzia leo tarehe 14 hadi 18 Februari, 2022. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kupata huduma hiyo.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge ninawatakitia jioni njema na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa nane mchana.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 15 Februari, 2022, Saa Nane Kamili Mchana)*